BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA SHERIA, UTAWALA BORA NA IDARA MAALUM YA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

FEBRUARI, 2018

BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA SHERIA, UTAWALA BORA NA IDARA MAALUM YA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

YALIOMO

SEHEMU YA KWANZA 1

1. UTANGULIZI 1

1.1 MALENGO YA KAZI NA MUDA WA KAZI ZA KAMATI 2

1.2 MUUNDO WA KAMATI 3

1.3 HADIDU REJEA 3

SEHEMU YA PILI 4

2. WIZARA YA NCHI OFISI YA RAIS - KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA 4

IDARA YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU PEMBA 13

2.1.7 IDARA YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO *(E – GOVERNMENT)* 14

2.1.8 IDARA YA UTAWALA BORA 16

2.1.9 OFISI YA AFISA MDHAMINI PEMBA 18

2.1.10 TAASISI ZINAZOJITEGEMEA AMBAZO ZINASIMAMIWA NA WIZARA YA NCHI, OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTWALA BORA 20

2.1.11 AFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI 20

2.1.12 OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI (CAG) 23

OFISI YA MKAGUZI NA MDHIBITI WA HESABU ZA SERIKALI PEMBA 24

2.1.13 MAHAKAMA 25

2.1.13.1 UJENZI WA MAHAKAMA KUU, TUNGUU 26

2.1.13.2 MAHAKAMA KUU PEMBA 27

2.1.13.3 MATENGENEZO YA MAHAKAMA YA WILAYA MWANAKWEREKWE 29

2.1.13.4 MAHAKAMA YA WILAYA YA MKOKOTONI 30

2.1.13.5 MAHAKAMA YA WILAYA YA KONDE 32

2.1.14 OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA 33

OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA PEMBA 34

2.1.15 OFISI YA MUFTI 39

2.1.16 TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA 41

2.1.17 KAMISHENI YA UTUMISHI SERIKALINI 43

2.1.18 TUME YA UTUMISHI SERIKALINI 44

2.1.19 KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA 46

2.1.20 OFISI YA MSAJILI WA HAKIMILIKI 50
OFISI YA MSAJILI WA HAKIMILIKI – PEMBA 50
2.1.21 TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR 52
2.1.22 MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI (ZAECA) 53
MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI PEMBA 54
2.1.23 CHUO CHA UTAWALA WA UMMA 57
SEHEMU YA TATU 59
3. WIZARA YA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ 59
3.1 UTANGULIZI 59
3.2 IDARA NA TAASISI ZA WIZARA YA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ 61
3.2.1 IDARA ZA KAWAIDA 61
3.2.2 MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MIKOA 61
3.2.3 MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA 61
3.2.4 IDARA MAALUM ZA SMZ 62
3.3 IDARA ZA KAWAIDA 62
3.3.1 IDARA YA MIAPANGO SERA NA UTAFITI 62
3.3.2 IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI 63
3.3.3 IDARA YA URATIBU WA IDARA MAALUM ZA SMZ 64
3.3.4 IDARA YA URATIBU WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA 65
3.3.5 AFISI YA USAJILI WA VIZAZI, VIFO NA KADI ZA UTAMBULISHO 65
3.3.5.1 OFISI YA USAJILI WA VIZAZI, VIFO NA KADI ZA UTAMBULISHO WILAYA YA WETE 66
3.3.5.2 OFISI YA VIZAZI, VIFO NA KADI ZA UTAMBULISHO WILAYA YA MICHEWENI 67
3.3.5.3 OFISI YA VIZAZI NA VIFO, NA OFISI YA KADI ZA UTAMBULISHO WILAYA YA CHAKE – CHAKE 68
3.3.6 OFISI YA AFISA MDHAMINI PEMBA 70
3.4 MAMLAKA YA SERIKALI ZA MIKOA 72
3.4.1 MKOA WA MJINI MAGHARIBI 72
3.4.2 MKOA WA KUSINI UNGUJA 73
3.4.3 MKOA WA KASKAZINI UNGUJA 75

3.4.4 MKOA WA KUSINI PEMBA 77
3.4.5 MKOA WA KASKAZINI PEMBA 80
3.5 MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA 84
3.5.1 BARAZA LA MJI WETE 85
3.5.2 BARAZA LA MJI MKOANI 87
3.5.3 BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE 90
3.5.4 WILAYA YA KATI UNGUJA 93
3.5.5 WILAYA NDOGO TUMBATU 94
3.5.6 ZIARA YA KAMATI KATIKA MANISPAA YA DODOMA KATIKA WIZARA YA OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA 96
3.6 IDARA MAALUM ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR 99
3.6.1 KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM) 100
KIKOSI CHA KMKM MASINGINI 102
KIKOSI CHA KMKM – MARUMBI 103
KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM) UNGUJA UKUU 104
3.6.2 IDARA YA CHUO CHA MAFUNZO 105
CHUO CHA MAFUNZO KINUMOSHI 107
3.6.3 IDARA YA JESHI LA KUJENGA UCHUMI ZANZIBAR 108
JESHI LA KUJENGA UCHUMI BAMBI MATOLA NA BAMBI 'KIM' 111
KIKOSI CHA JKU MACHUI 113
KIKOSI CHA JKU – KAMA 114
3.6.4 KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU) 116
3.6.5 KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR (KVZ) 119
KIWANDA CHA KUTENGENEZEA VIATU CHA KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR (KVZ) MTONI 120
KIWANDA CHA USHONI CHA IDARA MAALUM ZA SMZ 121
UJENZI WA NYUMBA ZA MAAFISA NA MAHANGA YA WAPIGANAJI KWA IDARA MAALUM ZA SMZ PEMBA 123
SEHEMU YA NNE 125
4. HITIMISHO 125

SEHEMU YA KWANZA

1. UTANGULIZI

Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ni Kamati ya Kudumu ambayo imeundwa na kupewa majukumu kwa mujibu wa kifungu cha *85* cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka *1984* na kanuni ya *106(1)* ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Toleo la mwaka *2016*. Majukumu ya Kamati yameelezwa katika *Jadweli la Kwanza* la Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar kama ifuatavyo:

(i) Kufuatili utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia.

(ii) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na Hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza.

(iii) Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi ya Wizara husika.

(iv) Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.

(v) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.

(vi) Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika.

(vii) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo.

(viii) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati hii inasimamia utekelezaji wa majukumu ya wizara *mbili (2)* zifuatazo:

(a) Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
(b) Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

1.1 MALENGO YA KAZI NA MUDA WA KAZI ZA KAMATI

Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Kamati ilitekeleza kazi zake kwa malengo yafuatayo:

(a) Kufuatilia maagizo yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka *2016/2017*.
(b) Kufuatilia ahadi za Serikali zilizotolewa katika Mkutano wa Bajeti wa mwaka *2017/2018*.
(c) Kufuatilia utekelezaji wa Bajeti (kazi za kawaida na kazi za maendeleo) ya mwaka *2017/2018*.
(d) Kufuatilia ukusanyaji wa mapato katika Taasisi za Serikali pamoja na kufanya ziara katika Taasisi husika.

Katika mwaka wa fedha*2017/2018*, Kamati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki *sita (6)* katika utaratibu ufuatao:

(i) Kuanzia tarehe *14* hadi *25 Agosti, 2017*, Kamati ilitekeleza majukumu yake kisiwani Pemba kwa wiki ya mwanzo na Unguja kwa wiki ya pili.
(ii) Kuanzia tarehe *13* hadi *17 Novemba, 2017*, Kamati ilitembelea baadhi ya idara/taasisi zilizo chini ya Wizara husika kwa kila Wizara kwa muda wa wiki *moja (1)* kwa upande wa kisiwa cha Unguja. Katika ziara hizo, Kamati ilitembelea miradi na shughuli zinazotekeleza na idara/taasisi hizo pamoja na kupokea taarifa ya utekelezaji.
(iii) Kuanzia tarehe *15 Januari, 2018* hadi *26 Januari, 2018*, Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa muda wa wiki *moja (1)* kwa upande wa Unguja na wiki *moja (1)* kwa upande wa Pemba.

1.2 MUUNDO WA KAMATI

Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum inaundwa na Wajumbe wafuatao:

Nam.	**Jina**	**Wadhifa**
1.	Mhe. Machano Othman Said	Mwenyekiti
2.	Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf	Mjumbe
4.	Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	Mjumbe
5.	Mhe. Ali Khamis Bakari	Mjumbe
6.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Mjumbe
7.	Mhe. Suleiman Makame Ali	Mjumbe
8.	Ndg. Ali Alawy Ali	Katibu
9.	Ndg. Haji Jecha Salim	Katibu

1.3 HADIDU REJEA

Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum katika kutekeleza majukumu yake ilitumia:

(a) Katiba ya Zanzibar ya mwaka *1984*.

(b) Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka *2016*.

(c) Ripoti ya Kamati ya mwaka *2016/2017*.

(d) Hotuba za Bajeti za *Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora* pamoja na *Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ* kwa mwaka wa fedha *2017/2018.*

(e) Taarifa za Utekelezaji wa bajeti za Wizara na Taasisi husika.

SEHEMU YA PILI

2. WIZARA YA NCHI OFISI YA RAIS -KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina jukumu la kusimamia na kuhakikisha kuwa masuala ya Katiba na Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora yanaimarika kwa kasi kubwa ili kuweza kuleta ufanisi na faida pamoja na maendeleo kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wananchi kwa ujumla. Aidha, wizara hii inalojukumu la kuhakikisha dhana kamili ya utawala bora imesimama na kumfikia kila mmoja katika misingi ya haki na sheria ili kujenga misingi iliyo bora ya demokrasia.

Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inasimamia jumla ya programu*13*, kati ya hizo, programu*tano (5)* zinasimamiwa na kutekelezwa kupitia idara zilizo chini ya Katibu Mkuu na programu*nane (8)* zinatekelezwa na taasisi zinazojitegemea.

Aidha, Wizara hiiinaundwa na Idara zifuatazo:

(a) Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
(b) Idara ya Uendeshaji na Utumishi.
(c) Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi.
(d) Idara ya Mipango na Rasilimali Watu.
(e) Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa.
(f) Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(e – Government)*.
(g) Idara ya Utawala Bora.
(h) Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba.

Vilevile, Wizara hii inasimamia Taasisi zinazojitegemea zifuatazo:

(a) Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(b) Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
(c) Mahakama.
(d) Tume ya Utumishi ya Mahakama.
(e) Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.
(f) Ofisi ya Mufti.
(g) Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma.
(h) Kamisheni ya Utumishi wa Umma.
(i) Tume ya Utumishi Serikalini.
(j) Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana.
(k) Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki.
(l) Tume ya Kurekebisha Sheria.
(m) Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi.

2.1.1 IDARA ZILIZO CHINI YA WIZARA YA NCHI, OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

2.1.2 IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ni kiungo muhimu katika Wizara hii pamoja na Taasisi zake. Idara hii ina jukumu la kuratibu shughuli zote za Wizara.

Katika kipindi cha mwaka huu, Idara iliandaa ripoti *nne (4)* za utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kuziwasilisha katika mamlaka husika.

Vilevile, Idara imekamilisha kuandaa Sera ya Mafunzo kwa Watumishi wa Umma ambayo inatarajiwa kuwasilishwa katika kikao cha Uongozi wa Wizara na baadae katika kikao cha Makatibu Wakuu.

Pia, Sera ya Malipo kwa Watumishi wa Umma na Wanasiasa imefanyiwa tafsiri kwa lugha nyepesi ya Kiswahili.

Aidha, Idara imepatiwa vitendea kazi na mafunzo ya muda mfupi kwa takriban watumishi 60 katika fani ya Takwimu na Ufuatiliaji na Tathmini (M&E). Mafunzo hayo yalihusiana na utayarishaji wa ripoti za utekelezaji, uandaaji wa mipango na umuhimu wa misingi bora ya ufuatiliaji na tathmini ya kazi za Ofisi.

Idara imeratibu, shughuli za Mradi wa Mageuzi katika Sekta ya Sheria chini ya ufadhili wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na "United Nations Development Fund (UNDP)" ambapo kwa kipindi hiki ulilenga kukamilisha rasimu za Sera, Miongozo na Sheria mbalimbali zinazoongoza utendaji wa vyombo vya sheria. Shughuli zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha, kuzindua na kusambaza Sera ya Mswada wa Kisheria ya Zanzibar.

Hata hivyo,Uzinduzi huo ulikwenda sambamba na kujenga uelewa kupitia semina, mikutano na kurusha hewani vipindi kupitia Redio Jamii Micheweni na Mkoani Pemba. Aidha, maandalizi ya Sheria ya Msaada wa Kisheria yameanza kwa kuwa na rasimu ya awali. Kuzinduliwa kwa Sera hii na kukamilika kwa sheria kutatoa fursa na kurahisisha upatikanaji wa haki kwa wananchi wasio na uwezo na wenye mahitaji maalum.

Aidha, Ofisi Kuu Pemba kwa kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ilifanikiwa kuratibu mkutano juu ya sera ya msaada wa kisheria. Mafunzo hayo yalifanyika tarehe 15 – 16 Disemba, 2017 ambayo yalikuwa na lengo la kujenga uelewa kuhusiana na sera hiyo kwa wananchi pamoja na kuainisha maeneo ambayo hayakutajwa katika sera hiyo.

2.1.3 IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Idara ya Uendashaji na Utumishi ina jukumu la utoaji wa huduma za uendeshaji na utumishi zikiwemo malipo ya umeme, ununuzi wa vifaa mbalimbali vya Ofisi, kufanya matengenezo madogomadogo na kulipa stahiki mbalimbali za watendaji wa Ofisi pamoja na kulipia gharama za

mafunzo kwa watendaji waliopo vyuoni.Pia, jumla ya watumishi 25 wamelipwa stahiki zao na watumishi wengine 66 wamelipiwa gharama za mafunzo. Miongoni mwao, watumishi wanne (4) wamelipiwa mafunzo ya muda mrefu, watumishi watano (5) wamelipiwa posho la mavazi na kujikimu na watumishi 57 wamepatiwa mafunzo ya Miundo ya Utumishi na Mfumo wa kielektroniki wa rasilimali watu.

Vilevile, Ofisi Kuu Pemba kupitia Idara ya Utumishi na Uendeshaji, ilifanikiwa kutoa mafunzo kwa maofisa utumishi wa Wizara 13 kwa upande wa Pemba pamoja na Taasisi za Wizara hizo. Mafunzo hayo yalifanyika tarehe 25 Oktoba, 2017 na 23 Novemba, 2017 ambayo yalikuwa na lengo la kutoa uelewa na kuwataka kwa maofisa Utumishi kuzifahamu na kuzifanyia kazi kwa vitendo Sheria na Kanuni za utumishi wa umma pamoja na kuwafundisha moja kwa moja watumishi wengine katika Wizara/Taasisi zao ili kujenga misingi ya uadilifu na uwajibikaji kwa watumishi wa Umma. Ofisi ilinunua jumla ya Kanuni za Utumishi 13 na kuzigawa kwa maofisa utumishi waliohudhuria katika mafunzo hayo.

2.1.4 IDARA YA MIUNDO YA TAASISI, UTUMISHI NA MASLAHI YA WATUMISHI

Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi imefuatilia na kufanya tathmini juu ya Miundo ya Utumishi, Mkataba wa Utoaji wa Huduma kwa mteja na upimaji utendaji kazi katika Wizara za Serikali. Aidha, Muongozo wa Mkataba wa Utoaji wa Huduma kwa Mteja umetolewa kwa Wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kuhakikisha kwamba unazinduliwa rasmi na kuanza kutumika ndani ya robo mwaka ya tatu katika mwaka wa fedha *2017/2018*.

Vile vile, Kamati imeelezwa kuwa Idara katika kujenga uwezo wa kitaalamu na kubadilishana uzoefu, timu ya Maofisa ikiongozwa na Mkurugenzi ilifanya ziara ya kikazi Tanzania Bara katika Taasisi za

Utumishi wa Umma na kujifunza masuala mbalimbali ya kiutumishi ikiwemo masuala ya Mishahara na Posho kwa Mashirika ya Umma na uwekaji na uondoshaji kizuizi kwa Watumishi wa Umma.

Aidha, Kamati inapongeza sana juhudi zilizofanywa na Idara hii kwa kupitia na kupendekeza maposho kwa Watumishi wa Serikali Kuu, Mashirika na Wakala wa Serikali, ambapo tayari imefanyika. Muongozo umeandaliwa na kuwasilishwa Serikalini kwa lengo la kupendekeza utaratibu utakaotumika katika Mamlaka, Mashirika na Taasisi zinazojitegemea kuhusiana na malipo ya Mishahara na Posho kwa Watumishi na Watendaji wa Taasisi hizo.

Pia, Kamati imeelezwa kufanyika kwa Tathmini ya Kazi *(Job Evaluation)* na kuweka madaraja kwa mujibu wa uzito wa kazi husika ambapo tathmini hiyo imeshafanyika, ni imani ya Kamati kuwa maslahi ya watumishi yamezingatiwa na yataboreshwa vyema ili kukidhi maisha halisi ya Mzanzibari.

Vile vile, kazi ya kufanya mapitio ya Miundo ya Utumishi na Miundo ya Mishahara kutokana na matokeo ya Tathmini ya kazi na Madaraja imefanyika. Aidha, Idara imepitia na kuimarisha Miundo ya Utumishi ili kuiwezesha na kwenda sambamba na matokeo ya Tathimini ya kazi na Madaraja.

Idara kwa kushirikiana na Bodi ya Mishahara na Maslahi ya Watumishi ya Tanzania Bara, Tathmini ya Kazi na Madaraja imefanyika ambapo hatua iliyofikiwa sasa ni kuandaa ripoti ya kazi hiyo na kuiwasilisha Serikalini kwa mazingatio zaidi.

Vilevile, kwa upande wa**Ofisi Kuu Pemba** kupitia Idara hii ilifanya ukaguzi kwa Taasisi mbalimbali za Serikali kisiwani Pemba. Ukaguzi huo ulikuwa na lengo la kuangalia kiwango cha utendaji wa kila mtumishi wa

umma kwamba anayafahamu majukumu yake ili kuongeza ufanisi katika maeneo ya kazi. Jumla ya taasisi *sita (6)* zifuatazo zilifanyiwa ukaguzi huo:

(a) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali;
(b) Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko;
(c) Wizara ya Afya;
(d) Baraza la Mji Wete;
(e) Ofisi za Baraza la Wawakilishi; na
(f) Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Pia, Ofisi Kuu Pemba imetoa mafunzo elekezi kwa Maafisa utumishi juu ya muelekeo wa kuboresha maslahi ya maofisa hao na kupatiwa stahiki zao kutokana na uzito wa majukumu yao.

2.1.5 IDARA YA MIPANGO NA RASILIMALI WATU

Kamati kupitia Idara ya Mipango ya Rasilimali Watu imeelezwa kuwa katika kipindi cha mwaka huu iliandaa na kutoa mafunzo kwa watumiaji *145* wa Mfumo wa Taarifa za Utumishi wa Umma Unguja na Pemba.

Aidha, Idara imeratibu mafunzo yanayotolewa na washirika wa maendeleo ambapo jumla ya nafasi *26* za mafunzo zimeratibiwa. Ofisi imeshiriki Mkutano wa Kimataifa wa Utawala na Uongozi *(AAPAM)* ambapo masuala mbalimbali ya uendeshaji wa Taasisi, kikanda na kimataifa yamejadiliwa.

Vilevile, Idara imefanya mafunzo kwa wasimamizi wa Mpango wa Uandaaji Viongozi katika Utumishi wa Umma ambayo yamejumuisha Maafisa Wadhamini, Makatibu Tawala, Wakurugenzi wa Mabaraza ya Miji, Halmashauri na Maafisa Utumishi kwa upande wa Pemba.

Ofisi Kuu Pemba kupitia Idara ya Mipango Rasilimali Watu, imepokea watumishi mbalimbali kutoka masomoni katika vyuo mbali mbali na kuwarudisha katika wizara zao ili kupangiwa kazi kama taratibu za

kiutumishi zinavyoelekeza pamoja na kuelekeza kupatiwa stahiki zao za likizo kwa mujibu wa kanuni ya *77 (3)* ya Kanuni za Utumishi wa Umma. Jumla ya watumishi *58* kwa kipindi hiki wamepokelewa.

2.1.6 IDARAYA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZA TAIFA

Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa, Zanzibar ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu Zanzibar, nambari 3 ya mwaka 2008. Taasisi hii mbali ya majukumu mengine, ina jukumu kuu la kuhifadhi nyaraka na kumbukumbu mbalimbali za taifa kwa ajili ya kuweka kumbukumbu, kuhifadhi pamoja na kutunza historia ya Zanzibar. Nyaraka zinazohifadhiwa katika Taasisi hii sio siri labda kuwe na hatua au dharura maalum. Hivyo, wananchi wana haki ya kwenda na kutumia kwa mujibu wa sheria na taratibu husika.

Aidha, Kamati imeelezwa kwamba; Taasisi ilifanya ukaguzi wa kumbukumbu kwa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo pamoja na Wizara ya Afya. Baada ya ukaguzi huo, Wizara hizo zimepewa ushauri wa utunzaji na uhifadhi bora wa kumbukumbu.

Vilevile, kumbukumbu zote zilizopo katika wizara/taasisi za Serikali baada ya kufikia miaka *30*, hulazimia kupelekwa katika Taasisi hii kwa ajili ya matumizi ya jamii. Vilevile, Taasisi huzipatia wizara/taasisi ushauri na maelekezo juu ya namna ya kuhifadhi kumbukumbu kabla hazijafikiwa muda wa kuwasilishwa katika Taasisi husika.

Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum katika kipindi cha mwaka wa fedha uliopitakatika ziara zake kwa Taasisi hii ilibaini kuwepo kwa changamoto nyingi ambazo kwa sasa zimeshatatuliwa kwa kiasi kikubwa kwani Taasisi hiyo imeweka vipoza hewa, *'files jackets'*, *'masks'*, jengo limeezekwa na wafanyakazi kupimwa afya zao. Hivyo**, Kamati inatoa pongezi za dhati kwa hatua hiyo iliyofikiwa**.

MAFANIKIOYA IDARA YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU

Hadi kufikia sasa, Taasisi hii imepata mafanikio yafuatayo:

(a) Malengo yaliyowekwa yameweza kufikiwa.
(b) Uwekaji wa vipoza hewa.
(c) Jengo limeezekwa.
(d) Majalada *23* kutoka mfumo wa karatasi kwenda kwenye mfumo wa ki – elektroniki yamehaulishwa.
(e) Taarifa za kihistoria *"Oral History"* za watu binafsi zimekusanywa na kuhifadhiwa.
(f) Mazingira ya ofisi yameboreshwa kwa kupakwa rangi na kuwekwa *'tiles'*.
(g) Jengo la ofisi Pemba nalo limeboreshwa na kuwa nahadhi inayotakiwa.
(h) Taasisi imemleta mshauri elekezi kwa ajili ya kuja kuangalia namna nzuri ya kuweza kuhifadhi nyaraka na kutoa huduma kwa jamii.

CHANGAMOTOZA IDARA YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU

Licha ya kupatikana kwa mafanikio katika Taasisi hii, pia zipo changamoto mbalimbali zinazoikabili, kama ifuatavyo:

(a) Ukusanyaji na uhifadhi mdogo wa nyaraka kutokana nakukosekana kwa eneo la kuhifadhia nyaraka hizo katika Taasisi hiikwanihakuna nafasi katika jengo lao.
(b) Wizara/taasisi nyingi bado hazijatenga maeneo/vyumba maalum vya kuhifadhia kumbukumbu licha ya kushauriwa na kupewa maelekezo ya kufanya hivyo na kuziacha nyaraka ovyo.
(c) Ukosefu wa usafiri wa uhakika katika kutekelezea majukumu ya Taasisi.
(d) Hakuna sehemu/kituo maalumcha taifa cha kuhifadhia nyaraka (*Documents Recording Centre*). Hivyo, nyaraka ziliopo sasa katika Taasisi hii karibu zote ni za kabla ya *Mapinduzi ya mwaka 1964*.

(e) Kutokana na uwepo wa mashine za kisasa katika taasisi hii, matumizi ya umeme yamekuwa makubwa kwani kwa mwezi mmoja inakadiriwa kutumika zaidi ya *Tshs. Milioni Mbili (2,000,000)*kwa Unguja tu.

Ilikufikia lengo la kuhifadhi nakukusanya kumbukumbu kwa ajili ya kizazi kijacho, mambo yafuatayo yanalazimika kuzingatiwa:

(a) Taasisi imewahi kutoa dokezo kwa wizara/taasisi juu ya namna ya kuhifadhi kumbukumbu lakini halifuatwi kwani imebainika kuwa baadhi ya ofisi zinapohama katika majengo yao, huacha kumbukumbu zao katika majengo waliyohama.
(b) Tasisi imeagiza kila wizara/taasisi iweke chumba maalum cha kuhifadhia kumbukumbu.
(c) Majengo mapya yanayojengwa wakati huu yawekewe vyumba maalum vya kuhifadhia kumbukumbu.
(d) Serikali iharakishe ujenzi wa kituo cha taifa cha kuhifadhia nyaraka *(Documents Recording Centre)* ambapo Kamati imeelezwa kuwa eneo limeshapatikana kwa ajili ujenzi huo.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

Kamati inatoa maoni na maagizo yafuatayo:

(a) Kamati **inaagiza**Taasisi hii kufuatilia kwa karibu hatua zilizofikiwa juu ya ujenzi wa jengo jipya la ofisi huko Koani, katika kukabiliana na ufinyu wa eneo la kuhifadhia nyaraka na utekelezaji wa majukumu yao.
(b) Kamati **inashauri**Taasisi kufuatilia maendeleo ya ukusanyaji na utunzaji wa nyaraka katika maeneo waliyoyakagua ili kubaini kama kuna hatua zozote zilizochukuliwa.
(c) Kamati **inashauri** kufanyiwa marekebisho kwa sheriaya nyaraka na kumbukumbu ili iweze kutoa fursa kwa Mkurugenzi wa Nyarakakuwakabili na kuwatia hatiani wale wote wanaokiuka taratibu za uhifadhi wa nyarakana

kumbukumbuili kuepusha upotevu na uharibifu wa nyaraka na kumbukumbu nchini.

(d) Kamati **inshauri** Serikali kupitia Wizara hii kuandaa utaratibu maalum utakaosaidia kulinda na kuhifadhi nyaraka na kumbukumbu za nchi kwa kujenga kituo kikuu kitakachosaidia kuhifadhi kwa wingi.

IDARA YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU PEMBA

Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa Pemba, iliendelea na kazi za kawaida kwa kutoa huduma na mafunzo kwa wageni wa ndani na nje ya nchi juu ya umuhimu wa utunzaji wa kumbukumbu. Taasisi ilipokea wageni kutoka sehemu mbalimbali ambao walitaka kupata huduma ya utumiaji kumbukumbu ili kuweza kufamikisha shughuli zao za kila siku.

Pia, Taasisi iliendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wa masjala juu ya kuhifadhi, kulinda na utunzaji sahihi wa kumbukumbu, mafunzo hayo yalitolewa kwa watumishi kutoka Wizara ya Afya, Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Wizara ya Ardhi, Maji Nishati na Mazingira – Pemba,

Vilevile,Taasisi imefanikiwa kuziingiza kumbukumbu kwenye mfumo wa digitali pamoja na kufanya tathmini ya kumbukumbu na kuziingiza kwenye miongozo *(guide)*.

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI TAASISIYA NYARAKA NA KUMBUKUMBU PEMBA

(i) Ukosefu wa usafiri kwa watendaji na maafisa wa Idara.

(ii) Ufinyu wa bajeti ambao unapelekea Taasisi kushindwa kutekeleza baadhi ya majukumu yake ipasavyo.

(iii) Taasisi imepata fursa ya kupata jengo jipya, hata hivyo jengo hilo linaathiriwa na vumbi linalotokana na barabara iliyopita mbele ya jengo hilo, hivyo kupelekea kuchakaa kwa haraka katika sehemu za nje.

(iv) Upungufu wa vifaa kama vile makabati ya kuhifadhia nyaraka na vitu mbalimbali kama vile fotokopi na*'scanners'*.

(v) Upotevu wa baadhi ya kumbukumbu za mawizara kutokana na kuhamahama kwa wizara au Idara na kutozingatia umuhimu wa kumbukumbu hizo.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(a) Kamati inashauri Idara ya Nyaraka kwa kushirikiana na Tume ya Utumishi Serikalini kuhakikisha watumishi wote wa Serikali na wale wasio wa kiserikali wamepatiwa elimu juu ya namna ya kuhifadhi kumbukumbu katika sehemu zao za kazi. Aidha, wakuu wote wa Taasisi za Umma kuwachukulia hatua watendaji wao ambao wataharibu kumbukumbu kwa namna moja au nyengine ambayo itapelekea kupotosha au kupoteza taarifa husika.

(b) Kamati inashauri Serikali kufanya utaratibu wa kuwapatia usafiri Taasisi hii kwa vile kazi zao ni za ufutailiaji na umuhimu wake tuanauona ulivyo katika nchi yetu.

(c) Kamati inaagiza Idara ya Nyaraka ofisi kuu Unguja kusaidia sana kupunguza tatizo la uhaba wa vifaa katika ofisi ya Pemba ili kuendana na hadhi na umuhimu wa Idara hii.

(d) Kamati inashauri kupatiwa watumishi wataalamu katika fani za *Informatin System* na TEHAMA ili kuweka mazingira bora kiutendaji kwa ofisi hii.

2.1.7 IDARA YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO *(E – GOVERNMENT)*

Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ilitembelea ofisi ya Idara ya Serikali Mtandao Mazizini na kujionea utekelzaji wa majukumu yao mbali mbali, ambapo Ofisiimefanikiwa kufanya mapitio ya mpango mkakati wa Serikali mtandao wa miaka *mitano (5)* ambao umeshakamilika kwa asilimia *50*. Aidha, muongozo wa usimamizi wa miradi ya *TEHAMA* katika Utumishi wa Umma umetayarishwa na hatua inayofuata ni kupelekwa kwa wahusika wengine kwa ajili ya kupata maoni yao.

Vile vile, Idara imefanya tathmini ya mifumo ya "*software*" ya Serikali Mtandao na kutoa ripoti paamoja na kutayarisha maandiko ya awali *(concept paper)* za maeneo ya kufanya tafiti ya Serikali Mtandao.

Vilevile, mafunzo ya kitaalamu yametolewa kwa watendaji wa *TEHAMA* juu ya kudhibiti na kujikinga na Maambukizi ya Uhalifu Mitandaoni (*Ethical Hacker).* Pia, Idara imeratibu Miradi ya Serikali Mtandao *(e – Health* na *e – tax)* pamoja na kuratibu vikao vya wataalamu wa Kamati ya Kiufundi na Kamati ya Usimamizi za Serikali Mtandao ambapo Ripoti za Utekelezaji zinaandaliwa katika kila baada ya miezi *sita (6).*

Aidha, Idara imefanikiwa kutengeneza mfumo wa Tovuti na Baraua Pepe ya Serikali kwa ajili ya upokeaji na utumiaji wa taarifa mbali mbali za serikali kwa usalama zaidi.

Sambamba na hayo, Idara imeandaa Rasimu ya Sheria ya Kuanzishwa kwa wakala wa serikali mtandao, na kupitishwa na wahusika mbali mbali na kuuchangia kilicho bakia ni kupelekwa katika vikao vya BLM na hatimaye BLW.

Kamati pia, imeelezwa hatua ya Idara ya kuingia mkataba na kampuni ya Microsoft kwa ajili ya kutanua wigo wa huduma zinazotolewa na kupatikana msaada wa kitaalamu wa uendeshaji wa huduma hizo.

Aidha, jumla ya Taasisi 83 za Utumishi wa Umma zimeunganishwa na kituo kikuu cha Kuhifadhia taarifa za Serikali kupitia mkonge wa Taifa pamoja na kutengeneza tovuti ya Serikali na mfumo wa barua pepe ambao utatumika kwa Taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, mafanikio hayo yamepelekea Taasisi hizo kupatiwa huduma za internet bila ya malipo.

CHANGAMOTO ZA IDARA YA SERIKALI MTANDAO

(i) Chanagamoto ya uhaba wa watendaji hususan katika maeneo ya uhakiki wa mifumo *Information System Auditting* pamoja usimamizi na ufuatiliaji wa miradi katika masuala ya TEHAMA *ICT project Management.*

(ii) Pia, uwepo wa uhaba wa wataalamu wa usanifu na ubunifu wa mifumo ya TEHAMA *Information System Development*.

(iii) Uhaba wa fedha, kutokana na bajeti ndogo inayokadiriwa kwa matumizi ya Idara ingawa bajeti hiyo hupatikana kwa wastani wa asilimia 80 lakini bado haitoshelezi kwa mahitaji ya Idara hii.

(iv) Kuwepo kwa tatizo la vyombo vya usafiri, jambo ambalo Idara inashindwa kutekeleza majukumu yake kwa wakati na hivyo kushindwa kuzifikia sehemu za mbali kwa mda muafaka.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(a) Kamati inashauri, kwa kuwa Serikali mtandao inayo fursa kubwa ya kuleta mabadiliko katika utendaji wa kazi Serikalini ili kutoa huduma zilizo bora kwa wananchi. Hivyo, mabadiliko na mafanikio hayo yanaweza kufikiwa baada ya kufanya jitihada kubwa kama vile kupatiwa fedha na wataalamu wa kutosha kwa mujibu wa mahitaji yao.

(b) Aidha, Kamati inashauri Idara ya Serikali Mtandao kuboreshewa maposho yao ya msingi kutokana na kufanya kazi katika mazingira hatari kwa afya ya mwanadamu.

(c) Vile vile, Kamati inashauri watendaji wa Idara hii kupatiwa mafunzoya muda mfupi na yale ya muda mrefu ili kuenda sambamba na madiliko ya teknolojia ulimwenguni.

2.1.8 IDARA YA UTAWALA BORA

Idara ya Utawala Bora katika kutekeleza majukumu yake, imezijengea uwezo Kamati *14* za Ushauri za Shehia ili ziweze kusimamia vyema masuala ya utawala bora katika maeneo yao. Vilevile, vituo *viwili (2)* vya walimu vilipatiwa mafunzo yaliyohusisha ualimu wa somo la uraia kwa

lengo la kuwawezesha kujenga misingi ya Utawala Bora katika skuli za Sekondari.

Idara, pia, imefanya mapitio ya Sera ya Utawala Bora ya mwaka *2011* kwa kuundwa kamati itakayosimamia kazi hiyo. Kamati hiyo imejumuisha watendaji kutoka Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Wizara ya Fedha na Mipango na jumuiya isiyokuwa ya kiserikali ya ANGOZA, Kamati hiyo imeanza kazi ya kukusanya taarifa zitakazotumika katika mapitio ya sera hiyo.

Idara katika kuendelea na jitihada zake za kuelimisha jamii juu ya misingi ya utawala bora, Idara imeandaa kongamano la Kitaifa la Utawala Bora Unguja na Pemba kwa lengo la kuwezesha watendaji kuimarisha misingi ya utawala bora katika sehemu zao za kazi. Makongamano hayo yaliwashirikisha watendaji Wakuu wa Wizara, taasisi za Serikali pamoja na taasisi binafsi. Aidha, Idara imetoa mafunzo kwa Waheshimiwa Madiwani wote wa Unguja na Pemba. Mafunzo hayo yalizungumzia juu ya umuhimu wa Ugatuzi na utawala bora katika kuleta ufanisi na tija ili kuweza kuleta maendeleo endelevu katika taasisi zilizogatuliwa pamoja na taifa kwa jumla.

Kamati kupitia Idara hii imefarijika kwa kitendo cha kuendelea kutoa elimu ya utawala bora kwa njia ya redio na televisheni kwa kurusha hewani vipindi *kumi (10)* vya utawala bora. Kwa upande wa Unguja vipindi hivi vilirushwa na ZBC redio na Pemba vimerushwa na redio jamii Mkoani.

Idara pia imetoa mafunzo ya utawala bora kwa walimu katika vituo vinne vya walimu *(TC)* wanaosomesha somo la uraia. Aidha, Idara imekamilisha rasimu ya awali ya jarida la utawala bora litakalotoka kila mwaka kwa lengo la kutoa elimu juu ya masuala mbalimbali yanayohusu

utawala bora nchini. Vile vile, elimu ya utawala bora imetolewa kwa Kamati *16* za ushauri za Shehia Unguja na Pemba.

2.1.9 OFISI YA AFISA MDHAMINI PEMBA

Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba inajukumu kuu la kusimamia na kuratibu shughuli zote za Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kisiwani Pemba.

Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum inapongeza sana juhudi za Ofisi kuu Pemba kwa kufanikiwa vyema kuratibu kikao cha ukusanyaji maoni ya wadau kuhusu muongozo wa usalama na afya kazini kwa ajili ya kukidhi matakwa ya kifungu cha *77 (1)* cha Sheria ya Utumishi wa Umma, nambari *2* ya mwaka *2011*, kikao ambacho kilihudhuriwa na maafisa utumishi na wataalamu wengine wanaoshughulikia masuala ya afya za watumishi kazini.

Vilevile,Ofisi imeratibu kikao cha kutoa maoni kuhusu marekebisho ya *Sheria ya Mahakama Kuu,nambari 2 ya mwaka 1985* na marekebisho ya *Sheria ya Mahakama za Chini, nambari 6 ya mwaka 1985*, kikao ambacho kilihudhuriwa na watendaji wa Serikali pamoja na Taasisi binafsi, kama vile: Mahakimu, Wanasheria kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Jeshi la Polisi *(Wapelelezi wa Polisi)* pamoja na Mawakili wa kujitegemea.

Ofisi imeratibu kikao cha kutoa maoni kuhusu marekebisho ya *Sheria ya Kamati ya Uongozi ya mwaka 1986*, kikao ambacho kilihudhuriwa na maofisa wadhamini, makatibu tawala wa mikoa na wilaya, Masheha kutoka wilaya zote na maofisa mipango wa Wizara *13* za Pemba.

CHANGAMOTO ZA OFISI YA AFISA MDHAMINI PEMBA

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Ofisi Kuu Pemba inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Uchakavu wa jengo la Ofisi Kuu Pemba, hali ambayo husababisha gharama za mara kwa mara kwa kufanya matengenezo madogo madogo *(minor civil work)* kwa ajili ya kuendelea kulitumia jengo hilo. Hata hivyo, changamoto hii inatarajiwa kumalizika baada ya kukamilika kwa ujenzi wa jengo la Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora huko Gombani, Pemba.

(ii) Uchakavu wa vyombo vya usafiri kwa mfano magari husababisha gharama za mara kwa mara kwa kuzifanyia matengenezo.

(iii) Kesi za udhalilishaji kushindwa kuendelea katika vituo vya Polisi na Mahakamani kwa kukosa ushahidi kutokana na jamii kusuluhishana wenyewe kwa wenyewe na kuomba kuzifuta kesi hizo.

(iv) Tatizo la kufanya kazi kwa mazoea na kuendeleza muhali katika kusimamia haki na uadilifu.

(v) Uhaba wa watendaji katika ofisi ya Tume ya Maadili Pemba.

MAONI NA MAGIZO YA KAMATI

(a) Kamati **inaishauri** Ofisi Kuu Pemba kuhakikisha kuwa inaweka mahitaji yake ya vyombo vya usafiri katika bajeti ya mwaka *2018/2019* ili hali ya kifedha itakapo ruhusu waweze kusaidiwa kupunguza tatizo hili kwa mwaka wa fedha unaokuja.

(b) Kamati inaagiza uongozi wa Ofisi Kuu Pemba kuhakikisha wanasimamia vya kutosha watumishi wote wa Serikali ambao wanakiuka maadili ya utumishi wa Umma.

(c) Kamati inaagiza watendaji wa Taasisi zinazo jikita moja kwa moja na kutatua migogoro ya kijamii kuweza kufuatilia na kuchukua hatua mara tu tatizo linapotokea na waache tabia ya kukalia kiti kusubiri wananchi kuleta matatizo yao.

(d) Kamati inashauri watumishi wa umma maafisa na watendaji wa chini kuacha kufanya kazi kwa mazoea na badala yake watumie ujuzi na taaluma zao ili kuleta mabadiliko katika sekta zao.

(e) Kutokana na changamoto ya watendaji wachache katika ofisi ya Tume ya Maadili Pemba, Kamati inashuri Ofisi kuu Pemba kuwa karibu sana katika

kufuatilia viongozi wote ambao hawakurejesha fomu kwa wakati kuwaelekeza kufuata hatua zinazotakiwa kisheria.

2.1.10 TAASISI ZINAZOJITEGEMEA AMBAZO ZINASIMAMIWA NA WIZARA YA NCHI,OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTWALA BORA

2.1.11 AFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar pamoja na Sheria ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu (Utekelezaji wa Majukumu), nambari 6 ya mwaka *2013*.Afisi ina jukumu la kutoa ushauri juu ya masuala ya sheria kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Aidha, Afisi imetoa ushauri wa Kisheria kwa Serikali na Taasisi zake katika kuthibitisha Miongozo ya Uandaaji wa Mikataba na Uandishi wa Sheria. Miongozo *miwili (2)* imekamilika, ukiwemo Muongozo wa Mikataba na Muongozo wa Uandishi wa Sheria.

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Afisi ya Mwanasheria Mkuu imefuatilia indhari zinazohusiana na kutaka kuishitaki Serikali Unguja na Pemba.

Vilevile, Afisi imeiwakilisha Serikali na taasisi zake katika kesi za madai, imeandaa miswada ya sheria mbalimbali ambayo iliwasilishwa katika Mikutano tofauti ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar na baadhi yake kwa sasa imeshakuwa sheria baada ya kupitishwa na Baraza pamoja na kutiwa saini na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Katika kipindi cha *Oktoba* hadi *Disemba, 2017*, afisi imeshiriki katika mapatano ya utekelezaji na usimamizi wa mikataba ambapo jumla ya Mikataba *90* imesimamiwa, Memorandum of understanding *(MoU)* 18 zimeandaliwa na watumishi *35* wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi.

Pia, katika kipindi hicho, Serikali imewakilishwa Mahakamani katika kesi za madai dhidi yake na jumla ya Indhari *tano (5)* zimefuatiliwa, kesi *80*, zimesimamiwa kati ya hizo, kesi nne zimekamilika. Vile vile, Miswada mitatu, Kanuni *16* na matangazo ya kisheria *22* yameandaliwa. Vikao vya Kamati ya Msamaha wa Rais pamoja na vikao vingine na taasisi za Serikali vimesimamiwa. Aidha, huduma za uendeshaji na utawala zimetolewa.

CHANGAMOTO ZA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

Afisi ya Mwanasheria Mkuu inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Miswada kuchelewa kuletwa kwa wakati kutoka Wizara/Taasisi husika. Hali hii inapelekea Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuchelewa kuiwasilisha miswada hiyo katika Baraza la Wawakilishi na pia kukosa ufanisi.

(ii) Ongezeko kubwa la kesi zinazohusiana na migogoro ya ardhi.

(iii) Kutokuwepo kwa mashirikiano ya kutosha kutoka kwa taasisi zilizokasimiwa mamlaka ya kusimamia kesi kwani baadhi ya wakati hata kesi hizo zinapomalizika hushindwa kutoa taarifa hiyo katika Afsi ya Mwanasheria Mkuu ambayo ndiyo iliyokasimu mamlaka kwao.

(iv) Mashirikiano madogo kutoka katika Wizara/taasisi mbalimbali ambayo hupelekea Afisi ya Mwanasheria Mkuu kushindwa pale kunapokuwa na kesi.

(v) Kukosekana kwa ofisi ya Mwanasheria Mkuu kisiwani Pemba na kupelea wakaazi wa Kisiwa cha Pemba kufuatia huduma za sheria ofisi kuu Unguja.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(a) Kamati **inaishauri,** Serikali kuandaa mpango maalum wa uwasilishaji wa Miswada ya Sheria katika Baraza la Wawakilishi kwa mwaka mzima. Mpango huu:

(i) utaweka utaratibu mzuri wa kuwasilisha miswada Barazani kwa kila mwaka wa fedha;

(ii) utaisaidia Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuandaa na kuwasilisha miswada kwa wakati na yenye ufanisi kwani uzoefu unaonesha kwamba miswada mingi inayowasilishwa Barazani katika kipindi kifupi kilichopita imekuwa na kasoro nyingi za kimantiki na kisarufi;

(iii) utaepusha Tume ya Kurekebisha Sheria kwa kushirikiana na ofisi hii kuzifanyia marekebisho sheria katika kipindi kifupi baada ya kupitishwa na Baraza;

(iv) utaiwezesha Serikali kuepuka gharama nyingi zinazoweza kuepukika ambazo hutumika kuchapishia miswada upya na kwa mara ya pili kabla ya miswada hiyo kujadiliwa na Baraza;

(v) utaepusha kufanya makosa ya kimaudhui/kimantiki ambayo husababisha athari katika utekelezaji wake.

(b) Kamati **inashauri**ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuzingatia kwa ujumla wake masharti ya kanuni ya *79(2)* ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka *2016* ambayo inaeleza:

"Tangazo la kwanza la Mswada wa Serikali litatokea kukiwepo **angalau siku ishirini na moja kabla ya Mswada huo kusomwa kwenye Baraza kwa mara ya kwanza** na litakuwa linaonesha Mswada mzima, pamoja na maelezo yaliyotiwa saini na Waziri yanayotaja madhumuni na sababu za Mswada huo".

Hivyo, kwa mnasaba wa kanuni hiyo ni vyema ukawepo utaratibu utakaoweza kusaidia uandaaji wa miswada ya sheria kwa kutumia mpango maalum wa mwaka mzima utakaozihusisha Wizara au Taasisi zote zenye kuhitaji kufanyiwa marekebisho au kutunga upya sheria zao.

(c) Kamati **inashauri** Serikali kuzitaka Wizara/Taasisi zake kutoa mashirikiano ya karibu kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu hasa wakati Wizara/taasisi hizo zinapokuwa ama zimefungua au zimesfunguliwa kesi Mahakamani kwani uzoefu unaonesha kuwa kesi nyingi Serikali hushindwa katika hatua za awali.

(d) Kamati **inashauri** kwa mara nyengine Serikali kufikiria juu ya umuhimu wa kuwa na ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kisiwani Pemba ili kupunguza

mrundikizo wa kesi Ofisi kuu lakini pia, itawarahisishia wakaazi wa Pemba huduma na kwa wakati mahususi.

(e) Kamati **inashauri** Serikali iiridhie Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kubadilisha muundo wake wa kada za kiutumishi, kutokana na muda wote kutumia muundo wa ***vitengo*** na badala yake kutumia muundo wa ***Idara*** kama ilivyo kwa ofisi nyengine kama hizi kwa Nchi za Jumuiya ya Madola. Muundo huu utasaidia kupunguza changamoto ndogo ndogo zinazojitokeza na hivyo kupelekea ufanisi wa kiutendaji kwawatumishi.

(f) Pamoja na changamoto mbali mbali za Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Kamati imeridhika na inaipongeza sana Afisi hiyo kwa utendaji wake uliobora na kuitaka kuendelea kuwajibika zaidi hasa kwa vile Mwanasheria Mkuu na Naibu wake wamekuwa msaada mkubwa wa Kamati hii.

2.1.12 OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI (CAG)

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) imeanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 112(1) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 pamoja na Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, *Nam. 11 ya mwaka 2003.*

Ofisi hii ina jukumu la kufanya ukaguzi na kuhakikisha kunakuwa na nidhamu katika ukusanyaji wa mapato pamoja na matumizi ya fedha na mali za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Ofisi hii inawajibika/inalazimika kufanya ukaguzi wa hesabu zote za Mawizara, Mashirika na Taasisi za Umma pamoja na Miradi ya Maendeleo na kutoa taarifa zenye kuonyesha namna fedha na mali za Serikali zinavyotumika na hatimae kutoa ushauri na maelekezo kwa Wizara/Taasisi husika.

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imefanya ukaguzi katika Wizara zote *13* na Taasisi zake. Aidha, jumla ya

wakaguzi waandamizi *15* walipatiwa mafunzo maalum ya ukaguzi yakinifu ya komputa *'IFMS'* na mafunzo ya viwango vya uhasibu na ukaguzi vya kimataifa.

OFISI YA MKAGUZI NA MDHIBITI WA HESABU ZA SERIKALI PEMBA

Katika mwaka wa fedha *2017/2018*, Ofisi imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

(i) Kufanya ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha*2016/2017* kwa Wizara/Taasisi zote za Serikali pamoja na Miradi ya Maendeleo.
(ii) Kujenga uwezo wa Ofisi kiutendaji na kielimu.

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Pemba, inaendelea na kazi zake za Ukaguzi wa Mahesabu katika Wizara/Taasisi mbalimbali za Serikali pamoja na kufanya ukaguzi katika miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha *2016/2017*.

Kazi ya ukaguzi wa hesabu ni kazi ambayo inahitaji kutekelezwa na watendaji wenye uwezo wa kielimu, kutokana na hali hiyo Ofisi inaendelea kuwaandaa wafanyakazi wake ili waweze kutekeleza na kusimamia vyema majukumu yao.

Aidha, Ofisi inaendelea kuwapatia wafanyakazi wake mafunzo katika vyuo mbalimbali vilivyopo nchini ili waweze kumudu vyema utekelezaji wa majukumu yao pamoja na kuweza kukabiliana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

CHANGAMOTO ZA OFISI YA *'CAG'*

(i) Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inakabiliwa na uhaba wa watendaji wa fani mbali mbali kama vile *Engineer* wa Ujenzi.
(ii) Mashirikiano madogo kutoka katika Wizara/taasisi mbalimbali.
(iii) Wakuu wa Wizara/taasisi kushindwa kuhudhuria katika mikutano wa kufungua au kufunga ukaguzi katika Taasisi zao. Hali hii hupelekea

kushindwa kujibiwa kwa hoja zinazowasilishwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Taasisi husika.

(iv) Wizara/taasisi kushindwa kujibu hoja kwa wakati (quiry).

(v) Baadhi ya mashirika ya Serikali hushindwa kuwasilisha taarifa za fedha *(financial s*tatement*)* kwa wakati.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(a) Kamati **inashauri** kushughulikiwa kwa haraka suala la uhaba wa watendaji ili shughuli za ukaguzi ziweze kufanyika kwa wakati na kwa ufanisi.

(b) Kamati **inashauri** kuhusiana na ukaguzi wa fedha za Mfuko wa Jimbo kwamba, ukaguzi wake ufanyike kwa haraka mara tu baada ya utekelezaji wa shughuli yenyewe ili kuweza kuona uhalisia wake.

(c) Kamati **inaishauri** Serikali kuzitaka Wizara/taasisi zake kutoa mashirikiano ya karibu na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Mkaguzi.

(d) Kamati **inaishauri** Serikali kuwataka wakuu wa Wizara/taasisi kujibu kwa ufasaha na kwa wakati hoja zinazoibuliwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

2.1.13 MAHAKAMA

Mahakama ni moja kati ya muhimili wa dola ambao unajumuisha:

(a) Mahakama ya Mwanzo.
(b) Mahakama ya Wilaya.
(c) Mahakama ya Kadhi wa Wilaya.
(d) Mahakama ya Kadhi wa Rufaa.
(e) Mahakamaya Mkoa.
(f) Mahakama Kuu.

Vilevile, kuna jumla ya vitengo vya Mahakama Kuu *vitatu (3)* hadi sasa ambavyo ni:

(i) Mahakama ya Kazi.
(ii) Mahakama ya Biashara.
(iii) Mahakama ya Watoto.

Mahakama ina majukumu makuu ya kuitafsiri sheria, kusikiliza kesi na kutoa maamuzi kwa mujibu wa sheria za nchi. Katika kusikiliza na kutoa maamuzi ya kesi, Mahakama ina jukumu la kusikiliza na kutoa uamuzi kwa kesi zote zinazohusiana na madai na jinai.

Mahakama iliwapatia mafunzo ya kiutendaji Majaji *wanne (4)* na Mahakimu *sita (6)* ambao walishiriki katika Mkutano wa Jumuiya ya Madola uliofanyika nchini Namibia. Vilevile, Mheshimiwa Jaji *mmoja (1)* na Mahakimu *wawili (2)* wameshiriki mkutano wa kimataifa wa Majaji nchini India. Mahakimu walishiriki mkutano wa Jumuiya ya Majaji na Mahakimu wa Afrika Mashariki uliofanyika nchini Rwanda kwa lengo la kubadilishana mawazo na Mahakimu wenzao wa nchi nyengine.

Katika kuhakikisha kuwa miundombinu ya Mahakama inaimarika, matayarisho ya ujenzi wa jengo jipya la Mahakama Kuu huko Tunguu umeanza kwa mashirikiano na Wakala wa Majengo Zanzibar.

2.1.13.1 UJENZI WA MAHAKAMA KUU, TUNGUU

Matayarisho ya ujenzi wa jengo jipya la Mahakama Kuu Tunguu yameanza na Mshauri elekezi wa ujenzi huo tayari ameshapatikana. Kamati ilipata fursa ya kutembelea eneo hilo la MahakamaTunguu.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(i) Kamati **inaiagiza** Mahakama Kuu kuhakikisha kwamba inatenga fedha katika bajeti yake ya kila mwaka ili kuharakisha ujenzi huo.

(ii) Kamati **inaishauri** Mahakama Kuu kujenga jengo ambalo litazingatia ubora wa viwango ili liweze kudumu kwa muda mrefu na vilevile, jengo hilo liwe na nafasi ya kutosha kwa ajili ya kuweza kutumiwa na wale wote wanaohusika.

2.1.13.2 MAHAKAMA KUU PEMBA

Mahakama Kuu Pemba inajumuisha Vituo *vitano (5)* vya kazi ambavyo ni Chake Chake, Wete, Konde, Mkoani na Kengeja pamoja na Mahakama za Baraza la Mji za Chake Chake, Wete na Micheweni. Aidha, Mahakama za Ardhi zilizopo katika Mikoa *miwili (2)* ya Pemba *(Kaskazini na Kusini)*.

Vituo vyote hivyo vinaongozwa na Mrajis wa Jimbo ambaye pia anafanya kazi za kiutawala katika Mahakama Kuu kwa upande wa Pemba pamoja na kutoa maamuzi ya mashauri mbalimbali ya Jinai na Madai.

Mahakama Kuu Pemba inajumla ya wafanyakazi *125* kati ya hao wanaume ni *83* na wanawake ni *42*,idadi hii inajumuisha wafanyakazi wa kada mbalimbali ikiwemo kada ya Mahakimu *(23)* na Makadhi*(5)*.

Malengo makuu ya Mahakama hii ni kutoa haki kwa mujibu wa Sheria za Nchi na taratibu zilizowekwa katika Mashauri ya Jinai na Madai yanayofunguliwa huko Pemba. Mashauri ya Madai yapo yale ya kawaida na ya Mahakama za Kadhi yanayohusu Ndoa, Talaka, Mirathi, Matunzo ya Watoto, Wakfu na Hiba kwa wahusika watakuwa Waislamu.

Kwa upande wa Mahakama Kuu, Majaji wameendelea kusikiliza kesi mbali mbali hapa Pemba, kwa kipindi cha *Octoba* hadi *Disemba, 2017* jumla ya Majaji *wanne (4)* walifika Pemba katika vipindi tofauti kwa ajili ya kusikiliza mashauri yaliyofunguliwa katika Mahakama Kuu Pemba.

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI MAHKAMA PEMBA

Mahakama Kuu Pemba inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Baadhi ya Majengo ya Mahakama bado ni chakavu yanahitaji matengenezo makubwa.
(ii) Upungufu wa wafanyakazi bado ni tatizo kwa baadhi ya maeneo kama sehemu ya Manunuzi, sehemu ya Mtunza ghala na wapiga chapa.
(iii) Ufinyu wa Bajeti unaopelekea Mahakama kutofikia malengo yake iliyojipangia.
(iv) Uhaba wa vyombo vya usafiri.
(v) Kushindwa kwa kuendelea kwa baadhi ya kesi za udhalilishaji kutokana na mashahidi kukataa kutoa ushahidi wanapoitwa Makamani.

Mahakama Kuu Pemba mbali na changamaoto inazokabiliana nazo, imeweza kutekeleza yafuatayo:

(a) Kuondoa mrundikano mkubwa wa kesi zinazosubiri Maamuzi.
(b) Kuondoa mrundikano wa madeni ya mashahidi.
(c) Kupunguza idadi kubwa ya madeni kwa wafanyakazi katika kada mbali mbali.
(d) Ununuzi wa vifaa vya stationary na vifaa vya magari*(mipira)*.
(e) Ununuzi wa vifaa vya Ofisi yakiwemo makabati ya kuhifadhia Majalada.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(i) Kamati inaiagiza Mahakama kutafuta njia mbadala itakayosaidia kuendelea kwa kesi wakati mashahidi *namba moja* (01) wanapokataa kutoa ushahidi.

(ii) Kamati inaishauri Mahakama katika Bajeti yao mwaka 2018/2019 kuweka mpango utakaosaidia kuzifanyia matengenezo ofisi zake pamoja ununuzi wa vyombo vya usafiri.

(iii) Kamati inaigiza Mahakama kutoridhika na tabia za wanajamii Pemba kufuta kesi kiholela kutokana na kuoneana muhali katika kesi za udhalilishaji.

Vilevile, Kamati inapongeza Mahakama Kuu Pemba pamoja na Changamoto mbalimbali zinazozikabili watendaji wake bado wanatoa ushirikiano wa kutosha na Taasisi nyengine za Sheria ili kuhakikisha kwamba Mahakama inafikia kwa kiasi kikubwa malengo yake iliyojipangia.

2.1.13.3 MATENGENEZO YA MAHAKAMA YA WILAYA MWANAKWEREKWE

Kamati imetembelea na kuona hatua iliyofikia ya ujenzi wa Mahakama ya Wilaya Mwanakwerekwe. Jengo la Mahakama ya Wilaya Mwanakwerekwe ambalo linaendelea kufanyiwa matengenezo makubwa lipo katika hali ya kuridhisha, hali ambayo itapelekea kuongeza ufanisi katika usikilizaji wa kesi. Ifahamike kwamba Mahakama hiyo inatoa huduma zake kwa Wilaya *tatu (3)* zifuatazo:

(i) Wilaya ya Mjini.
(ii) Wilaya ya Magharib *'A'*.
(iii) Wilaya ya Magharib *'B'*.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(a) Kamati imeridhishwa na hatua za ujenzi zilizofikiwa pamoja na mazingira mazuri.

(b) Mahakama inaagizwa kuhakikisha kuwa ujenzi huo unakamilika kwa wakati uliopangwa ili huduma zilizokuwa zikitolewa na Mahakama hiyo ziweze kuendelea.

(c) Kamati inaagiza Mahakama kuangalia uwezekano wa kupata fedha kwa ajili ya kuweka vipoza hewa *(AC)* katika jengo hilo.

(d) Kamati inaagiza uongozi wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuzungumza na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira juu ya vibanda *viwili (2)* vilivyo pembezoni mwa jengo hilo kujumuishwa miongoni mwa maeneo ya Mahakama hiyo.

2.1.13.4 MAHAKAMA YA WILAYA YA MKOKOTONI

Kamati ilitembelea katika Mahakama ya Wilaya ya Mkokotoni ni miongoni mwa Mahakama zilizo chini ya Mahakama Kuu Zanzibar ambayo ipo katika kijiji cha Mkokotoni. Mahakama hii inajumuisha Mahakama ya Wilaya, Mahakama ya Kadhi wa Wilaya na Mahakama ya Mwanzo.

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Mahakama hii inapokea kesi mbalimbali zinazohusiana na udhalilishaji, makosa ya usalama barabarani, ndoa na talaka, wizi wa mazao pamoja na kesi za madai.

Mahakama hii imefanikiwa makubwa kiutendaji kwa kusikiliza kesi na kuzitolea uamuzi wa haraka hadi kufikia asilimia *50*. Hata hivyo, Mahakama hii inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(a) Ukongwe na ubovu wa jengo pamoja na uhaba wa vyumba vya ofisi kutokana na kuwa jengo hilo linatumiwa na taasisi nyengine *mbili (2)* za Serikali *(Shirika la Bandari na Shirika la Umeme)*;

(b) Ukosefu wa chumba/ghala cha kuhifadhia mafaili yanayotumika na yaliyofungwa;

(c) Uhaba wa vitendea kazi na vifaa mbalimbali kama vile gari, viti, meza, makabati n.k.;

(d) Kuchelewa kukamilika kwa ushahidi ambako hupelekea kufutwa kwa kesi;
(e) Kukimbia kwa watuhumiwa kwenye kesi zao kunakosababishwa na kuchelewa kukamilika kwa ushahidi;
(f) Kuomba kuakhirishwa kwa kesi za udhalilishaji mara kwa mara.
(g) Hali mbaya ya jengo kutokana na uchakavu na mazingira hatarishi ya nje ya jengo kwa usalama wa afya za watendaji na watumiaji wa Mahakama hii.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

Kamati inatoa maoni na maagizo yafuatayo kwa Mahakama hii:

(a) Mahakama**inaagizwa** kuandaa utaratibu maalum wa kuukata mti ambao huwa unaota juu ya jengo hilo katika upande wa nyumana kuhakikisha kuwa hauoti tena, uwepo mti wa huo kuhatarisha uhai wa jengo hilo pamoja na watumiaji wake.
(b) Mahakama**inashauriwa** kuhakikisha kuwa inahifadhi mazingira ya jengo hilo ambapo iliwataka wafanyakazi kuyathamini maeneo wanayofanyia kazi.
(c) Mahakama**inaagizwa** kuandaa utaratibu mzuriutakaosaidia kuondoa kabisa tatizo la makabati ya kuhifadhia majadala na mafaili mengineyo ambayo yalikuwa tayari yameshaharibika kwa kuliwa na mchwa.Kumbukumbu na taarifa hizo muhimu za wananchi zinahitaji kutunzwa ipasavyo ili kuepusha kupotea au kuharibika.
(d) Kuhusiana na kesi za udhalilishaji, Kamati **imelishauri** jeshi la Polisi kutoa mashirikiano na kuhakikisha kuwa kesi za udhalilishaji hazimaliziki katika kituo cha Polisi na badala yake ziwasilishwe Mahakamani ili haki ipatikane kwa wanaohusika.

2.1.13.5 MAHAKAMA YA WILAYA YA KONDE

Kamati ilitembea katika maeneo mbalimbali yaMahakama ya Wilaya ya Konde na kutoa shukurani zake za dhati kwa Mahakama hiyo kwa kuweza kupata Hatimiliki ya eneo la Mahakama.

CHANGAMOTO ZA MAHAKAMA YA KONDE

Mahakama hiyo inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(a) Ubovu wa paa la mbele ya jengo la Mahakamahiyo na linahatarisha maisha ya watendaji na watu wengine wanaoitumia Mahakama hii.
(b) Pia, Mahakama inakabiliwa na upungufu wa vitendea kazi ambapoMahakama nzima ina *'computer'moja(1)* tu inayotumika kwa shughuli zote za Mahakama pamoja na uhaba wa mabenchi ya wasikilizaji kesi.
(c) Ukosefu wa vyoo ambapokipo choo *kimoja(1)*tu ambacho kinatumiwa ni Hakimu, watendaji, mahabusu na wasikilizaji kesi na wakati mwengine hutumiwa hata ni wananchi wapita njia.
(d) Kamati ilisikitishwa sana na kuwepo kwa mazingira machafu ya choo kinachotumika kwani tatizo la uchafu ndio lilipelekea vyoo viwili (2) vya Ofisi ya *'DPP'* kutotumika na hivyo kutumia choo kimoja cha Mahakama.
(e) Uhaba wa makabati ya kuhifadhia majalada kunakopelekea majalada ya kesi kutapakaa kila sehemu.
(f) Uhaba na uchakavu wa samani katika vyumba vya ofisi na ukumbi wa kusikilizia kesi.
(g) Changamoto ya fedha ya kuwalipa mashahidi wakati wanapoitwa kwa kutoa ushahidi.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

Kamati ilitoa maoni na maagizo yafuatayo kwa Mahakama ya Konde:

(i) Kamati **inaiishauri** Serikali kupitia Mahakama Kuu kusaidia nguvu kwa kujenga uzio katika eneo lote la Mahakama ili kuepusha kuvamiwa na wananchi.

(ii) Kamati **imeiagiza** Mahakama kuhakikisha kuwa, katika kipindi hiki wanajenga choo chengine au kuvifanyia matengenezo vyoo ambavyo havitumiki ili kuweza kutumiwa na Hakimu wa Mahakama hii.

(iii) Kamati **inaishauri** Mahakama ya Kadhi Konde kupatiwa vitendea kazi ili kuboreshwa mazingira yake kiutendaji.

(iv) Kamati inashauri Mahakama hii kupatiwa vifaa vitakavyo saidia kuhifadhia majalada na vile vile kupatiwa samani kwa ajili ya ofisi za watendaji.

2.1.14 OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ni miongoni mwa Taasisi muhimu Serikalini ambayo ina jukumu la kusimamia maswala yote yanayohusiana na kesi za jinai.

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka katika utekelezaji wa majukumu yake, imeendelea kusimamia kesi katika Mahakama mbalimbali nchini ikiwemo kutolewa maamuzi kwa majalada mbalimbali yenye kesi tofauti pamoja na kuchapisha ripoti za kisheria.

Aidha, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imeratibu ufanyikaji wa vikao tofauti kuhusiana na uimarishaji wa uendeshaji wa kesi za udhalilishaji wa wanawake na watoto na madawa ya kulevya. Vikao hivi vina lengo kuu la kutafuta mbinu za kupambana na vitendo hivyo. Pia, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imelazimika kuchukua jitihada hizi kutokana na ongezeko kubwa la vitendo hivyo nchini.

Vilevile, Ofisi katika kipindi cha *Oktoba – Disemba 2017*, katika jukumu lake la msingi la kusimamia kesi, imepokea jumla ya kesi*2,750*, ambapo imetoa maamuzi kwa majalada *500* na imechapisha ripoti ya Kesi za Udhalilishaji na ripoti ya Kesi za Dawa za Kulevya.

Katika kuimarisha uendeshaji wa kesi za udhalilishaji na dawa za kulevya, jumla ya vikao *vitatu (3)* vya uratibu vilifanyika kujadili mbinu za kupambana na kesi hizo.

Ofisi pia, imefanyia mafunzo Waendesha Mashtaka na Wapelelezi *14* kuhusiana na namna ya ujazaji na usomaji wa ripoti za madaktari na kesi za udhalilishaji pamoja na kesi zinazohusiana na vifo mbalimbali.

Licha ya mafanikio makubwa ambayo ofisi hii imefikia lakini bado inakabiliwa na **changamoto** mbali mbali, kama vile:

(a) Uhaba wa vyombi vya usafiri,
(b) Kutoingizwa fedha za matumizi kwa wakati,
(c) Kushindwa kuendelea kwa kesi kutokana na Mashahidi kushindwa kutoa mashirikiano kikamilifu, na
(d) Kuongezeka kwa wimbi la kesi za udhalilishaji siku hadi siku.

OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA PEMBA

Kwa upande wa **Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba** ina jukumu kubwa la kusimamia haki ya jinai kwa kuratibu shughuli za uendeshaji wa Mashtaka ya jinai kisiwani Pemba. Katika kutekeleza jukumu lake hilo, Ofisi hupokea na kufanyia kazi majalada ya uchunguuzi wa kesi za jinai kutoka vituo *11* vya Polisi na kutoka Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar kwa upande wa Pemba.

Ofisi inaendesha mashtaka ya jinai katika Mahakama Kuu ya Zanzibar kwa upande wa Pemba, Mahakama za Mikoa ya Kusini na Kaskazini Pemba na Mahakama za Wilaya *nne (4)* za Pemba. Pia, imetoa elimu kwa umma kuhusu haki ya jinai kwa ujumla.

Hali ya Kesi za Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto

Katika kipindi cha *Oktoba – Disemba 2017*, jumla ya majalada *59* yanayohusu kesi za udhalilishaji yamepokelewa, kati ya hayo majalada*nane(8)* kutoka Wilaya ya Mkoani, *24* Wilaya ya Chake Chake, *17* Wilaya ya Wete na*kumi(10)* Wilaya ya Micheweni.

Makosa yanayohusika katika majalada hayo ni kubaka *(29)*, kutorosha wasichana *(12)*, kulawiti*tisa (9),* shambulio la aibu*sita (6)* na majalada*matatu(3)* yanahusiana na udhalilishaji/unyanyasaji wa kijinsia.

Katika majalada *59* yaliyopokelewa, majalada *53*yalipata ruhusa ya kufunguliwa Mahakamani, majalada*sita(6)* ambayo hayakupata ruhusa, manne(4) yalirejeshwa kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho na *miwili (2)*yalielekezwa kufungwa kwa sababu ushahidi wake ulikuwa dhaifu sana. Majalada yaliyotakiwa kupelekwa mahakamani tayari yameshapelekwa kwa kiasi kikubwa na yanaendelea katika hatua mbalimbali, na kesi *mbili (2)* zimeshamalizika na mshitakiwa *mmoja (1)* alihukumiwa kwenda Chuo cha Mafunzo kwa muda wa miaka *mitano (5)* pamoja na kulipa faini na fidia na kesi nyengine mshitakiwa ametakiwa kulipa fidia.

Kwa ujumla, kesi za udhalilishaji wa wanawake na watoto zilizotolewa hukumu katika kipindi hiki ambazo hazikufunguliwa kipindi hicho ni *nane (8)*. Kati ya hizo, kesi*sita(6)* washitakiwa walipatikana na hatia na kesi*mbili(2)* hawakupatikana na hatia. Kwa zile walizopatikana na hatia, washitakiwa walipewa adhabu ya kwenda Chuo cha Mafunzo kwa kipindi cha miaka *minne minne (4)* na kulipa fidia *{kesi tatu(3)*, fidia kesi mbili (2)} na faini na fidia *{kesi moja (1)}*.

Katika kipindi cha *Oktoba – Disemba, 2017*, kumetokea matukio *saba (7)* mabaya zaidi ya udhalilishaji katika Mikoa yote *miwili (2)* ya Pemba kama ifuatavyo:

(a) Tukio la ng'ombe Ole.
(b) Tukio la Mshindo.
(c) Tukio la mganga wa kienyeji Mgogoni.

(d) Tukio la baba wa kambo Kiungoni.
(e) Tukio la afisa ustawi mstaafu.
(f) Tukio la mzee mlemavu Wete.
(g) Tukio la mzee wa miaka 70 Kiuyu.

Majalada ya matukio yote hayo yalifikishwa katika Ofisi ya DPP na kesi zote zimeshafunguliwa mahakamani.

Hali ya Kesi za Madawa ya Kulevya

Katika kipindi cha *Oktoba – Disemba, 2017*, jumla ya majalada *34* yanayohusiana na kesi za madawa ya kulevya yamepokelewa, kati ya majalada hayo, majalada *matano (5)* kutoka Wilaya ya Mkoani, majalada *12* kutoka Wilaya ya Chake Chake, majalada *15* kutoka Wilaya ya Wete na majalada *mawili (2)* kutoka Wilaya ya Micheweni.

Katika majalada yote *34* yaliyopokelewa, majalada *32* yalipata ruhusa ya kwenda mahakamani na majalada *mawili (2)* yalirejeshwa kwa kufanyiwa marekebisho. Katika majalada 34, majalada 19 yanahusiana na *'bhang'*, majalada 14 *'heroin'* na jalada *moja (1)'Cocaine'*.

Kwa upande wa majalada ambayo yalipata ruhusa ya kwenda mahakamani, kesi zimeshaanza kusikilizwa ingawa bado hakuna iliyomalizika. Katika kipindi husika, zipo hukumu *tano (5)* ambazo zilitoka kwa kesi ambazo zilifunguliwa kabla ya mwezi *Oktoba, 2017*. Katika hukumu hizo, zote washitakiwa walipatikana na hatia na kupewa adhabu ya kutumikia Chuo cha Mafunzo kati ya miaka *mitatu (3)* na *15* au kulipa faini kati ya Shilingi za Kitanzania milioni tano (5) na milioni 40.

Aidha, kipindi hicho kulijitokeza matukio *manne (4)* makubwa kuhusiana na kesi za madawa ya kulevya kwa upande wa Pemba ukilinganisha na hali ilivyozoeleka kama ifuatavyo:

(i) Tukio la mama aliyekamatwa na kete *3,621(Heroin)*.

(ii) Kesi ya *'DVD'* (kete *962 'Heroin'*)
(iii) Kesi ya Pemba 'bag' (misokoto ya 'bhang'*2,240*).
(iv) Kesi ya Jahazi (kete *560 'Heroin'*).

Matukio hayo yameshariporiwa Mahakamani na kesi zipo katika hatua ya kusikilizwa.

Hali ka Kesi za Rushwa na Uhujumu Uchumi

Katika kipindi cha *Oktoba – Disemba, 2017*, jumla ya kesi *nne (4)* zinazohusu rushwa na uhujumu wa uchumi zimepokelewa katika Ofisi hii kisiwani Pemba. Kesi hizo zinahusu zaidi makosa ya rushwa na matumizi mabaya ya Ofisi.

Kesi zinazohusiana na Karafuu

Katika kipindi cha *Oktoba – Disemba, 2017*ulikuwa ni msimu wa uvunaji wa zao la karafuu. Kwa hivyo, jumla ya kesi *42* zinazohusiana na karafuu zilipokelewa katika Ofisi ya DPP. Kati ya hizo, kesi *33* zinahusiana na wizi wa karafuu mashambani, kesi*tatu(3)* zinahusiana na kusafirisha karafuu bila kibali, kesi*mbili(2)*zinahusiana na kununua karafuu bila ya kibali, kesi*moja(1)*inahusiana na kuhifadhi karafuu bila ya kibali, kesi *moja (1)* inahusiana na uharibifu wa mikarafuu na kesi *mbili (2)* zinahusiana na kusafirsha karafuu kwa njia ya magendo.

Katika kesi hizo, jumla ya kesi *29*zilipata ruhusa ya kufunguliwa Mahakamani na kesi *13* hazikupata ruhusa. Kesi *29* zilizopata ruhusa ya kufunguliwa Mahakamani, kesi *25* tayari zimeshafunguliwa Mahakamani ambapo kesi *17* zimeshamalizika na zote washitakiwa wamepatikana na hatia na kutozwa faini kama sheria inayohusiana na zao la karafuu inavyoelekeza.
Aidha, zipo kesi nyengine *mbili (2)* ambazo zinahusiana na kusafirisha karafuu bila ya kibali zilitolewa hukumu katika kipindi husika ingawa zilifunguliwa kabla ya kipindi hicho. Katika kesi hizo *moja (1)* ilipatikana na hatia na mshitakiwa alitozwa faini ya shilingi za Kitanzania milioni *moja (1)* na nyengine mshitakiwa hakupatikana na hatia.

Kesi Zinazohusiana na Watoto ambao ni Watuhumiwa/Washtakiwa

Katika kipindi cha *Oktoba – Disemba, 2017*, watoto mbali mbali wametuhumiwa kuhusika katika vitendo vya udhalilishaji dhidi ya watoto wenzao pamoja na kutuhumiwa kushiriki katika vitendo vyengine vya kihalifu. Jumla ya majalada *16* miongoni mwa majalada yaliyowasilishwa katika Ofisi ya DPP yanahusiana na kesi za watoto ambapo kesi *15* zinahusiana na udhalilishaji wa watoto wenzao ambapo *13* zimepata ruhusa ya kwenda Mahakamani na*moja (1)* inahusiana na wizi ambayo pia imepata ruhusa ya kwenda mahakamani. Kesi zote zimeshafunguliwa Mahakamani na zipo katika hatua ya kusikilizwa.

CHANGAMOTO ZA OFISI YA DPP PEMBA

Katika utekelezaji wa kazi zake, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba inakabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwa ni pamoja na:

(i) Mashahidi muhimu (kama vile watoto walioathiriwa) katika kesi za udhalilishaji wanaendelea kukataa kutoa ushahidi mahakamani.
(ii) Uhaba wa wakemia wa Serikali unasababisha usumbufu katika uharakishaji wa usikilizaji wa kesi zinazohusu madawa ya kulevya.
(iii) Upungufu wa vyombo vya usafiri katika usimamizi wa shughuli za uendeshaji wa mashtaka.
(iv) Kucherewa kuripotiwa kwa matukio ya jinai hasa katika kesi za udhalilishaji.
(v) Uingizaji hafifu wa fedha za matumizi mengineyo ambao umesababisha kukwama kwa shughuli nyingi sana za uendeshaji wa Ofisi.
(vi) Uhaba wa ofisi zenye kukidhi mahitaji kwa watendaji.

Licha ya changamoto zote hizo, Ofisi inaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa jitihada kubwa na mafanikio yanapatikana.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(a) Kamati **imeiagiza** Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka itafute njia nyengine itakayowezesha kuendelea na kesi hususani za udhalilishaji bila ya kutegemea ushahidi wa mashahidi muhimu ambao wanakataa kutoa ushahidi wao.

(b) Kamati **inashauri** kuchukuliwa jitihada za ziada zinazohitajika kwa kushirikiana na Wizara husika kuajiri wakemia ili kuondoa kasoro iliopo.

(c) Kamati inashauri ofisi ya DPP kuomba fungu maalum katika bajeti inayokuja kwa lengo kutafuta usafiri ili kupunguza tatizo hilo.

(d) Kamati inshauri Idara hii kupatiwa fedha za matumizi mengineyo kama ilivyoomba na kwa wakati mahususi ili kukabiliana na changamoto mbali mbali zinazowakabili.

(e) Aidha, Kamati inampongeza Mwendesha Mashtaka pamoja na wafanyakazi wake kwa juhudi zao za utekelzaji wa majukumu yao ya kila siku.

2.1.15 OFISI YA MUFTI

Ofisi ya Mufti Zanzibar imeanzishwa chini ya *Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mufti*, nambari *9* ya mwaka *2001*, ofisi ya hii ina jukumu la usimamizi na uratibu wa masuala mbalimbali ya dini ya Kiislamu yanayohusiana na utatuzi wa migogoro katika familia, masuala ya ndoa na talaka, kutoa fatwa katika misingi ya Kiislamu, usajili wa vyuo vya Quran na Misikiti, kufanya ziara za kutembelea Misikiti na vyuo vya Quran, kukutana na viongozi mbalimbali wa kijamii pamoja na Taasisi nyengine za Kiislamu nje ya Nchi.

Ofisi ya Mufti imetekeleza shughuli za kusajili Misikiti na Madrasa Unguja na Pemba. Pia, Ofisi imetembelea Misikiti na madrasa kwa lengo la kutoa nasaha na kukumbushana juu ya kufuata maadili ya Kiislamu. Ofisi ilipokea migogoro ikiwemo migogoro ya ndoa ambapo baadhi yake imetatuliwa na mengine imepelekwa mahakamani wakati mengine bado inaendelea kutafutiwa ufumbuzi.

Katika kipindi cha *Oktoba – Disemba 2017*, vipindi vya masuala na majibu vinaendelea kutolewa ambapo jumla ya masuala *48* yamejibiwa pamoja na kurusha hewani vipindi vya nasaha na mawaidha ya dini

kupitia ZBC Redio. Vipindi hivyo vinahusu masuala ya ndoa, mshikamano wa wanadini na sherehe za watoto *(hakika)*.

Ofisi ya Mufti katika kutekeleza majukumu yake, ilifanya mikutano mbalimbali kwa viongozi wa dini yenye lengo la kusisitiza amani na utulivu na kupinga udhalilishaji wa wanawake na watoto Unguja na Pemba.
Vilevile, katika kuimarisha mahusiano mema ya kidini na Taasisi nyengine, Mufti na Katibu wake walihudhuria Kongamano la kidini la Afrika Mashariki na Kati lililoandaliwa na Jumuiya ya '*Islamic Foundation*' kwa lengo la kukuza mahusiano na viongozi wa dini wa kanda hii.

Aidha, **Ofisi ya Mufti Pemba** imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya usimamizi na uratibu wa masuala mbalimbali ya dini ya kiislamu yanayohusiana na utatuzi wa migogoro ya kifamiliya, migogoro ya ndoa na talaka, fatwa katika misingi ya dini yaKiislamu, usajili wa vyuo vya Quran, usajili wa Misikiti pamoja na kutembela Misikiti na vyuo vya quran.

CHANGAMOTO ZA OFISI YA MUFTI

(a) Ukosefu wa vyombo vya usafiri ambapo hupeleka kushindwa kutekeleza majukumu yao vijijini.
(b) Ukosefu wa jenereta kwa ajili kukabiliana na changamoto ya umeme.
(c) Uhaba wa fedha za matumizi kutokana na kupata Ruzuku kutoka Wizarani.
(d) Kushamiri kwa migogoro mbali mbali ya kindoa na Misikiti.
(e) Utendaji usioridhisha kwa Maafisa wa Afisi hiyo kwa upande wa Pemba kusababisha migogoro isiyokwisha baina ya Waumini wa Dini ya Kiislamu.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(i) Kufuatia uwepo wa migogoro inayohusiana na masuala ya dini ya Kiislamu kama vile misikitini, Kamati inashauri Ofisi ya Mufti Pemba kutokukaa Ofisini na kusubiri migogoro hiyo iwasilishwe juu ya meza badala yake wafuatilie Mitaani ili waweze kuibaini migogoro hiyo katika jamii, kwani ni idadi ndogo ya wananchi wanaofahamu majukumu na taratibu za Ofisi hii.

(ii) Kamati inashauri Ofisi hii kupatiwa vyombo vya usafiri angalu vespa kwa waale maafisa wanaofuatilia migogorokatika jamii.

(iii) Kamati inashauri ofisi ya Mufti kupatiwa fungu lake la bajeti ili kuwasaidia kutatua changamoto mbali mbali zinazowakabili.

(iv) Kamati inashauri Afisi hii kupatiwa jenereta kwa ajili ya kukabiliana na tatizo la umeme wakati unapokatika.

(v) Kamati inashuri Afisi ya Mufti Zanzibar kufuatilia utendaji wa Afisi hii huko Pemba na kuhakikisha wameboresha utendaji wao katika majukumu yao ya kila siku.

2.1.16 TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni Taasisi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyoanzishwa kwa mujibu wa *Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, nambari 4 ya mwaka 2015*. Kwa mujibu wa sheria, Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ina mamlaka ya kusimamia maadili ya viongozi wa umma ikiwemo kupokea, kusajili na kuhakiki tamko la mali na madeni kutoka kwa viongozi wa umma; kufanya uchunguzi kuhusu uvunjwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma pamoja na kutoa elimu kwa umma na viongozi kuhusiana na umuhimu wa kuimarisha maadili nchini.

Tume katika kutekeleza jukumu lake la msingi la kupokea na kuhifadhi tamko la mali na madeni kwa viongozi wa umma, Tume imetoa fomu kwa viongozi wote ambao kwa mujibu wa Sheria *Nambari 4 ya mwaka 2015* wanaopaswa kujaza fomu za tamko la mali na madeni. Fomu hizo ziliweza kupatikana katika Ofisi za Tume Unguja na Pemba na kwenye mtandao wa Tume ya Maadili.

Hadi kufikia tarehe *31 disemba 2017*,Tume ilikwishapokea jumla ya fomu *1575*za Viongozi. Hata hivyo, Tume inaendelea na zoezi la kupokea fomu za Viongozi walioshindwa kuziwasilisha kwa wakati na waliopata uteuzi mpya. Vilevile, Tume inaendelea kuzipitia fomu na hatimaye kuandaa orodha ya majina ya Viongozi wote wa Umma waliowasilisha fomu zao kwa ajili ya kuchapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma katika kutekeleza majukumu yake ndani ya kipindi hiki, ilisajili taarifa za mali na madeni ya viongozi wa umma. Pia, Tume ilifanya uhakiki wa taarifa za mali na madeni kwa viongozi wa umma na kushughulikia malalamiko mbalimbali juu ya uchunguzi wa tuhuma za ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Aidha, katika kuhakikisha kazi ya uhakiki inafanyika kwa ufanisi, vifaa vikiwemo *'GPS'*, *'Tapes'* na Kamera vimenunuliwa. Pia, maandalizi ya ununuzi wa gari itakayotumika katika shughuli za uhakiki na Ofisi kwa ujumla yanaendelea.

Vilevile, katika kuhakikisha kuwa viongozi na wananchi wanapata uelewa juu ya umuhimu wa jamii yenye maadili nchini, Tume iliandaa vipindi vya Televisheni na redio ambavyo vilirushwa hewani katika nyakati tofauti. Mbali ya kurushwa hewani kwa vipindi hivyo, pia, Tume iliandaa semina kuhusu umuhimu wa maadili ambazo zilitolewa kwa maafisa wa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU), Maskuli na Kamati za Masheha. Mafunzo ya kitaalamu kuhusu maadili ya viongozi wa umma yalitolewa kwa watumishi wa Tume.

Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Pemba, katika kipindi cha Octoba – Disemba, 2017, imetoa mafunzo kwa kamati za Masheha, wanajamii kupitia vyombo vya habari na wanafunzi mashuleni. Lengo

kuu la mafunzo ni kukuza uelewa kwa jamii juu ya umuhimu wa kuimarisha maadili katika jamii pamoja na kuwataka washirikiane na Tume, ili Tume iweze itekeleze majukumu yake ipasavyo.

Aidha, Tume imetoa mafunzo kuhusiana na ujazaji fomu za tamko la rasilimali na madeni na uhakiki kwa viongozi wa ngazi zote ambao wanawajibika kujaza fomu hizo kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya mwaka 2015.

CHANGAMOTO ZA TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Pemba inakabiliwa changamoto na zifuatazo:

(i) Ufinyu wa Ofisi, kutokana na Tume kupatiwa chumba kimoja tu ndani ya Ofisi ya Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
(ii) Uhaba wa vitendea kazi kama vile vyombo vya usafiri pamoja na rasilimali watu.
(iii) Kuchelewa kwa baadhi ya viongozi katika utrejeshaji wa fomu wengi wao wakiwa ni Wahasibu na watu wengine wenye dhamana ya fedha.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

Katika kutatua changamoto hizo, Kamati inashauri na kuaagiza mambo yafuatayo:

(a) Kuchukuliwa hatua za haraka viongozi wote wanaochelewesha kurejesha fomu kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Maadili, Sheria namba 4 ya mwaka 2015.
(b) Baada kukamilika kwa ofisi mpya za Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Tume ya Maadili wapatiwe ofisi yao ya kudumu ambayo itakidhi mahitaji yao katika ofisi hiyo mpya.
(c) Srikali ifanye utaratibu wa kuwapatia vyombo vya usafiri na vifaa vyengine vyenye kuhitajika katika majukumu yao ya kila siku.

2.1.17 KAMISHENI YA UTUMISHI SERIKALINI

Kamisheni ya Utumishi wa Umma imeundwa chini ya *Katiba ya Zanzibar* ya mwaka *1984* kuwa ni chombo cha juu kabisa kwa Tume zote za Utumishi. Kamisheni ina mamlaka ya kusimaia na kuratibu mambo yote ya utumishi kwa Zanzibar.

Kamisheni imeridhia mapendekezo ya Miundo ya Taasisi kutoka Taasisi za Umma *mbili (2)* ambazo ni Tume ya Maadili na Baraza la Mitihani Zanzibar *(BAMIZA)*. Pia, muundo wa Utumishi wa Bodi ya Mapato ya Zanzibar *(ZRB)*umeidhinishwa. Rasimu ya *pili(2)* ya Muongozo wa Usalama na Afya kazini imeandaliwa ambapo maoni ya wahusika wengine yamepokelewa. Vilevile, watumishi *wanne (4)* wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika Fani ya Usimamizi wa Rasilimali watu.

Widha, Kamisheni imepokea rufaa *moja (1)* na malalamiko *manne (4)*ambayo yameshughulikiwa na kutolewa uamuzi ambapo kesi zilizoshughulikiwa zinawahusu aliyekuwa mtumishi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar na watumishi *watano (5)* kutoka Wizara ya Fedha na Mipango.

2.1.18 TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

Tume ya Utumishi Serikalini imeanzishwa kwa mujibu wa *Katiba ya Zanzibar* ya mwaka *1984*, ibara ya *117* sambamba na *Sheria ya Utumishi wa Umma, nambari 2 ya mwaka 2011*. Tume inaundwa na Bodi ambayo inajumuisha Mwenyekiti na Wajumbe *sita (6)* ambapo kiutendaji imegawika katika vitengo *vinne (4)* ikiwa ni Kitengo cha Ajira, Kitengo cha Nidhamu na Sheria, Kitengo cha Utawala na Kitengo cha Fedha ambavyo vipo chini au usimamizi wa Katibu wa Tume ya Utumishi Serikalini.

Kwa mujibu wa Sheria, Tume ya Utumishi Serikalini imepewa mamlaka ya kuajiri watumishi wapya, kuthibitisha kazini watumishi

wapya, kuidhinisha nyongeza za muda wa utumishi, ajira za mikataba, kupandisha daraja, kuidhinisha kustaafu kazi kwa watumishi waliofika umri wa kustaafu kazi kwa lazima, wenye maradhi na kwa hiari, kubadilisha kada na kuacha kazi kwa hiari.

Tume ya Utumishi Serikalini inawajibika kusimamia haki na nidhamu za watumishi walio chini ya usimamizi wa Tume pamoja na kuidhinishwa kuwafukuza kazi watumishi waliokwenda kinyume na Sheria na Taratibu za Utumishi.

Vilevile, Tume ina jukumu la kupokea, kusikiliza na kuyatolea maamuzi sahihi malalamiko na Rufaa zote zinazowasilishwa baada ya kuzingatiwa taratibu zote kwa mujibu wa Sheria na Kanuni.

Aidha, Tume hupokea na kusikiliza na kuyatolea maamuzi sahihi malalamiko na rufaa zote zinazowasilishwa baada ya kuzingatiwa taratibu zote kwa mujibu wa sheria na kanuni.

Katika kipindi cha mwaka unaomalizika, Tume imepata mafanikio yafuatayo:

(a) Imeweza kutoa ajira kwa kuzingatia misingi ya haki na usawa kulingana na maelekezo ya *Sheria ya Utumishi wa Umma, nambari 2 ya mwaka 2011* na *Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014.* Hali hii imepelekea Tume kuajiri vijana wengi wenye sifa zinazofaa kulingana na elimu zao na mahitaji ya Serikali.

(b) Tume imeweza kueleweka zaidi kutokana na mwamko wa vijana katika kuwasilisha maombi na utaratibu unaotumika katika suala la ajira umefahamika kwa vijana wanaomaliza vyuo na wananchi kwa ujumla.

Licha ya mafanikio iliyopata, pia, Tume **inakabiliwa na changamoto** zifuatazo ambazo hupelekea Tume kushindwa kutekeleza majukumu iliyojipangia:

(a) Tume haina usafiri kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa shughuli zake za kila siku.

(b) Tume inakabiliwa na tatizo la nafasi za kuhifadhia Nyaraka zinazowasilishwa mara kwa mara katika Ofisi hii hususani wingi wa maombi inayopokea kutoka kwa waombaji kazi.

(c) Baadhi ya nafasi zinazokosa wataalamu wenye sifa kwa kuzijaza nafasi hizo (kada adimu) kwa mfano kwa kada ya *'Soro veya Survey'*, *'Geologist'* na *'Mining Engineer'*.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

Kamati ilitoa maoni na ushauri ufuatao kwa Tume ya Utumishi Serikalini:

(i) Tume **inaigiza**kuchukuwa tahadhari ya hali ya juu kuhusiana na tabia ya baadhi ya waajiriwa kuomba nafasi za ajira katika maeneo ambayo hawapo tayari kufanya kazi na mara tu baada ya kuajiriwa huchukua uhamisho na kupelekea kuendelea kwa upungufu katika eneo hilo.

(ii) Tume **inaagizwa**kuhakikisha kuwa wakati wa ajira unapofika, watu wenye ulemavu wanapewa kipaumbele cha kuajiriwa kwa mujibu wa sifa zao na mahitaji halisi.

(iii) Kamati inashauri kufanyika kwa uchunguzi utakaoweza kubaini iwapo kama kuna watendaji hewa ndani ya utumishi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

(iv) Kamati **inaiagiza** Tume ya Utumishi Serikalini kufuatilia utekelezaji wa sheria, kanuni na taratibu zinazohusiana na ajira katika wizara/taasisi za umma ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa nidhamu ya kazi inakuwepo.

(v) Vile vile, Kamati imebaini kwa kipindi kifupi kijacho watumishi wengi hasa katika kada ya Ualimu na Udaktari watafikishaumri wa kustaafu kwa lazima, hivyo, Serikali ijiandae mapema kukabiliana na tatizo hilo hasa kwa vile watumishi hao wanautaalamu na uzoefu wa kutosha wa kazi.

2.1.19 KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA

Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ni taasisi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambayo imeundwa chini ya Sheria ya Kamisheni

ya Wakfu na Mali ya Amana, nambari *2* ya *2007*. Kamisheni inashughulikia mambo yanayohusiana na mali za Wakfu kwa Waislamu; inashughulikia taratibu za Hija kwa mahujaji wanaotoka Zanzibar pamoja na kukusanya na kugawa Zakka na vitu vyengine vinavyohusiana.

Kamisheni imepata mafanikio mazuri ya kiuhusiano baina yake na Taasisi mbalimbali za nje ikiwemo Mamlaka ya Wakfu ya Uturuki. Aidha, jamii imehamasika katika suala la uwekaji wa Wakfu na utoaji wa Zakka kwa kiasi kikubwa. Vilevile, wananchi wameshajihishika kurithishana kupitia Kamisheni baada ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupunguza ada kutoka asilimia *5* ya awali hadi kufikia asilimia *0.25* Kamisheni, pia, imefanikiwa kuanzisha Tovuti yake katika kuboresha utekelezaji wa majukumu yao.

Warathi ambao tirka zao zimeripotiwa kuanzia *Oktoba* hadi *Disemba,2017* wameendelea kupatiwa haki zao ambapo jumla ya tirka *281* za mirathi zimefunguliwa (*207* Unguja na *74* Pemba), tirka *199* za Unguja na *35* za Pemba zenye thamani ya *Shilingi za Kitanzania 3,985,087,950* zimerithishwa na tayari wamekabidhiwa warathi. Aidha, jumla ya Nyaraka *67* zimetolewa (*60)* za Warathi na *saba(7)* za Mauzo.

Aidha, jumla ya nyumba za Wakfu *260* (*250* Unguja na *kumi (10)* Pemba) na Mashamba *tisa(9)* Pemba yamekaguliwa. Nyumba *kumi (10)* za Wakfu zimefanyiwa matengenezo ambapo jumla ya *Shilingi za Kitanzania 32,036,500* zimetumika kugharamia matengenezo hayo. Vile vile, jumla ya *Shilingi za* Kitanzania*106,278,650* za kodi zimekusanywa kwa nyumba za Wakfu, *Shilingi za Kitanzania33,960,700*kwa nyumba za Amana na *Shilingi za Kitanzania2,280,000*zimepatikana kwa ukodishaji wa mashamba ya Wakfu na Amana. Aidha, huduma za utekelezaji wa wasia na huduma za Misikiti mbalimbali zimetolewa na jumla ya *Shilingi za*

Kitanzania16,692,958 zimetumika pamoja na kusajili Wakfu mpya nne*(4).*

Ofisi imekusanya na kusambaza kwa wananchi Unguja na Pemba msaada wa chakula, misahafu, vitabu, nguo na fedha taslim wenye thamani ya Shilingi za Kitanzania396,885,000.

CHANGAMOTO ZA KAMISHENI YA WAKFU

Mbali ya mafanikio yaliyopatikana, Kamisheni inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa vitendea kazi ambavyo haviendani kabisa na wakati kutokana na teknolojia ya kisasa inayotumika sasa ulimwenguni.

KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA PEMBA

Kwa upande wa **Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Pemba**, inatekeleza majukumu yake ya msingi ya kusimamia mali za Wakfu, Amana, Mirathi ya Kiislamu, Sala na Baraza la Iddi Kitaifa, kuratibu safari za Hijja, ukusanyaji na ugawaji wa Zakka na Sadaka na misaada ya kheri.

Katika kipindi cha *Oktoba – Disemba, 2017,* Ofisi ilipangiwa kukusanya jumla ya *Shilingi za Kitanzania 20,178,800,* hata hivyo, imefanikiwa kukusanya jumla ya *Shilingi za* Kitanzania 21,895,300 ambazo ni sawa na asilimia *108.5%* licha ya Nyakfu nyengine mara hii kukodishwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na kwa madai ya kwamba ni shamba zilizokatwa eka na Serikali. Aidha, fedha hizo ni makusanyo ya ndani ya kodi za nyumba za Wakfu/Amana na mashamba ya Wakfu/Amana ya makadirio yote.

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI KAMISHENI

Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Pemba inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Ufinyu wa bajeti unaopelekea Kamisheni ya Wakfu kutofikia malengo iliyojiwekea.
(ii) Badhi ya wananchi kutumia uwezo wao wa kifedha na kiwazifa kuhodhi maeneo ambayo yako chini ya usimamizi wa Kamisheni.
(iii) Wananchi kuitumia vibaya sheria ya eka tatu (3) na kupinga agizo la Baraza la Mapinduzi la mwaka *1993* la kuyarejesha mashamba ya Wakfu/Amana kwa Katibu Mtendaji Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(i) Kamati **inaiagiza** Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kukaa pamoja na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kulitafutia ufumbuzi suala la mashamba ya yaliyo chini ya Kamisheni kuchukuliwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ili kila *mmoja (1)* afahamu mipaka yake.
(ii) Kamisheni **inashauriwa** kuendelea kutoa elimu na kuihamasisha jamii juu ya umuhimu wa kuitumia Kamisheni badala ya kusuburi mpaka wanapopatwa na matatizo.
(iii) Kamati inaagiza Wizara kutafutia ufumbuzi kwa migogoro yote ya Mashamba ya Waqfu na Mali za Amana kwa upande wa Pemba kutokana na malalamiko mengi kuhusiana na wahusika kukosa haki zao kutokana na kushikiliwa na Kamasheni hii.
(iv) Kamati inashauri maafisa wa Kamisheni kushirikiana kikamiifu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kesi zote ambazo Kamisheni inatakiwa kuzisimamia na kuwapatia wahusika haki zao.
(v) Kamati inaigiza Kamasheni kuchukuwa hatua za haraka mara tu wanapoona Mashamba na mali za Amana zinavamiwa na kuchukuliwa ni watu wasiojua umuhimu wa Amana na Mali za Waqfu. Hii itasaidia jamii kuelewa umuhimu wa Taasisi hii muhimu katika kusimamia haki za Waislamu katika Nchi yetu.

(vi) Kamati inaigiza Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kufanya mazungumzo na Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kufikia muafaka kwa kila upande uwe na Akaunti yake kwa masuala ya Hijja ili kuepusha usumbufu unaojitokeza kwa Mahujaji wa Zanzibar.

2.1.20 OFISI YA MSAJILI WA HAKIMILIKI

Ofisi ya Msajili wa Hakimilikiimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Hakimiliki, *nambari 14 ya mwaka 2003*. Miongoni mwa majukumu ya Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki ni kusimamia, kulinda pamoja na kutetea haki na maslahi ya wasanii, kukusanya na kugawa mirahabainayotokana na matumizi ya kazi za wasanii.

OFISI YA MSAJILI WA HAKIMILIKI – PEMBA

Ofisi hii imeundwa chini ya Sheria ya Hakimiliki, nambari *14* ya mwaka *2003*katika kipindi kifupi, jumla ya kazi*50* za hakimiliki zimesajiliwa na kuingizwa katika mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu na kuwa na takwimu ya wanufaika wa mirabaha.

Aidha, jumla ya vipindi kumi vimerikodiwa na kurushwa hewani na vituo vya Utangazaji vya *"Hits FM"* na *"Zanzibar Cable"*. Mkutano mmoja wa mafunzo juu ya Hakimiliki katika zama hizi za kidigitali *(Copyright and the Digital Environment)* umefanyika kwa kushirikiana na Shirika la Milki bunifu Ulimwenguni *(WIPO)*.

Uandaaji wa mfumo wa kielektroniki wa kutambua na kupima kiwango cha matumizi ya kazi za Hakimiliki katika vyombo vya habari umekamilika.

Ofisi imekusanya mirabaha yenye thamani ya shilingi 5,712,000 kutoka kwa watumiaji mbalimbali wa kazi za Hakimiliki kibiashara. Ofisi pia, imewatembelea wabunifu na wasanii wagonjwa kumi katika maeneo yao na kupatiwa kiasi cha fedha kinachotokana na fungu maalum la mafao ya mirabaha.

Vilevile, Ofisi imefanya ukaguzi katika maeneo mbalimbali ya watumiaji wa kazi za Hakimiliki kibiashara. Watumiaji 30 wa kazi za Hakimiliki wamekaguliwa Unguja na Pemba, wakiwemo wenye maduka ya kuuza na kukodisha vinasa sauti vya kusikia na kuona, wenye mahoteli na vituo vya utangazaji. Watumiaji hao walielimishwa juu ya matumizi halali na sahihi ya kazi za Hakimiliki na walitakiwa kukata leseni ya Hakimiliki ili kufanya biashara zao kihalali.

Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki – Pemba, ina jumla ya watumishi *wanne (4)*, kati ya hao mwanamme *mmoja (1)*na wanawake*watatu(3)*. Aidha, Ofisi imefanya ukaguzi kwa watumiaji wa kazi za sanaa katika Wilaya ya Mkoani, Wilaya ya Wete, Wilaya ya Chake Chake na Wilaya ya Micheweni, kwa ajili ya kuhakikisha kuwa watumiaji hao wanafanya kazi zao kwa mujibu wa Sheria ya Hakimiliki, nambari *14* ya mwaka *2003* pamoja na kuendelea kulinda, kusimamia na kutetea kazi za wasanii.

Ofisi imekusanya jumla ya Mirabaha yenye thamani ya *Shilingi za Kitanzania 3,320,000* zinatokana na matumizi ya kazi za wasanii.

CHANGAMOTO ZA OFISI YA HAKIMILIKI

Ofisi kwa upande wa Pemba inakabiliwa na changamoto ya usafiri wa uhakika ambao unahitajika katika zoezi zima la usimamizi wa kazi za wasanii ambapomara nyingi hulazimika kutumia magari kutoka kwa Ofisa Mdhamini wakati wa kufanyadoria ili kuwatambua watumiaji haramu wa kazi za wasanii na kuwapa maelekezo na ufafanuzi wa kisheria.

MAONI NA USHAURI WA KAMATI

(a) Kamati inashauri Serikali kuboresha miundombinu ya Ofisi ya Hakimiliki ikiwemo suala zimala usafiri na vifaa vyengine vya utendaji ili kutekelza ipasavyo majukumu yao ya kusimamia haki za wasanii.

(b) Aidha, Kamati inashauri hatua kali kuchukuliwa dhidi ya watu wenye kughushi kazi za wasanii ili kusaidia kulinda maslahi ya wasanii ambao wamaamua kujiajiri wenyewe kujtokana na hali ngumu ya maisha.

2.1.21 TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar ni taasisi iliyoundwa kwa mujibu wa *Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria,* nambari *16* ya mwaka *1986* yenye jukumu la kufanyia mapitio sheria mbalimbali nchini.

Tume ilifanyia mapitio baadhi ya sheria zikiwemo *Sheria ya Jumuiya*, nambari *6* ya mwaka *1995*; Sheria ya Kamati ya Uongozi, nambari 10 ya mwaka *1986*; Sheria ya Mahakama Kuu, nambari *2* ya mwaka *1985*; Sheria ya Mahakama za Chini nambari 6 ya mwaka *1985*; Sheria ya Msimamizi wa Mirathi, Sura ya *23* ya mwaka *1925* ambayo imependekezwa kufutwa kutokana na marekebisho yaliyofanywa katika Sheria ya Mirathi kwa Wasio kuwa Waislamu, Sura ya *21* ya mwaka *1917*. Wakati wa mapitio hayo, Tume ilikukusanya maoni ya wananchi katika Wilaya zote za Unguja na Pemba pamoja na kutoa elimu.

Aidha, ushirikiano wa Kitaifa na Kimataifa umeimarishwa kwa kulipia ada za mwaka za uanachama wa Tume za Kurekebisha Sheria za Mashariki na Kusini mwa Afrika *(ALRAESA)*, na Umoja wa Tume za Kurekebisha Sheria za Nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola *(Calras)*.

Tume, pia, imetafsiri *Sheria ya Mikataba*, sura ya *149* ya mwaka *1917* na *Sheria ya Mawakili Binafsi*, sura ya *28* ya mwaka *1941* katika lugha nyepesi ya Kiswahili yenye kufahamika kwa urahisi.

2.1.22 MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI(ZAECA)

Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar ni taasisi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iliyoundwa chini ya *Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi*, nambari *1* ya mwaka *2012* ambapo inatekeleza majukumu makuu yafuatayo:

(a) Kufanya utafiti na kuzishauri taasisi za umma na binafsi juu ya namna ya kudhibiti mianya ya rushwa na uhujumu wa uchumi.
(b) Kutoa elimu kwa umma inayohusiana na rushwa na uhujumu wa uchumi pamoja na athari zake kwa lengo la kuishirikisha jamii katika kuzuia rushwa na uhujumu wa uchumi na kubadilisha mitazamo yao kuhusiana na rushwa na uhujumu wa uchumi.
(c) Kufanya uchunguzi dhidi ya vitendo vya rushwa na uhujumu wa uchumi.

Kuundwa kwa Mamlaka hii kunatokana na azma ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika mapambano yake dhidi ya rushwa kama ilivyoelezwa katika mipango ya Maendeleo ya Taifa Zanzibar: DIRA ya *2020* pamoja na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini. Ofisi kuu ya Mamlaka ipo Unguja na Ofisi ndogo za mikoa zipo Chake Chake Mkoa wa Kusini Pemba na Kinyasini, Mkoa wa Kaskazini Pemba.
Mamlaka katika utekelezaji wa majukumu yake, ilitoa elimu kwa umma yenye lengo la kudhibiti na kuzuia kikamilifu vitendo vya rushwa na uhujumu wa uchumi nchini ambapo ilifanya mikutano iliyozihusisha taasisi za Serikali, binafsi n mamoja na wananchi kwa ujumla Unguja na Pemba.

Aidha, Mamlaka iliandaa vipindi vya televisheni na redio vilivyorushwa hewani kupitia Shirika la Habari Zanzibar (ZBC) vilivyoelezea juu ya

madhara ya rushwa na uhujumu uchumi ikiwemo namna bora ya kuweza kuepukana na vitendo hivi nchini.

Katika kipindi cha *Oktoba – Disemba 2017*, Mamlaka imepokea jumla ya tuhuma *51* za makosa mbalimbali yakiwemo kuomba na kupokea rushwa, matumizi mabaya ya Ofisi, matumizi mabaya ya mali za umma, kukwepa kulipa kodi na rushwa katika zabuni. Ofisi imekamilisha uchunguzi wa tuhuma *11* na majalada yake kupelekwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa hatua za kisheria.

Vilevile, Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kuzuia Rushwa umepitishwa na Baraza la Mapinduzi Zanzibar na kuanza kutoa elimu kwa taasisi zote zinazojumuisha mapambano dhidi ya rushwa ili kufanikisha kuundwa kwa kamati mbili *(2)* zenye lengo la kutathmni utekelezaji wa mkakati huo.

MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI PEMBA

Mamlaka kwa upande wa Pemba ina jumla ya watumishi *17*, kati ya hao, watumishi *10*kutoka Mkoa wa Kusini, Pemba na watumishi *saba 7* kutoka Mkoa wa Kaskazini, Pemba.

Ushirikiano wa kiutendaji katika Ofisi za Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar kisiwani Pemba umeimarika zaidi katika Ofisi hii na wadau wengine wa kupambana na rushwa na uhujumu wa uchumi baada ya Ofisi kusogezwa katika Mkoa Kaskazini, Pemba.

Katika kipindi cha utekelezaji *Octoba – Disemba, 2017,*Mamlaka kupitia Idara yake ya Elimu kwa Umma na Udhibiti imetoa elimu ya rushwa na kuwafikia wananchi wasipoungua *1,825*ambapo kati ya hao *1,499* ni kutoka Mkoa wa Kusini Pemba na wananchi *326* kutoka Mkoa wa Kaskazini Pemba. Elimu hiyo ilihusisha mikutano ya hadhara katika shehia, mikutano na watumishi wa umma, semina

mbalimbali, elimu ya uanzishwaji wa klabu za mpinga rushwa mashuleni, warsha mbali mbali pamoja na bonanza.

Vilevile, Mamlaka imetoa elimu ya rushwa kupitia vipindi vya redio jamii iliyoko Micheweni na redio Istiqama iliyoko Chake Chake, Mamlaka inaamini kuwa redio hizi zina idadi kubwa ya watumiaji katika kisiwa cha Pemba.

Mamlaka inaendelea kukemea vitendo hivi kwa kufanya udhibiti mbalimbali katika kuhakikisha kuwa fedha/mali za Serikali hazibakii kwenye mikono ya watu wachache. Mamlaka imefanikiwa kuokoa jumla ya shilingiza Kitanzania *163,018,000*, kati ya hizo shilingi za Kitanzania *84,705,500* zimeokolewa kutoka Mkoa wa Kusini, Pemba na shilingi za Kitanzania *75,312,500* zimeokolewa kutoka Mkoa wa Kaskazini, Pemba. Uokozi huo umefanyika kupitia zao la karafuu, Hospitali ya *'Cottage'* Micheweni, pamoja na kodi mbalimbali zilizokuwa zinataka kukwepwa kupitia bandari ndogo ya Wesha.

Aidha, katika kipindi cha mwezi wa*Disemba, 2017* ambapo wananchi wengi hutumia bandari ya Mkoani kusafiri, Mamlaka ilipokea malalamiko mengi juu ya ulanguzi wa tiketi unaofanywa na watu wasio kuwa waaminifu, hivyo,Mamlaka imeweza kufanya udhibiti au doria za kushtukiza bandarini hapo na kuwachukulia hatua wale wote wanaohusika, operesheni hizo za mara kwa mara zimezaa matunda kwa kiasi kikubwa kwani uhalifu huo umepungua bandarini hapo.

Miongoni mwa taarifa au malalamiko yaliyopokelewa katika kipindi hiki cha *October – December, 2017* zinahusiana na matumizi mabaya ya mali na mapato, mgongano wa maslahi, matumizi mabaya ya Ofisi, ukiukwaji wa Sheria na taratibu za manunuzi, kushawishi katika kutenda kosa, kutoa ushauri wa siri kwa lengo la kujipatia maslahi kinyume na utaratibu, kuomba na kupokea rushwa pamoja na matumizi mabaya ya rasilimali.

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI'ZAECA' PEMBA

Pamoja na utekelezaji mzuri wa majukumu ya Mamlaka hii ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi kwa Ofisi za Pemba, Ofisi inaendelea kukabiliwa na changamoto zifuatazo:

(a) Usafiri umekuwa ni kikwazo kikubwa kwa ofisi hii huku ikizingatiwa mazingira ya kazi inayofanya/inayokabiliana nayo kwani Ofisi ina gari *moja(1)* tu ambayo inatumiwa naOfisi zote *mbili(2)* – Kaskazini na Kusini, Pemba, suala hili linakosesha ufanisi katika kazi za Ofisi.

(b) Muhali katika kutoa taarifa kwa wananchi wa kawaida na watumishi kuhusiana na masuala ya rushwa licha ya kutolewa kwa elimu mara kwa mara.

(c) Ushirikiano mdogo kati ya Mamlaka hii na Taasisi nyengine za umma.

(d) Uhaba wa watumishi.

(e) Kukosekana kwa jengo la kudumu kwa Ofisi ya Mkoa wa Kusini Pemba iliyopo Chake Chake kwani jengo linalotumika sio la Serikali.

(f) Kutishiwa amani na usalama wao watendaji wa ZAECA wakati wa kutekeleza majukumu yao.

(g) Wafanyakazi wa Mamlaka hii Kisiwani Pemba mara nyingi inabidi watumie usafiri wa vespa katika kutekeleza kazi zao hali ambayo ni hatari hasa wakati wa operesheni maalum na kipindi cha mvua.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(a) Kamati **inawataka** watendaji wa Mamlaka kuwa waaminifu na kutokubali kurubumiwa kwa njia yoyote.

(b) Kamati **inaiagiza** Mamlaka kulitafutia ufumbuzi tatizo la uhaba wa vifaa hasa usafiri wa gari na vifaa vyengine ambavyo vitawasaidia watendaji wake katika kupambana na wahalifu pamoja na kulinda usalama wao.

(c) Kamati **inaiagiza** Mamlakakwa kushirikiana na Ofisi kuu kuhakikisha kwamba inalipatia ufumbuzi tatizo la usafiri ikiwa ni pamoja na kuliingiza katika bajeti ya mwaka wa fedha *2018/2019*.

(d) Kamati **imeitaka** Mamlaka kulitafutia ufumbuzi tatizo la jengo la kudumu kwa Ofisi ya Mkoa wa Kusini Pemba iliyopo Chake Chake.

(e) Kamati **inashauri** Mamlaka kuzidi kusimamia na kutetea haki za wananchi hasa wale wa tabaka la chini ambao ndio waathirika wakubwa wa vitendo vya rushwa na uhujumu wa uchumi.

Aidha, Kamati**inapongeza sana** juhudi za ZAECA Pemba, kwa kufanya kazi kwa bidii na kujitolea kwa moyo wa Uzalendo kuwafichua wahalifu na kuwachukulia hatua zinazostahiki. Kamati inshauri jamii kuunga mkono juhudi hizo na kusaidia kwa hali na mali katika kuwafichua walarushwa na wahujumu uchumi wa Nchi yetu.

2.1.23 CHUO CHA UTAWALA WA UMMA

Chuo cha Utawala wa Umma (*Institute of Public Administration – IPA)* ni Taasisi ya Serikali ambayo imesajiliwa rasmi Zanzibar kimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Taasisi ya Utawala wa Umma, nambari *1* ya mwaka *2007*. Chuo hiki kimeanzishwa kwa ajili ya kuunga mkono programu ya kuimarisha watumishi wa umma. Chuo kinaendesha na kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa wanafunzi wa fani mbalimbali.

Mafunzo mbalimbali yametolewa kwa watumishi *521* ambapo mafunzo ya *'e – Library'* na uandaaji wa taarifa za Chuo *(Prospectus)* yalitolewa kwa watumishi wa Chuo na Wakufunzi kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Zanzibar *(SUZA)* na Zanzibar University *(ZU)*. Aidha, mafunzo juu ya Kanuni za Wanafunzi *(Students Regulations)* yalitolewa kwa Serikali ya Wanafunzi.

Mtumishi *mmoja (1)* ameshiriki mafunzo ya muda mfupi ya utunzaji wa nyaraka na kumbukumbu Tanzania Bara. Vilevile, watumishi *watatu(3)* wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu ya uzamili katika fani ya Uchumi na Utawala na *watatu(3)* shahada ya kwanza katika fani ya uhifadhi wa nyaraka na kumbukumbu, ununuzi na ugavi.

CHUO CHA UTAWALA WA UMMA – PEMBA

Kwa upande wa Chuo cha Utawala wa Umma Tawi la Pemba, jumla ya wanafunzi *68* waliweza kujiunga na Chuo katika muhula huu na kufanya idadi ya wanafunzi kufikia *349*, kati ya hao *109* sawa na asilimia *31.2* ni wanaume na *240* sawa na

asilimia 68.8 ni wanawake. Aidha, wanafunzi *150* sawa na asilimia *43* miongoni mwa wanafunzi wote ni watumishi wa Serikali.

Katika kutekeleza jukumu la kuwaendeleza wafanyakazi, Chuo kimeendesha mafunzo elekezi ya muda mfupi kwa wafanyakazi wapya 17 wa Taasisi za umma. Kupitia mafunzo hayo jumla ya *Shilingi za Kitanzania 2,550,000* zimekusanywa.
Aidha, Chuo kwa kushirikiana na Idara ya Ardhi, kimefanikiwa kupata Ardhi kwa ajili ya ujenzi wa Chuo kwa upande wa Pemba. Eneo hilo lipo Mgogoni *(njia ya kuelekea uwanja wa ndege)* Chake Chake na kwa sasa hatua za kutayarisha michoro zinaendelea kufanyiwa kazi na Idara ya Ardhi. Vilevile, Chuo kimefanikiwa kukusanya ada hadi kufikia asilimia *95*ya makusanyo yatokanayo na wanafunzi hao.

CHANGAMOTOZINAZOKIKABILI CHUO CHA UTAWALA WA UMMA – PEMBA

Chuo kinakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(a) Ukosefu wa walimu wa kudumu ambapo Chuo kinatoa kozi katika fani tofauti za cheti na diploma lakini hakina hata mwalimu mmoja ambaye ni wa ajira ya kudumu.
(b) Ubovu wa miundombinu ya njia *(barabara)* inayokwenda katika Chuo hicho hususani wakati wa mvua za masika na vuli.
(c) Ukosefu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.
(d) Uhaba wa fedha kwa ajili ya matumizi katika Chuo hicho.
(e) Idadi ndogo ya wanafunzi waliojiunga na Chuo muhula ulioanzia *Novemba 2017* ambayo imetokana na mabadiliko ya mihula ya kuanzia masomo.
(f) Mabadiliko ya ghafla ya kuanza kwa mihula yaliyotokana na maelekezo ya *'NACTE'*.
(g) Ukosefu wa majengo ya kudumu kwa chuo hicho.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(i) Kamati **inashauri**uongozi wa Chuo ushirikiane na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kutafuta kila njia ili kuhakikisha kwamba walimu wa kudumu wanapelekwa katika tawi lao la Pemba kwa ajili ya kuimarisha hadhi na huduma katika Chuo hicho.

(ii) Kamati **inaagiza** uongozi wa Chuo kusimamia nidhamu ya wanafunzi ili kujenga mazingira bora ya kitaaluma na kuwa watumishi bora wa baadae.

*(iii)*Kamati **inaagiza** Uongozi wa Chuo kuchukua hatua za kitaalamu katika kulifanyia utafiti eneo ambalo wamepata kwa ajili ya ujenzi wa Chuo kama linakidhi mahitaji na kanuni za ujenzi basi kuliendeleza eneo hilo kama taratibu za kisheria zimeshakamilika.

SEHEMU YA TATU

3. WIZARA YA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

3.1 UTANGULIZI

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ina jukumu la kuratibu, kusimamia shughuli za Ofisi pamoja na kuratibu shughuli za Mamlaka ya Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Kusimamia utekelezaji wa Idara Maalum za SMZ.

Vile vile, Ofisi inasimamia mazingira ya ushiriki wa wananchi katika kudumisha amani, ulinzi wa mali zao, kuimarisha huduma za kijamii, kuhakikisha kuwa, kila mtu anashiriki katika kupanga na kusimamia shughuli za maendeleo katika maeneo yakekwa kuzingatia misingi ya utawala bora ikihusisha kuwatambuwa wakaazi wa maeneo husika na utambulisho wao.

Dira ya Ofisi hii ni kuwa Taasisi imara katika kusimamia amani, usalama, usajili wa wakaazi na upatikanaji wa huduma karibu na wananchi.

Malengo Makuu ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ni:

(a) kudumisha amani na utulivu;
(b) kuwafanya vijana wawe na maadili mema na mtazamo wa kujiajiri wenyewe;
(c) kustawisha haki za wanafunzi waliohalifu kisheria;
(d) kutoa huduma bora kwa jamii; na
(e) kuimarisha maendeleo ya wananchi wa Zanzibar.

Vile vile, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaundwa na kusimamia Idara na Taasisi mbalimbali zilizogawika maeneo makuu *manne (4)* katika kutekeleza majukumu yake ikiwemo Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba.

Aidha, Kamati inaipongeza sana Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuweza kuwapatia fedha ambazo waliomba na kuidhinishiwa katika bajeti ya mwaka

wa fedha *2017/2018* kwa asilimia kubwa mpaka kufikia baadhi ya Taasisi kuvuka malengo yaliyokadiriwa katika Taasisi na Idara zake, jambo ambalo linaleta faraja kwa watendaji lakini na hata jamii inafaidika sana kutokana na upatikanaji nzuri wa fedha za miradi ya maendeleo kwa ujumla.

3.2 IDARA NA TAASISI ZA WIZARA YA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

3.2.1 IDARA ZA KAWAIDA

(i) Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
(ii) Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
(iii) Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ;
(iv) Tume ya Utumishi wa Idara Maalum za SMZ;
(v) Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
(vi) Ofisi ya Usajili wa Vizazi, Vifo na Kadi za Utambulisho; na
(vii) Ofisi Kuu Pemba.

3.2.2 MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MIKOA

(i) Mkoa wa Mjini Magharibi;
(ii) Mkoa wa Kusini Unguja;
(iii) Mkoa wa Kaskazini Unguja;
(iv) Mkoa wa Kusini Pemba; na
(v) Mkoa wa Kaskazini Pemba.

3.2.3 MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA

(i) Baraza la Manispaa ya Mjini;
(ii) Baraza la Manispaa ya Magharibi ‘A’;
(iii) Baraza la Manispaa ya Magharibi ‘B’;
(iv) Baraza la Mji – Wete;

(v) Baraza la Mji – Chake Chake;
(vi) Baraza la Mji – Mkoani;
(vii) Wilaya ya Mjini;
(viii) Wilaya ya Magharibi 'A';
(ix) Wilaya ya Magharibi 'B';
(x) Wilaya ya Kaskazini 'A'
(xi) Wilaya ya Kaskazini 'B'
(xii) Wilaya ya Kati – Unguja
(xiii) Wilaya ya Kusini - Unguja
(xiv) Wilaya ya Mkoani;
(xv) Wilaya ChakeChake;
(xvi) Wilaya ya Wete;
(xvii) Halmashauri ya Wilaya ya Kusini – Unguja;
(xviii) Halmashauri ya Wilaya ya Kati - Unguja;
(xix) Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'A';
(xx) Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'B'
(xxi) Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni.

3.2.4 IDARA MAALUM ZA SMZ

(i) Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo *(KMKM)*;
(ii) Jeshi la Kujenga Uchumi *(JKU)*;
(iii) Chuo cha Mafunzo *(MF)*;
(iv) Kikoksi cha Zimamoto na Uokozi (KZU); na
(v) Kikosi cha Valantia *(KVZ)*.

3.3 IDARA ZA KAWAIDA

3.3.1 IDARA YA MIAPANGO SERA NA UTAFITI

Idara ya Mipango,Sera na Utafiti ndio kiungo baina ya Taasisi za Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ na

wizara/taasisi nyengine, Kamati imeelezwa kuwa, Idara hii imeendelea kuratibu utekelezaji wa malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka *2015*, pamoja na kuandaa Mpango kazi na ufuatiliaji na tathmini katika miradi *kumi* ya maendeleo inayotekelezwa.

Idara pia, inaendelea kuratibu shughuli za masomo kwa watendaji wake pamoja na kuandaa vikao kwa maafisa mipango juu ya masuala ya mipango na uandaaji wa taarifa za msingi za ofisi.

Licha ya majukumu yote hayo ambayo Idara hii imekuwa ikiyaratibu, Kamati imebaini kuwa uingizwaji wa fedha za matumizi kwa Idara hii umekuwa tofauti kidogo na Idara nyengine zilizochini ya Wizara hii, hivyo juhudi zaidi zinahitajika kwa kupatiwa asilimia inayokidhi mahitaji yao.

3.3.2 IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Idara ya Uendeshaji na Utumishi ina jukumu la kutoa na kusimamia huduma za uendeshaji na utumishi katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, zikiwemo kusimamia sheria na kanuni zinazosimamia utumishi na uendeshaji wa Ofisi, kuwaendeleza wafanyakazi kielimu pamoja na kusimamia utumishi na vitendea kazi na kuendelea na kusimamia utunzaji wa kumbukumbu.

Katika vipindi tofauti, Idara imekuwa ikiratibu shughuli za uendeshaji wa Ofisi kwa kuipatia vifaa mbalimbali vya kiofisi, kufanya matengenezo ya magari pamoja na kutoa huduma za kiutawala kwa kusimamia safari za viongozi na watendaji mbalimbali wa Ofisi. Vilevile, Idara imeweza kufanya malipo ya huduma za umeme, maji na mafuta kwa matumizi ya Ofisi.

Sambamba na hayo, Idara imefanya malipo ya masomo kwa watendaji wa Ofisi hii katika fani mbalimbali za kitaaluma ikiwemo Rasilimali Watu na TEHAMA.

Aidha, Kamati inaipongeza Idara ya Uendeshaji na Utumishi kwa kufanya ukaguzi katika Taasisi zilizochini ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ikiwemo Ofisi ya Kadi za Utambulisho, Jeshi la Kujenga Uchumi, Fedha za Mfuko wa Jimbo pamoja na kupitia Ripoti ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Tasisi zote za Ofisi.

3.3.3 IDARA YA URATIBU WA IDARA MAALUM ZA SMZ

Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina jukumu la kuratibu na kusimamia kazi za Idara Maalum za SMZ zikiwemo za utekelezaji wa sera, sheria na kanuni za Idara Maalum na kusimamia vikao vya Mahakama ya Rufaa ya Idara Maalum za SMZ.

Hivyo, Idara hii imeendelea kufuatilia na kusimamia miradi mbalimbali ya KMKM, Chuo cha Mafunzo, JKU na KVZ. Miradi hiyo ni ya ujenzi wa Nyumba za Askari na Mahanga kwa upande wa Pemba na ujenzi wa Chuo cha Kurekebisha tabia wanafunzi watoto. Kwa upande wa JKU kuna ujenzi unaoendelea wa Skuli ya Sekondari Mtoni na KVZ ujenzi wa kiwanda cha kutengenezea viatu kilichopo Makao Makuu yaKVZ Mtoni.

Aidha, Kamati ilitembelea na kuangalia namna kazi hizi zinavyofanyika katika maeneo yote yanayotekelezwa ujenzi huu kwa mashirikiano makubwa yaliyopo baina ya Idara Maalum na Watendaji wa Wizara hii, licha ya changamoto ndogondogo zinazojitokeza katika miradi hiyo.

Vilevile, kikao *kimoja (1)* cha Mahakama ya Rufaa kimefanyika na jumla ya Malalamiko *matatu (3)* yamewasilishwa na kusikilizwa hata hivyo hukumu bado haijatolew. Idara pia, inalengo la kuandaa Sheria ya Idara Maalum za SMZ ambapo ipo katika hatua ya kutafuta washauri elekezi wa ndani ya vikosi. Aidha, Idara ilitoa miongozo kwa lengo la kusaidia

miradi ili ikamilike kulingana na malengo yaliyokusudiwa kwa *robo ya kwanza, July – Septemba 2018.*

3.3.4 IDARA YA URATIBU WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ina jukumu la kuratibu, kusimamia na kutoa miongozo kwa Taasisi za Mamlaka na Serikali za Mitaa. Katika kufanikisha majukumu yake Idara inasimamia utekelezaji wa maagizo ya mipango mikuu ya Serikali, sera za Serikali na kusimamia utekelezaji wa *Sheria ya Serikali za Mitaa, nambari 7 ya 2014* na *Sheria ya Tawala za Mikoa, nambari 8 ya 2014*.

Aidha, Idara inaendeleza Mkakati wa Upelekaji wa Madaraka kwa Wananchi ambapo Idara imekamilisha kazi ya kuandaa Miongozo ya Uundaji wa Mabaraza ya Wadi na Kamati za Mashauriano za Shehia. Miongozo imeelezwa kuwa ni hatua muhimu zinazopaswa kuchukuliwa ili kuwawezesha wananchi kushiriki katika kusimamia uendeshaji wa shughuli za Serikali za Mitaa kuanzia ngazi za Shehia.

3.3.5 AFISI YA USAJILI WA VIZAZI, VIFO NA KADI ZA UTAMBULISHO

Afisi ya Usajili wa Vizazi, Vifo na Kadi za Utambulisho ina dhima ya kisheria ya kusajili vizazi, vifo na Kadi za Utambulisho pamoja na kutunza kumbukumbu zinazotokana na usajili huo. Vilevile, Afisi hii inawajibika kuishauri Serikali kuhusu masuala ya usajili wa vizazi, vifo, utambulisho na ndoa juu ya kutoa mafunzo yanayohusiana na usajili kwa watendaji na wakala wa usajili pamoja na jamii kuhusiana na masuala ya usajili.

CHANGAMOTO ZA OFISI YA USAJILI WA VIZAZI, VIFO NA KADI ZA UTAMBULISHO

(a) Kamati imebaini kwamba kutopatikana vifaa kwa wakati unaohitajika na kwa upungufu mkubwa kama vile vitabu vya fomu za *B1*, *D1* na *D2* katika Shehia na Hospitali kunarudisha nyuma juhudi za Wilaya katika usajili wa vizazi na vifo.

(b) Vile vile, Magamba ya vyeti ni tatizo kubwa katika vituo vya usajili na pia hayapatikani kwa wakati.

(c) Aidha, upungufu wa wafanyakazi katika taasisi za usajili wa matukio ya kijamii imekuwa ni changamoto kubwa kutokana na jamii kukuwa na kuongezeka kwa hamasa ya kujisajili.

(d) Pia, suala la vitendea kazi katika vituo vyoye vya usajili wa vizazi na vifo limekuwa ni kikwazo kwani vifaa hivyo vinavyotumika ni vichakavu na vikongwe ambavyo vimeshapitiwa na wakati.

3.3.5.1 OFISI YA USAJILI WA VIZAZI, VIFO NA KADI ZA UTAMBULISHOWILAYA YA WETE

(a) Kamati imeelezwa kuwa kwa kipindi cha *Aprili* hadi *Juni, 2017* Wilaya ya Wete iliandikisha jumla ya vizazi *1,681* ambapo wanaume ni *848* na wanawake ni *833*, aidha, jumla ya vifo *110* vimesajiliwa ikiwa wanaume ni *55* na wanawake ni *55*.

(b) Aidha, Kamati imeelezwa kuwa wilaya hii imekuwa ya mwanzo kwa kipindi cha *May – July* katika ukusanyaji wa mapato ya uandikishwaji wa vizazi na vifo kwa upande wa Pemba ambapo jumla ya *Shilingi za Kitanzania 1,004,000*zimekusanywa.

(c) Pia, Kamati imeelezwa kuwepo kwa changamoto kubwa ya upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa wakati kutokana na uhaba wa magamba ya vyeti.

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI OFISI

(i) Hali mbaya ya Ofisi ya Vizazi na Vifo inayosababishwa na ufinyu wa nafasi huku ikiwa chumba kimoja cha ofisi ndio hufanywa shughuli zote za kiofisi.

(ii) Ukosefu wa makabati ya kuhifadhia nyaraka mbalimbali za Serikali.
(iii) Uhaba wa vitendea kazi kama vile 'computer', 'printer' na fotokopi.
(iv) Uchakavu mkubwa wa mashine ya kuchapishia vyeti (Ronyo) ambapo inasababisha baadhi ya wakati kushindwa kufanya kazi.
(v) Mwamko mdogo wa kujiandikisha kwa wananchi katika vizazi na vifo hususan wananchi wa vijijini.

MAONI NA USHAURI WA KAMATI

(a) Kamati **inaishaiuri**Wizara kusimamia vyema utekelezaji wa majukumu kwa Taasisi hizi pamoja na kuhakikisha mazingira yao kiutendaji yameboreshwa.
(b) Kamati pia, **inashauri** kuandaliwa kwa mpango maalum utakaotoa elimu kwa wananchi hususan vijijini na visiwani juu ya umuhimu wa kujisajili kwa dhamira ya kuboresha maendeleo ya nchi yetu.

3.3.5.2 OFISI YA VIZAZI, VIFO NA KADI ZA UTAMBULISHOWILAYA YA MICHEWENI

(a) Kamati imeona kuwa uhamasishaji wa usajili wa vizazi na vifo katika wilaya hii ni mdogo kutokana na kuwepo kwa mwamko mdogo wa wananchi katika kujisajili.
(b) Kamati imeelezwa kuwa mapato ya ofisi ya vizazi na vifo kwa kipindi cha *Aprili* hadi *Juni, 2017* ni jumla ya *Shilingi za Kitanzania 640,000.*
(c) Kamati pia, imeelezwa kuwa Ofisi inakabiliwa na tatizo la kutokupatikana kwa vifaa kwa wakati unaohitajika pamoja na upungufu vifaa kama vile fomu ya *B1*, *D1* na *D2* katika Shehia na Hospitali kunarudisha nyuma juhudi za Wilaya katika usajili wa vizazi na vifo.
(d) Magamba ya vyeti ni tatizo na hayapatikani kwa wakati licha ya hayo upatikanaji wake huwa wa idadi ndogo sana ukilinganisha na mahitaji.

(e) Aidha, utendaji wa Ofisi hii uko katika hali ambayo hauridhishi kutokana na idadi kubwa ya matukio ya kijamii ambapo ni wafanyakazi *wawili (2)* tu wanaohudumu katika Ofisi hii.

(f) Kamati pia, imeelezwa kuwepo kwa baadhi ya wananchi ambao hutoa maneno machafu wakati wa kufuata vitambulisho vyao pale wanapokosa kutokana na kuchelewa kutoka Makao Makuu.

(g) Vilevile, Kamati imeelezwa kuwepo kwa uhaba wa watendaji ambapo Ofisi inahitaji angalau watendaji*watatu (3)* ili kuondoa tatizo hili.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(i) Kamati **inashauri** kupatiwa watendaji wengine zaidi ili kuboresha huduma za utoaji wa vyeti kwani Wilaya hii ina idadi kubwa ya vizazi ukulinganisha na wilaya nyengine za Pemba.

(ii) Vile vile, Kamati **inaishauri** Serikali pamoja na Taasisi husika kuwapatia fomu za usajili kwa wakati watendaji wa Wilaya hii, kama vile fomu za *B1*, *D1* na *D2* ili kupunguza idadi kubwa ya watoto wanaosubiri kupatiwa vyeti.

(iii) Sambamba na hayo, Kamati **inaishauri**Ofisi kupatiwa magamba ya vyeti vya kuzaliwa ili kuondoa mrundikano wa wananchi wanaosubiri vyeti vyao kwa muda mrefu sasa.

(iv) Kamati inaishauri Ofisi kutoa elimu kwa jamii kwani sasa wakati umefika kwa jamii kufahamu juu ya umuhimu wa kujisajili na kuwa na vitambulisho vya ukaazi.

(v) Kamati **inaagiza** vitambulisho vilivyokaa kwa muda mrefu bila ya kuchukuliwa na wenyewe virudishwe Makao Makuu ili wenyewe kama bado wapo tayari waende kuvifuata huko au viharibiwe kwa mujibu wa utaratibu uliopo baada ya kupita muda uliokusudiwa kutumika kwa vitambulisho hivyo.

3.3.5.3 OFISI YA VIZAZI NA VIFO, NA OFISI YA KADI ZA UTAMBULISHOWILAYA YA CHAKE – CHAKE

(a) Kamati imeona kuwa katika Ofisi ya vizazi na vifo Wilaya ya Chake – Chake inamfanyakazi *mmoja (1)* tu wa kudumu na msaidizi wake ambaye anajitolea kufanya kazi hii kwa takribani miaka *11* sasa bila ya malipo yoyote.

(b) Kamati imeelezwa kuwa idadi kubwa ya wananchi wanaojifungulia Hospitali hukosa vyeti vya kuzaliwa kwa wakati kutokana na uhaba wa fomu za usajili.

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI OFISI

(i) Kama ilivyo katika wilaya nyengine, katika Wilaya hii pia lipo tatizo la ukosefu wa fomu za *B1*, *D1* na *D2* na kusababisha changamoto kubwa katika usajili wa vizazi na vifo.

(ii) Upungufu wa magamba ya kutengenezea vyeti vya kuzaliwa na vifo.

(iii) Ukosefu wa vifaa vya kisasa vya kuchapishia magamba ya vyeti vya kuzaliwa na vifo.

(iv) Upungufu mkubwa wa watendaji katika Ofisi ya usajili wa kadi za utambulisho; pamoja na

(v) Ufinyu wa vyumba vya Ofisi.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(i) Kamati **inaishauri** Ofisi kuwa, kijana ambaye anafanya kazi kwa muda mrefu zaidi ya miaka *11* sasa, aajiriwe kwani ameshapata uzoefu wa kutosha katika masuala ya usajili wa vizazi na vifo lakini pia, itasaidia kujali maslahi yake na familia yake inayomtegemea. Kamati inaamini kwamba sio rahisi kwa mfanyakazi kujitolea kwa miaka 11 bila kulipwa chochote, lazima zipo njia zisizorasmi ambazo zinatumika kumpatia malipo.

(ii) Kamati **inasisitiza**kuwa ikiwa hakuna mpango wa kumuajiri kijana huyu kuwa mfanyakazi wa kudumu, basi aajiriwe kwa mkataba kwa vile sheria ya uajiri inaruhusu.

(iii) Kamati **inaishauri** Taasisi inayohusika kuipatia magamba ya vyeti Ofisi hii kwa wakati na kwa kuzingatia mahitaji yao.

(iv) Vile vile, Kamati **inashauri** kupatiwa wafanyakazi na wataalamu hasa katika fani za IT *(Informatin Technology)*Ofisi ya Usajili wa Kadi za Utambulisho.

3.3.6 OFISI YA AFISA MDHAMINI PEMBA

Ofisi ya Afisa Mdhamini Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ambayo ndio kiungo kikuu cha kuratibu shughuli zote za Ofisi hasa za Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Kamati imeelezwa kuwa kwa kipindi cha miezi mitatu (*Oktoba* hadi *Disemba, 2017*), Ofisi ya Afisa Mdhamini – Pemba iliweza kutekeleza mambo yafuatayo:

(a) Ofisi imekamilisha taratibu za ununuzi wa gari *mbili (2)* kwa ajili ya shughuli za ufuatiliaji kwa upande wa Pemba.

(b) Ofisi imetekeleza shughuli za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambapo imefanikiwa kufanya vikao *viwili (2)* vya wadau ambavyo vilijadili utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo pamoja na changamoto mbalimbali zinazowakabili kwa lengo la kuzipatia ufumbuzi.

(c) Katika kuwajengea uwezo watendaji, Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba imewapatia fursa za masomo wafanyakazi*sita(6)* wanaoendelea na masomo yao katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi kama ifuatavyo;diploma –*1*, shahada ya kwanza – *1* na shahada ya pili –*4* (wanawake *4* na wanaume *2*).

(d) Vile vile, katika kuimarisha mazingira bora ya Ofisi imeweza kununua vifaa mbalimbali vya kufanyia kazi ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji kwa wafanyakazi. Miongoni mwa vifaa vilivyonunuliwa ni pamoja na wino za printa, vifaa vya kuandikia (stationaries) vifaa vidogovidogo, huduma ya mtandao, maji na umemepamoja na kuzifanyia matengenezo gari na vespa.

(e) Aidha, Ofisi imesimamia upatikanaji wa haki na maslahi ya wafanyakazi ambapo jumla ya wafanyakazi *91* wamepatiwa mishahara yao kwa wakati, posho la likizo na malipo baada ya masaa ya kazi.

CHANGAMOTO ZA OFISI YA AFISA MDHAMINI PEMBA

(i) Uingizwaji wa fedha usio wa kuridhisha kutoka Serikalini, Ofisi bado inakabiliwa na changamoto ya udogo wa ukomo wa bajeti ambapo unapunguza ufanikishaji wa shughuli za kiofisi.

(ii) Aidha, taasisi za Serikali za Mitaa zinakabiliwa na uhaba wa wafanyakazi hasa idara ya mapato na afya, uhaba wa vitendea kazi hususan magari ya kusombea taka pamoja na yale ya kunyonyea maji machafu.

(iii) Kwa upande wa Tawala za Mikoa, changamoto zinazozikabili ni kukosekana kwa nyumba za Serikali za kuishi Wakuu wa Mikoa na Wilaya.

(iv) Kuhusu Idara Maalum za SMZ zinakabiliwa na upungufu mkubwa wa magari kwa ajili ya shughuli za ulinzi ambalo ndio jukumu kubwa la idara hizo. Hata hivyo, zipo gari chache katika Idara Maalum zilizopo kisiwani Pemba ambazo ni chakavu na chache ambazo pia hazikidhi mahitaji.

MAONI NA MAAGIZO WA KAMATI

(i) Kamati **inashauri** kwa mwaka wa fedha unaokuja Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha kuwa inaisaidia Ofisi hii kwa upande wa Pemba katika kuongeza kiwango chao cha bajeti ili wapate kutekeleza majukumu na mipango yao waliyojipangia kwa ufanisi na wakati.

(ii) Kamati **inaishauri** Taasisi inayohusika na uajiri, kuajiri vijana wenye sifa zinazohitajika kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kazi zao.

(iii) Kamati **inaagiza** kufanywa jitihada za makusudi katika kuwapatia vifaa vya kufanyia kazi Mabaraza na Halmashauri zote za Pemba ili ziweze kuwajengea wafanyakazi mazingira bora ya utendaji.

(iv) Kamati **inashauri** baada ya kukamilika kwa mpango wa ujenzi wa Mahanga ya kulala Askari kwa upande wa Idara Maalum basi Serikali ielekeze nguvu zake

katika kuwapatia usafiri wapiganaji hawa kwa kambi zote zilizopo kisiwani Pemba pamoja na ujenzi wa Nyumba za Maafisa wa Vikosi.

3.4 MAMLAKA YA SERIKALI ZA MIKOA

3.4.1 MKOA WA MJINI MAGHARIBI

Mkoa wa Mjini Magharibi ni miongoni mwa mikoa *mitano (5)* ya Zanzibar ambayo imeanzishwa kwa mujibu wa *Sheria ya Tawala za Mikoa, nambari 1 ya mwaka 1998* ambayo imefutwa na kuanzishwa upya ni *Sheria nambari 8 ya mwaka 2014*. Mkoa wa Mjini Magharibi ni Makao Makuu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Manispaa ya Mji wa Zanzibar.

Kiutawala Mkoa wa Mjini Magharibi ni mkusanyiko wa Wilaya *tatu (3)*; Wilaya ya Mjini, Wilaya ya Magharibi *'A'* na Wilaya ya Maharibi *'B'*. Kimakaazi Mkoa huu, kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka *2012* una idadi ya watu wapatao *593,678* (wanawake *310,088* na wanaume ni *283,590*) sawa na asilimia *46* ya wakaazi wote wa Zanzibar.

Aidha, takwimu za sensa ya *2012* zinaonesha kuwa, kila kaya inakaliwa na wastani wa watu *5.2*, Mkoa wa Mjini Magharibi una msongamano mkubwa wa watu ambapo kila kilomita *moja (1)* ya mraba inakaliwa na watu *2,581*. Dira ya Mkoa ni kuwa na wananchi wenye maisha bora katika Mkoa.

MAJUKUMU YA MKOA WA MJINI MAGHARIBI

(a) Kufuatilia, kusimamia na kuwajibika katika utekelezaji wa kazi za Serikali ndani ya Mkoa;
(b) Kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Mipango na Miongozo ya Serikali ndani ya Mkoa;
(c) Kuimarisha ulinzi na usalama;

(d) Kutatua migogoro inayojitokeza ndani ya Mkoa;
(e) Kusimamia haki za Binaadamu;
(f) Kuhakikisha kuwa Sheria na taratibu zilizowekwa zinatekelezwa kwa kushauriana na vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria;
(g) Kuhakikisha kuwa rasilimali zote kama vile vifaa na nguvu kazi vinatumika kwa maendeleo ya uchumi na usatawi wa jamii.

MAFANIKIO YA MKOA WA MJINI MAGHARIBI

(i) Kupungua kwa migogoro ya ardhi;
(ii) Kupungua kwa wanyama wanaozurura ovyo mitaani;
(iii) Mahusiano bora ya taasisi ndani na nje ya Mkoa;
(iv) Kudhibiti ulinzi na usalama wa raia na mali zao;
(v) Ushiriki mzuri wa raia katika shughuli za kijamii na kiuchumi.

CHANGAMOTO ZA MKOA WA MJINI MAGHARIBI

Mkoa wa Mjini Magharibi unakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Ongezeko kubwa la idadi ya watu ndani ya Mkoa;
(ii) Ukosefu wa majengo ya kudumu kwa Wilaya ya Mjini, Magharibi *'B'* na ngazi za Shehia;
(iii) Uhaba wa vitendea kazi;
(iv) Uharibifu wa mazingira ikiwemo vyanzo vya maji na uchimbaji wa mchanga usiofuata utaratibu uliowekwa;
(v) Kuongezeka kwa kesi za udhalilishaji wa wanawake na watoto;
(vi) Uhaba wa madarasa katika skuli za msingi na sekondari.
(vii) Kutokuwepo kwa kituo cha Magari ya abiria ikiwemo Daladala.

3.4.2 MKOA WA KUSINI UNGUJA

Mkoa wa Kusini Unguja ni miongoni mwa mikoa *mitano (5)* ya Zanzibar ambayo ipo chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na

Idara Maalum za SMZ. Mkoa huu unajumuisha Wilaya *mbili (2)* ambazo ni Wilaya Kati na Wilaya ya Kusini Unguja.

Majukumu ya Mkoa wa Kusini Unguja ni kufuatilia, kusimamia, kuratibu utekelezaji wa shughuli za Serikali, kuhakikisha kuwa sera, mipango na miongozo ya Serikali inatekelezwa.

Dhamira ya Mkoa ni kuimarisha uratibu wa upatikanaji wa huduma nzuri kwa wananchi, kuwashirikisha katika kuibua, kupanga, kutekeleza na kutathmini maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Katika kipindi cha *July – Septemba, 2017,* Kamati ilielezwa kuwa Mkoa wa Kusini Unguja umefanikiwa kufuatilia na kutathmini miradi *mitano (5)* ya maendeleo na utekelezaji wa shughuli za sekta zilizotanguliwa katika Serikali za Mitaa ukiwemo mradi wa ufugaji samaki wa maji baridi wa Shehia ya Mgenihaji, ufugaji wa samaki wa Maji chumvi wa Shehia ya Kitogani, kilimo cha mboga mboga Shehia ya Ndijani – Mseweni, ujenzi wa madarasa *manne (4)*, ukumbi *mmoja (1)* na maktaba katika skuli ya Pongwe, pamoja na ujenzi wa Kituo cha mafunzo ya amali Makunduchi.

CHANGAMOTO ZA MKOA WA KUSINI UNGUJA

Mkoa wa Kusini Unguja unakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) ukosefu wa Hatimiliki za majengo ya Serikali kama vile skuli na mashamba;
(ii) uhaba wa matrekta katika msimu wa kilimo cha mpunga;
(iii) uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi na hisabati;
(iv) mwamko mdogo wa wananchi katika ujasiriamali na kukosa uendelevu wa miradi midogo midogo wanayoibuni.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI KWA MKOA WA KUSINI UNGUJA

(i) Kamati **inaigiza**Wizara kusimamia suala la upatikanaji wa Hatimiliki katika maeneo yote ya Serikali ikiwemo majengo, maeneo ya wazi na mashamba ya Serikali.

(ii) Kamati **inashauri** kufuatiliwa na kusimamiwa vyema upatikanaji wa vitendea kazi hasa katika sekta ya kilimo ili kwenda sambamba na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

(iii) Kamati **inashauri** kuimarishwa kwa maendeleo ya elimu katikaa Mkoa huu kwa msingi wa kupatiwa walimu waliobora na wenye uzoefu wa kutosha katika masomo ya sayansi na sayansi jamii pamoja na kupatiwa maktaba za kutosha zenye kuweza kuwasaidia walimu na wanafunzi kwa ujumla.

(iv) Kamati inashauri Mkoa kujitahidi kukabiliana na wanafunzi watoro ambao wanarudisha nyuma maendeleo ya elimu ya Mkoa huu laikini pia na Zanzibar kwa ujumla.

3.4.3 MKOA WA KASKAZINI UNGUJA

Mkoa wa Kaskazini Unguja ni miongoni mwa Mikoa *mitano (5)* ya Zanzibar ambayo inafanya kazi sambamba na malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mkoa huu huratibu shughuli zake kupitia Wilaya ya Kaskazini *"A"* na Kaskazini *"B"* pampja na Wilaya Ndogo ya Tumbatu na Shehia. Vyombo hivi ni muhimili mkuu wa Mkoa huu ambapo husimamia utekelezaji wote wa majukumu ya Serikali ndani ya Mkoa huu.

MAJUKUMU YA MKOA WA KASKAZINI UNGUJA

Mkoa una Majukumu yafuatayo:

(a) Kuratibu, kufuatilia, kusimamia na kutekeleza kazi za Serikali pamoja na shughuli za maendeleo ya Mkoa.

(b) Kuzifanyia marekebisho sheria ndogo ndogo kwa kushirikiana na Taasisi husika.

(c) Kuhakikisha kuwa Sera, Mipango na Maelekezo yote ya Serikali yanatekelewa.
(d) Kusimamia na kuendeleza shughuli zote za usalama wa Mkoa.
(e) Kuhakikisha kuwa rasilimali zote za Mkoa kama vile vifaa na nguvu kazi vinatumika kwa maendeleo ya uchumi na ustawi wa jamii.

CHANGAMOTO ZA MKOA WA KASKAZINI UNGUJA

Mkoa wa Kaskazini Unguja unakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Kutokuwepo kwa ulinzi wa uhakika katika maeneo ya Utalii.
(ii) Uhaba wa fedha na vitendea kazi.
(iii) Kuongezeka na kushamiri kwa vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto.
(iv) Uhaba wa maji safi na salama.
(v) Mwamko mdogo wa wananchi katika kushiriki katika kazi za maendeleo na ujasiriamali.
(vi) Uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi na hisabati katika skuli za msingi na sekondari pamoja na utoro uliokithiri kwa wanafunzi wa Mkoa huu.
(vii) Kushamiri kwa migogoro ya ardhi.
(viii) Wawekezaji na wananchi dhidi ya ajira kwa vijana na wananchi wazawa katika mahoteli.
(ix) Miundombinu mibovu ya barabara pamoja na umeme.
(x) Kuwepo kwa matamasha (*Full Moon*) na vitendo viovu vinavyoambatana na matamasha hayo, ikiwemo vitendo vya ngono na utumiaji wa madawa ya kulevya.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI KWA MKOA WA KASKAZINI UNGUJA

(i) Kamati **inashauri** kuimarishwa kwa ulinzi kwa kuwepo ulinzi wenye uhakika katika sehemu zote ambazo ni vituo na vivutizi vya wageni.
(ii) Kamati **inaagiza** kuchukuliwa hatua kali wale wote wenye kupatikana na hatia za kufanya vitendo vya udhalilishaji.

(iii) Kamati **inashauri** Taasisi zote pamoja na NGO's zinazoshughulikia kupamba na maradhi ya UKIMWI na Kifua Kikuu kuchukua hatua za haraka kuweza kuusaidia Mkoa huu ambao upo katika hali mbaya dhidi ya matatizo haya.

(iv) Kamati kwa mara nyengine tena **inautaka** uongozi wa Mkoa kupiga marufuku Matamasha hayo.

3.4.4 MKOA WA KUSINI PEMBA

Mkoa wa Kusini Pemba ni sehemu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Mkoa umeanzishwa chini ya *Sheria nambari 8 ya mwaka 2014*, Mkoa umeundwa na Wilaya *mbili (2)*za Chake Chake na Mkoani.

Kwa mujibu wa sensa ya watu na maakazi ya mwaka *2012*, Mkoa wa Kusini Pemba una idadi ya watu *195,116*ambapo kati ya hao wanawake ni *101,245* na wanaume ni *93,871*.

HALI HALISI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MKOA WA KUSINI PEMBA

(a) Katika kipindi cha *Oktoba – Disemba, 2017*, Mkoa wa Kusini Pemba umeendelea na utekelezaji wa malengo yaliyomo katika programu zake ikihusisha shughuli za maendeleo katika Mkoa, Ulinzi na Usalama, Mipango na Utawala.

(b) Jumla ya vikao *15* vya Kamati ya Usalama vimefanyika na kujadili masuala ya amani na utulivu, udhibiti wa madawa ya kulevya, matayarisho ya maadhimisho ya miaka *54* ya Mapinduziya Zanzibar, udhalilishaji wa kijinsia, udhibiti wa magendo ya karafuu, mikopo iliyotolewa na shirika la *'ZSTC'* kwa wakulima wa karafuu, maegesho ya magari barabarani, kufuatilia matukio mbalimbali ikiwemo migogoro ya ardhi na ufuatiliaji wa shughuli za mitihani ya darasa la nne, sita, kidato cha II na kidato cha IV.

(c) Jumla ya kesi 29 za udhalilishaji zimeripotiwa na kufuatiliwa, kesi zote hizo ziko Polisi kwa hatua zaidi na kesi moja ya utelekezaji imeshapatiwa suluhu.

(d) Vile vile, kwa upande wa miradi ya maendeleo ya Kisekta, Mkoa umeweza kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimaendeleo, ikiwemo mradi wa ujenzi wa barabara ya Kuyuni –Ngomeni, Chonga – Mgelema na Ole – Kengeja, ujenzi wa kituo cha Afya Ngomeni, Kituo cha Afya Michenzani, Skuli ya Chokocho, Skuli ya Kuukuu Kangani, Skuli ya Minazini, Skuli ya Michenzani, ufugaji wa Samaki Ndagoni na Pujini, Bwawa la kuhifadhia maji Kibokoni, pamoja na vikundi vya ushirika.

(e) Pia, Mkoa katika kuwajengea uwezo watendaji, wafanyakazi *wawili (2)* wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Diploma na Digirii katika vyuo vilivyopo Zanzibar na Tanzania Bara pamoja na kupatiwa stahiki zao zikiwemo likizo, posho baada ya saa za kazi na mshahara.

(f) Vile vile,katika kusimamia na kufuatilia uetekelezaji wa Ugatuzi, Mkoa wa Kusini Pemba unaendelea na utekelezaji wa Ugatuzi kwa Sekta *tatu (3)*. Sekta ya Afya yenye jumla ya vituo *30*, Elimu – Skuli za Msingi *64* na sekta ya Kilimo. Vilevile, zoezi la uandaaji wa Kamati za Mashauriano za Shehia na Mabaraza ya Wadi linaendelea baada ya kupokea muongozo kutoka Wizarani na kutarajiwa kukamilika katika kipindi cha robo ya *nne* ya utekelezaji.

(g) Aidha, katika kuwapatia wazee msaada wa kujikimu kimaisha jumla ya wazee *1,451* wamepatiwa msaada wa *Shilingi za Kitanzania 5,000,* kati ya hao Wilaya ya Chake Chake *1,004* na Wilaya ya Mkoani *447*, kwa upande wa Pencheni Jamii wa *Shilingi za Kitanzania 20,000.* Mkoa wa Kusini Pemba una jumla ya wazee *5,353* ambao wanapatiwa pencheni kwa wakati.

MAFANIKIO KATIKA SEKTA ZA UGATUZI

Kamati imeelezwa kuwa mafanikio makubwa yamepatikana katika kipindi cha *Oktoba – Disemba, 2017* ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa huduma bora kwa wakati.

Aidha, Kamati inayapongeza Mabaraza yote ya Mkoa huu kwa juhudi zao za kuongeza kwa kasi ukusanyaji wa mapato na kuvuka malengo waliyojipangia, hali hii inaonesha wazi kuwa dhana ya Ugatuzi katika visiwa vya Zanzibar inawezekana

cha msingi ni kuhakikisha kuwa wakuu wa Idara na Taasisi zilizochaguliwa kuanza na Ugatuzi waachie madaraka kwa wahusika waliopelekewa Taasisi hizo.

CHANGAMOTO ZA MKOA WA KUSINI PEMBA

Mkoa wa Kusini Pemba unakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Kuwepo kwa mgogoro wa ardhi katika shehia ya Ndagoni Jamvini unaopelekea baadhi ya wananchi kutishiwa usalama wa maisha yao na baadhi ya watu ambao wanajimilikisha eneo la ardhi katikakijiji hicho.
(ii) Uchakavu wa majengo katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Wilaya.
(iii) Kwa upande wa Mabaraza ya Mji mbali na shughuli zinazofanyika,yanakabiliwa na uhaba wa wafanyakazi zaidi katika sekta ya usafi,
(iv) Kwa upande wa Sekta zilizo gatuliwa kuna uhaba wa wafanyakazi, uchakavu wa vituo vya afya na kukosekana kwa vyoo katikaa baadhi ya vituo.
(v) Uhaba wa madarasa na vyoo katika baadhi ya skuli pamoja na upungufu wa walimu.
(vi) Kukosekana kwa walinzi katika vituo vya afya na skuli za msingi.
(vii) Kukosekana kwa hatimiliki kwa vituo vya afya, na
(viii) Uhaba wa walimu wa skuli za msingi kutokana na kundi kubwa la walimu kustaafu kwa kumalizika muda wao wa utumishi kisheria.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI KWA MKOA WA KUSINI PEMBA

(i) Kamati **inaiagiza** Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kuhakikisha kuwa inachukua hatua za haraka kumaliza mgogoro wa ardhi na kuhakikisha kwamba viongozi wa Mkoa, Wilaya au Shehia hawakushiriki katika mgogoro huu kwa hali yoyote ambayo itapelekea wananchi wa Ndagoni kupoteza imani na Serikali yao kupitia mgogoro huu kwa ajili tu ya maslahi ya viongozi hawa au kwa manufaa ya mtu binafsi.

(ii) Kamati **inaishauri**Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini kwa kushirikiana na Wizara hii kufanya utafiti na kujua chanzo cha ongezeko la vitendo vya udhalilishaji katika jamii.

(iii) Mabaraza ya Miji na Halmashauri **yanaagizwa** kuwachukulia hatua watendaji wote ambao si waaminifu katika utendaji wao na zaidi wale wanaohusika na ukusanyaji wa mapato.

(iv) Kamati **inaishauri**Serikali kuanzisha Tume ya Uajiri wa Tawala za Mikoa kama ilivyo kwa tume nyengine kwa kutumia Sheria ile ile iliyotumika kuunda tume kama hizo katika taasisi nyengine ili kudhibiti suala zima la uajiri kwa vile idadi ya waajiriwa iliyopo ni kubwa na ajira nyengine mpya huhitajika kila siku.

(v) Mabaraza **yameshauriwa** kuajiri walinzi katika vituo vya afya na skuli za msingi ili kudhibiti uhalifu na upotevu wa mali za umma, ushauri huu ni kutokana na baadhi ya skuli kuvunjwa na vifaa vya shule hizo kuhujumiwa na watu wasiopenda maendeleo.

(vi) Kamati **inaliagiza** Baraza la Mji Chakechake lijipange na lifanye tathmini juu ya namna ambayo itatumika kuweza kuhakikisha kwamba ujenzi wa soko la Mavambaruku Michakaini unafanikiwa na kuokoa fedha nyingi za umma ili kufikia malengo ya kuanzishwa soko hilo.

(vii) Aidha, Kamati **inaliagiza** Baraza la Mji Chakechake kuhakikisha kuwa linasimamia kwa nguvu zote suala la usafi katika soko la samaki la Machomane kwani hali yausafi hairidhishi na pia kuzuia kutupa taka katika eneo lililopo karibu na kituo cha mafuta kwa vile ni eneo linaloishi watu.

3.4.5 MKOA WA KASKAZINI PEMBA

Mkoa wa Kaskazini Pemba ni moja kati ya miongoni mwa mikoa *mitano (5)* ya Zanzibar ambo una jumla ya watu *211,731* kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka *2012*.

Mkoa wa Kaskazini Pemba una majukumu unatekeleza majukumu yafuatayo: kuratibu, kusimamia na kufuatilia shughuli za Serikali katika

Mkoa, kuhakikisha sera, mipango na maelekezo ya Serikali yanatekelezwa katika Mkoa, kusimamia ulinzi na usalama wa wananchi na kuhakikisha rasilimali za Serikali zinatumika ipasavyo kwa faida ya jamii na maendeleo ya kiuchumi.

Aidha, Mkoa wa Kaskazini Pemba kama ilivyo Mikoa mengine unatumia mpango mfupi wa matumuzi *(MTEF)* kama muundo mkuu wa mipango kwa ajili ya kutekeleza matumizi na majukumu yake.

Mkoa Kaskazini ulisimamia mradi wa Uchimbaji wa mtaro wa maji ya mvua hadi kukamilika kwa asilimia *90* katika Shehia ya Bubujiko jambo ambalo limeleta faraja kubwa kwa wananchi wanaoishi katika shehia hiyo kutokana na janga kubwa la mafuriko lililowakumba mwaka jana katika mvua za masika na kusababisha wananchi wengi kuyakimbia makaazi yao, baada ya maji ya mvua kuharibu mali na makaazi yao, pamoja na mradi wa umeme Shehia ya Fundo.

Pia**,** katika kuweka mazingira mazuri ya Ofisi na Wafanyakazi, Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini imenunua vitendea kazi vya Ofisi ikiwemo fotokopi, kompyuta na viti vya Mkutano na kufanya ukarabati wa majengo ya Ofisi pamoja na kutengeneza vyombo vya Usafiri.

Aidha, Ofisi imefanya juhudi za kuwapatia wafanyakazi wake *36* stahiki zao mbali mbali ikiwemo posho la likizo, malipo baada ya saa za kazi, posho la safari za kikazi na maposho maalum.
Vile vile, katika kuwajengea uwezo wafanyakazi wake Mkoa umewalipia ada ya mafunzo wafanyakazi*wawili (2)* katika ngazi ya Cheti na Diploma katika fani ya Rasilimali watu na 'Computer'.

Aidha, Mkoa ulifanya mikutano na Masheha na watendaji Wakuu wa Sekta mbalimbali kwa kujadili Maendeleo ya Mkoa.

HALI YA VITENDO VYA UDHALILISHAJI KATIKA MKOA WA KASKAZINI PEMBA

Vitendo vya udhalilishwaji wa watoto, wanawake na wazee ni tatizo linaloukabili Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa sasa na imekuwa ni tishio kubwa kwa watoto wetu ambao ndio vijana na wazee wa baadae.

Aidha, katika kukabiliana na tatizo hili, Kamati imeelezwa kuwa juhudi kubwa zinafanyika ikiwa ni pamoja na kuitisha vikao vya kamati ya Usalama pamoja na wadau mbalimbali wakiwemo wazee na Viongozi wa Dini.

Hata hivyo, juhudi nyengine zilizofanyika ni kuwaelimisha wananchi katika Shehia zote *61* ili kuweza kuripoti Matukio ya Udhalilishaji katika vyombo vya sheria mara tu yanapotokea katika maeneo yao, cha kushangaza na jambo la ajabu sana ni kuona baadhi ya wazazi katika Mkoa huu bado wanafumbia macho tatizo hili na kuweza kudiriki kuwaficha watendaji wa makosa haya na kuficha ushahidi na kutokutoa mashirikiano wakati wanapotiwa hatiani katika vyombo vya sheria.
Vilevile, Kamati inaupongeza sana Mkoa huu kwa jitihada zao kubwa za kufuatilia kesi hizo Mahakamani na kuangalia mwenendo wa kesi hizo na kuanzisha kikosi kazi *(Taskforce)* cha kupambana na udhalilishaji katika kila Shehia wakisaidiana na wasaidizi wa kisheria *(Paralegal).*Pia, Mkoa umeanzisha kamati za kupambana na Udhalilishaji katika ngazi ya Shehia.

Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Mkoa huo lipo tatizo la viongozi kuwafukuza kazi watumishi wa Serikali bila kufuata utaratibu unaotakiwa, mfano hai ni Katibu Tawala wa Mkoa huu kumfukuza kazi Sheha wa Shehia ya Chimba kuirifu Wizara kwa uamuzi wake huo.

HALI YA MADAWA YA KULEVYA KATIKA MKOA WA KASKAZINI PEMBA

Kwa kuwa, Madawa ya kulevya ni janga jengine linaloendelea kuukumba Mkoa huu, Zanzibar na Taifa kwa ujumla,na kwa kuwa vijana wetu wanaendelea

kuathirika na madawa hayo siku hadi siku licha ya juhudi kubwa za kuielimisha jamii. Serikali, jamii na jumuia za kiraia *(NGOs)* hazina budi kushirikiana kwa pamoja ili kupunguza au kuikomesha kabisa biashara hiyo haramu ya madawa ya kulevya.

Hivyo, katika kipindi cha miezi *mitatu* iliyopita *(Oktoba – Disemba, 2017),*Kamati imeelezwa kuwa jumla ya watuhumiwa *11* walikamatwa na kesi zao ziliripotiwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria. Kati ya kesi hizo *11*, kesi *tatu (3)* ziko mahakamani, kesi *moja (1)* imeshatolewa hukumu na kesi*saba (7)* ziko katika hatua ya upelelezi.

CHANGAMOTO ZA MKOA WA KASKAZINI PEMBA

Mkoa wa Kaskazinia Pemba unakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Kuwepo kwa elimu ndogo kwa walipa kodi.
(ii) Kushamiri kwa vitendo vya udhalilishaji na ukatili katika jamii.
(iii) Kuendelea kwa vitendo vya ajira za watoto.
(iv) Upungufu wa vitendea kazi katika Mabara na Halmashauri.
(v) Uhaba wa wataalamu wa *'IT'*, Wakandarasi na Maafisa wa Mipango.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(a) Kamati **inaushauri** uongozi wa Mkoa huu kuzisimamia Halmashauri na Mabaraza katika kupambana na ajira za watoto katika maeneo yote yenye vyanzo vya mapato kama vile bandarini na sehemu za kubanja kokoto.
(b) Kamati **inashauri**kutolewa kwa elimu zaidi kwa walipa kodi ili kuboresha kiwango cha ulipaji kodi katika Nchi yetu.
(c) Kamati **inauagiza** uongozi wa Serikali ya Mkoa kuwachukulia hatua wazazi na walezi wote ambao watawaficha wahalifu katika vitendo vya udhalilishaji wa watoto na watu walio katika makundi maalum ili kupunguza kasi ya ongezeko la kesi za udhalilishaji.

(d) Kamati **inaishauri**Wizara kwa kushirikiana na Mkoa pamoja na Baraza la Mji Wete kuendelea kusimamia vyanzo vya mapato bila ya kuwa na umuhali na kuachana na kasumba za baadhi ya watu ambao hawaitakii mema nchi yetu.

(e) Kamati inashauri kwamba ni vizuri viongozi kufuata taratibu katika kushughulikia matatizo ya watumishi wa ngazi za chini ili kulinda haki zao za msingi.

3.5 MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA

Katika ziara iliyofanywa na Kamati katika vipindi tofauti katika Mabaraza na Halmashauri mbalimbali, Kamati imepata fursa ya kushuhudia mambo mbalimbali ambayo yanaleta changamoto katika juhudi za kukuza uchumi na maendeleo ya Nchi. Kamati imebaini kuwepo kwa uhaba wa wafanyakazi, wataalamu pamoja na vitendea kazi katika maeneo yote ya Mabaraza na Halmashauri jambo ambalo ni kikwazo cha maendeleo ya Taasisi hizo.

Aidha, ukusanyaji mdogo wa mapato katika Taasisi hizi pia unachangiwa na uhaba wa wafanyakazi wenye sifa za kutosha katika ukusanyaji wa mapato, hivyo huzorotesha juhudi za Serikali katika kuendeleza mpango wake wa Mfumo wa Ugatuzi.

Vile vile, Taasisi hizi zinakabiliwa na uhaba wa vitendea kazi vya kisasa ambavyo vinauwezo mkubwa wa kufanya kazi na vyenye kuleta ufanisi katika Mabaraza na Halmashauri.

Kwa mnasaba huu, ili kufikia malengo ya DIRA ya*2020* ni lazima Serikali kupitia Taasisi hizi kuwapatia vifaa vya kutosha na vya kisasa vifaa vya kukusanyia mapato na pale ikilazimika, Halmashauri au Manispaa wawe na uwezo wa kununua vifaa vyao wenyewe au kupatiwa miradi ambayo itawasaidia katika kufanikisha malengo yao.

Aidha, ni vyema kwa Taasisi za Serikali zilizopunguziwa majukumu kwenye Ugatuzi kukubaliana na uamuzi huo wa Serikali ii kuleta tija.

Kwa ujumla Kamati inaipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake wa kimaendeleo kupitia Ugatuzi.

3.5.1 BARAZA LA MJI WETE

Baraza la Mji Wete ni miongoni mwa mabaraza *matatu (3)* yaliyopo katika kisiwa cha Pemba. Aidha, Baraza la Mji Wete linaongozwa na Mkurugenzi wa Baraza, Mwenyekiti, na Makamu Mwenyekiti, Madiwani *kumi (10)* wa kuchaguliwa na madiwani*watano (5)* wa kuteuliwa. Baraza lina jumla ya wafanyakazi *101* ambapo wanaume ni *40* na wanawake ni *61*.

MALENGO YA BARAZA LA MJI WETE

Baraza la Mji Wete limejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:

(i) Kuimarisha ukusanyaji wa mapato hadi kufikia*Shilingi za Kitanzania 55,292,750*kupitia kwenye vianzio vyake mbalimbali vya mapato.
(ii) Kuwapatia wafanyakazi Stahiki zao.
(iii) Kufanya usafi wa mazingira na kuweka mipango miji.
(iv) Kuipatia Ofisi huduma za uendeshaji pamoja na vitendea kazi mbalimbali.
(v) Kusaidia shughuli mbalimbali za maendeleo ya jamii.
(vi) Kutoa Elimu na kuhamasisha wananchi kufanya usafi wa mazingira katika maeneo yao.
(vii) Kuelimisha wafanyabiashara juu ya umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari.

UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA BARAZA LA MJI WETE

Katika utekelezaji wa majukumu iliyojipangia, Baraza la Mji Wete limelazimika kuchukua juhudi na mikakati maalum ili kuweza kunyanyua kiwango cha ukusanyaji wa mapato kutoka katika vianzio mbalimbali vya mapato. Aidha, katika

kipindi cha *Oktoba* hadi *Disemba, 2017*, Baraza la Mji Wete limetekeleza malengo yafuatayo:

(a) Baraza limeweza kuwapatia stahiki Waheshimiwa Madiwani *15* pamoja na wafanyakazi wa kutwa sita *(6).*
(b) Baraza limeweza kulipa mishahara kwa wafanyakazi *97* pamoja na kuwasilisha michango ya wafanyakazi wa kudumu katikaMfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF).
(c) Baraza limefanikiwa kuipatia Ofisi huduma muhimu za uendeshaji pamoja na vitendea kazi.
(d) Baraza limeweza kufanya usafi wa mji kwa kuzoa tani *1,800*za taka katika vizimba *(slabs)saba (7)* vilivyomo katika Mji huo.
(e) Baraza limeweza kufanya matengenezo ya ujenzi wa vyoo katika Skuli ya Jadida Msingi.
(f) Baraza limeweza kugharamia safari kwa watendaji wote walioshiriki kwenye vikao mbalimbali vilivyofanyika Unguja.
(g) Katika kusaidia miradi ya kijami, Baraza limesaidia ukarabati wa barabara ya Bubujiko Uchozini kwa kumwaga na kusambaza kifusi.
(h) Baraza limeweza kuwapatia huduma za uji wanafuzi *2927*katika skuli *34* za maandalizi.
(i) Baraza limeweza kulipa nauli kwa walimu *168* na maafisa*watatu (3)* wa elimu kwa Wilaya ya Wete.
(j) Baraza limeweza kuvipatia vifaa tiba vituo *19* vya Afya.

HALI HALISI YA UPATIKANAJI WA MAPATO

Kamati imeridhishwa sana na hali ya upatikanaji wa fedha kwa Baraza la Mji Wete tofauti na vipindi vilivyopita ambapo halijawahi kufikia robo *tatu* ya makusanyo ya makadirio ya Mapato yake. Hivyo, kwa robo ya *pili* ya utekelezaji wa bajeti yameonekana mabadiliko makubwa katika Baraza la Mji Wete ambapo limeweza kupiga hatua nzuri katika ukusanyaji wa Mapato na kuweza kwenda sambamba na Mabaraza ya Chakechake na Mkoani.

CHANGAMOTO ZA BARAZA LA MJI WETE

Baraza la Mji Wete linakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Uelewa mdogo wa wafanyabiashara katika ulipaji kwa ada kwa hiari.
(ii) Uelewa mdogo wa wananchi kuhusu suala la utunzaji wa mazingira.
(iii) Uhaba wa wataalamu kama vile wakandarasi, maafisa 'TEHAMA' na Maafisa Mipango.

MAONI NA MAAGIZO WA KAMATI

(i) Kamati **inalishauri** Baraza kuwahamasisha walipa kodi kulipa kodi kwa hiari.
(ii) Kamati inalishauri Baraza kuhakikisha kuwa linatoa elimu kupitia vyombo vya habari hususani Radio Jamii katika kuielimsha jamii juu ya umuhimu wa kutunza mazingirayanayowazunguka.
(iii) Kamati **inalishauri** Baraza kutafuta wataalamu wenye uwezo wa kufanya kazi pale inapolazimika kufanya hivyo hata kwa njia ya mkataba wa muda mfupi.
(iv) Vile vile, suala la mapato lisiwe la mtu *mmoja (1)* bali iwe ndiyo dhamira na malengo ya kila *mmoja* miongoni mwetu.
(v) Kamati **inaliagiza** Baraza la Mji Wete kusimamia wafanyabiashara katikasuala zima la kutoa risiti za mauzo na kuwahamasisha wananchi kudai risiti kwa ajili ya maendeleo ya Nchi yetu.

3.5.2 BARAZA LA MJI MKOANI

Baraza la Mji Mkoani limeendelea na kutekeleza kazi zake za kawaida kwa mujibu wa mipango na bajeti waliyojipangia.Baraza limeweza kuzitafutia ufumbuzi unaofaachangamoto mbalimbali zinazojitokeza ikiwemo yausimamizi wa ujenzi holela katika Mji.

Aidha, katika kuendeleza usafi wa Mji, Kamati yetu inalipongeza sana Baraza la Mji Mkoani kwani limefanya usafi wa mazingira katika maeneo yote ya Baraza kwa kusafisha Mji, mitaro na kuzoa taka na kuzitupa

katika jaa kuu la Chokaani na kupanda bustani kutoka Ikulu hadi Bandarini na mbele ya Ofisi ya Baraza la Mji.

Jumla ya tani *1,008* zimezolewa pia elimu ya usafi wa mazingira imetolewa katika shehia *saba (7)* kwa vile wanajamii ndio chanzo kikuu cha uharibifu wa mazingira.

*BARAZA LIME*TEKELEZA KAZI ZIFUATAZOKATIKA *SEKTA ZA ELIMU, AFYA NA KILIMO KAZI*

ELIMU YA MSINGI

Baraza kwa upande waSekta yaElimu, limetekeleza na kusimamia mambo yafuatayo:

(i) Utayarishaji wa eneo la ujenzi wa Ofisi ya Elimu Wilaya.
(ii) Uhamasishaji wa uandikishaji wa wanafunzi wapya katikamwaka *2018* ambapo zaidi ya wanafunzi *7,000* wameandikishwa.

AFYA YA MSINGI

Baraza kwa upande waSekta yaAfya, limetekeleza na kusimamia mambo yafuatayo:
(i) Kuandaa mafunzo na mikutano mbalimbali kwa wafanyakazi wa vituoni, *'DHMT'* pamoja na jamii. Jumla ya mikutano*miwili (2)* imefanyika kwa wahudumu *32* wa vituoni kwa muda wa siku*mbili (2)*kuhusiana na huduma ya mama baada ya kujifungua na mfumo wa ukusanyaji taarifa za afya kwa watendaji *34*uliofanyika kwa muda wa siku*tatu (3)*juu ya namna ya kutumia fomu za rikodi na kompyuta.
(ii) Kusambaza na kutoa huduma za chanjo, vifaa tiba na visivyokuwa tiba vijijini na maskulini.
*(iii)*Uwekaji wa samani na vifaa vya usafi katika kituo cha Afya Michenzani ambacho kimefunguliwa katika maadhimisho ya Sherehe za miaka *54* ya Mapinduziya Zanzibar.

SEKTA YA KILIMO

Kwa kuwa Sekta ya Kilimo inajumuisha Mifugo, Uvuvi, Misitu, Kilimo na Umwagiliaji, mambo yafuatayo yametekelezwa:

(i) Jumla ya vikundi*saba (7)* vya ufugaji wa samaki vimepatiwa majembe na mapauro kwa ajili ya uimarishaji wa mabwawa ya samaki.
(ii) Baraza limefanya uhamasishaji wa kupeleka mifugo kwenya josho la wanyama Mjimbini ambapo Shehia *kumi (10)* zilihusishwa.

Aidha, Kamati inapongeza Baraza la Mji Mkoani kwa kuvuka malengo ya makusanyo ndani ya kipindi cha *Oktoba – Disemba, 2017*, hali hii inaonesha jinsi juhudi zao nzuri wanazozitekeleza katika kusimamia ukusanyaji wa mapato kama ilivyoonekana katika Baraza la Mji Wete.

Miongoni mwa hatua zilizosaidia ongezeko hili la makusanyo ni pamoja na kusainiwa kwa Kanuni mpya za Serikali za Mitaa ambazo zimekuja na mabadiliko makubwa ya Ada na utekelezaji wake umeanza katika kipindi cha ukusanyaji wa mapato.
Aidha, Kamati inampongeza sana Mkurugenzi wa Baraza la Mji Mkoani kwa ubunifu wake mzuri na uongozi wenye tija kwa Baraza lake.

MAFANIKIO KATIKA SEKTA ZA UGATUZI

Upatikanaji wa huduma mbalimbali kwa wakati kulikotokana na usimamizi mzuri wa viongozi wake katika kufanikisha dhana ya Mfumo wa Ugatuzi.

CHANGAMOTO ZA BARAZA LA MJI MKOANI

Baraza la Mji Mkoani linakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Uhaba wa wafanyakazi zaidi katika sekta ya usafi.

(ii) Aidha, kwa upande wa sekta zilizogatuliwa, nazo zinakabiliwa na uhaba wa wafanyakazi.
(iii) Uchakavu wa vituo vya afya na kukosekana kwa vyoo katika baadhi ya vituo.
(iv) Uhaba wa madarasa na vyoo katika baadhi ya skuli pamoja na upungufu wa walimu.
(v) Kukosekana kwa walinzi katika vituo vya afya na skuli.
(vi) Kukosekana kwa hatimiliki za vituo vya afya.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI KWA BARAZA LA MJI MKOANI

(i) Kamati **inashauri** Baraza la Mji Mkoani kupatiwa wafanyakazi na wataalamu kama njia moja ya kuongeza ufanisi katika kazi zake.
(ii) Kamati **inalishauri** Baraza la Mji Mkoani kufanya juhudi za makusudi za kuvifanyia matengenezo vyoo viliopo katika vituo vya afya ambavyo hali zake haziridhishi pamoja na kujenga vyoo vipya katika maeneo ambayo hayana vyoo kwa ajili ya matumizi ya kawaida.
(iii) Kamati **inaishauri** Serikali kupitia Mamlaka ya Serikali za Mikoa kuajiriwa walinzi ambao watatumika kulinda katika skuli na vituo vya afya ili kudhibiti uharibifu na wizi wa rasilimali ziliopo katika vituo hivyo.
(iv) Kamati **inaiagiza** Mamlaka ya Serikali za Mitaa kufuatilia upatikanaji wa Hatimiliki za skuli na vituo vya afya pamoja na maeneo yote yanayomilikiwa na Mabaraza na Halmashauri.
(v) Kamati **inaliagiza** Baraza la Mji Mkoani kusimamia wafanyabiashara katika suala zima la kutoa risiti za mauzo na wananchi kuhamasishwa kudai risiti kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu.

3.5.3 BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE

Baraza la Mji Chake Chake limeendelea kufanya kazi zake mbalimbali ambazo limepanga kuzitekeleza katika mwaka huu wa fedha*2017/2018*. Katika utekelezaji wa malengo hayo Baraza limekwenda sambamba na matakwa ya mfumo wa Ugatuzi kwani limezingatia mahitaji ya taasisi zote ambazo zimegatuliwa na ziliopo chini ya mwamvuli wa Wizara hii.

SEKTA YA ELIMU YA MSINGI

(a) Huduma ya nauli kwa Walimu na uji kwa wanafunzi wa skuli *29* imetolewa.
(b) Walimu *130* wamepatiwa nauli na wanafunzi *1,338* wamepatiwa huduma ya uji.
(c) Jumla ya skuli *29* na Ofisi ya Elimu Wilaya zimepatiwa huduma za uendeshaji na vifaa.

AFYA YA MSINGI

Kamati imeelezwa kuwa katika sekta ya afya mambo mbali mbali yamefanyika ikiwa ni pamoja na kuendeleza utoaji wa chanjo za magonjwa mabli mbali kwa watoto na mama wajawazito pamoja na kutolewa elimu ya afya.

SEKTA YA KILIMO

(a) Jumla ya miti *32,250* imekuzwa ikiwemo Mikarafuu *20,000* na *12,250* miti ya matunda.
(b) Kazi za ufuatiliaji zimefanyika ikiwa ni pamoja na kukatisha leseni za uvuvi, kusimamia uchaguzi wa kamati ya uvuvi Kilindi, kufanya doria katika eneo la *'PECCA'* Wilaya ya Chake, uchukuaji wa takwimu mbalimbali zinazohusiana na maendeleo ya uvuvi.
(c) Kusaidia shughuli za ufugaji wa samaki kwa kuwapatia vifaa na upatikanaji wa mbegu. Roli *moja (1)* ya mpira kwa ajili ya bwawa la Ushirika wa Bora Uhai Mkumbuu imenunuliwa.
(d) Kukuza upatikanaji wa huduma katika vituo vya huduma kwa wakulima na huduma za uendeshaji pamoja na elimu kwa wakulima imetolewa.

CHANGAMOTO ZA BARAZA LA MJI CHAKECHAKE

Baraza la Mji Chake Chake linakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Uhaba wa wafanyakazi katika sekta ya usafi.
(ii) Uhaba wa wataalamu katika fani za ukandarasi na '*IT*'.
(iii) Uelewa mdogo wa wananchi juu ya ulipaji wa kodi.
(iv) Ukosefu wa walinzi katika vituo vya afya na skuli za Serikali.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(i) Kamati **inalishauri** Baraza la Mji ChakeChake kusimamia ukusanyaji wa mapato bila ya muhali na kuwachukulia hatua stahiki wafanyabiashara wote wenye kukwepa kulipa kodi.

(ii) Kamati **inalishauri** Baraza la Mji Chake Chake kuajiri watu/wataalamu katika kada zinazokabiliwa na upungufu kwa njia ya Mkataba wa muda mfupi hata kwa gharama zao wenyewe badala ya kusubiri ajira rasmi kutoka Serikalini.

(iii) Baraza **limeshauriwa** kuendelea kutoa elimu kwa walipa kodi ili kuweza kufikia lengo na dhamira ya Serikali katika kuihamasisha jamii kulipa kodi kwa hiari kwa ajili ya maendeleo ya Nchi yetu.

(iv) Kamati **inaliagiza** Baraza la Mji ChakeChake kulitumia jaa liliopo Vitongoji kwa kutupa taka na liacheutaratibu wa kukusanya taka katika maeneo yasiyorasmi.

(v) Baraza **limeagizwa** kuhakikisha kuwa linaweka makontena ya kukusanyia taka katika maeneo yenye msongomano wa watu ili kuepusha kuzagaa kwa taka kiholela katika Mji, kwani Mji huu ndio kioo cha kisiwa cha Pemba.

(vi) Kamati **inaliagiza** Baraza la Mji Chake Chake kusimamia vyema wafanyabiashara katika suala la kutoa risiti za mauzo na wananchi wawashajihishe kudai risiti kwa maendeleo ya Nchi yetu.

(vii) Sambamba na hayo, Kamati **inaliagiza** Baraza la Mji ChakeChake kuliendeleza soko la Michakaini (Mava Mbaruku) ambalo limeshatumia fedha nyingi za jamii lakini bado limeshindwa kukamilika na kufanya kazi iliyokusudiwa.

3.5.4 WILAYA YA KATI UNGUJA

Kamati ilipokea taarifa ya Ofisi ya Wilaya ya Kati Unguja katika utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha *April – June, 2017* pamoja kufanya ukaguzi wa jengo jipya la Wilaya ya Kati Unguja.

Kamati imeelezwa kuwepo kwa mwendelezo wa vitendo vya udhalilishaji katika Wilaya hii licha ya juhudi kubwa zinazochukuliwa. Wananchi wanaoishi katika Wilaya hii wamepata mwamko mkubwa katika kushirikiana na vyombo vya sheria katika kutoa ushahidi wa kesi za udhalilishaji.

Kwa upande wa jengo jipya la Wilaya, Kamati imebaini kwambalipo katika hali ya kuridhisha licha yakukabiliwa na uhaba wa fedha kutokana na kutegemea zaidi fedha 'OC' na wahisani.

Wilaya inakabiliwa na uwepo wa bandari zisizo rasmi zaidi katika maeneo ya Uzi na Bungi. Hata hivyo, Wilaya inaandaa mpango maalum wa kujenga *'De touch'* katika maeneo ya kuingilia Uzi.

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WILAYA YA KATI

Wilaya ya kati inakabiliwa na changamoto kuu zifuatazo:

(a) Ukosefu wa usafiri kwa Ofisi hii ambapo Afisa Tawala wa Wilaya hutumia vespa jambo ambalo ni changamoto kubwa katika kipindi cha mvua. Vilevile, mheshimiwa Mkuu wa Wilaya anaazimwa gari kutoka Tume ya Uchaguzi.
(b) Tatizo la maafisa wa kisekta kutumia fedha za bajeti ya Wilaya.
(c) Kuwepo tatizo kubwa la uuzwaji mashamba ya eka kiholela na bila kuzingatia wanunuzi wa mashamba hayo ni wenyeji au wageni ndani ya Nchi yetu.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(i) Kamati **inaishauri** Serikalikuirasimisha bandari ya Uzi ili iweze kudhibiti biashara za magendo katika eneo hilo.

(ii) Kamaati**inaishauri**Serikali kutilia nguvu utekelezaji wa sheria zinazohusiana na kupambana na magendo na uhujumu wa uchumi ili kukabiliana na vitendo vya Magendo na uhujumu uchumi nchini.

(iii) Kamati **inauagiza** uongozi wa Wilaya kusimamia vyema vyanzo vya mapato katika Halmashauri yake na vilevile kuweza kuviainisha vyanzo hivyo pamoja na mapato yake katika kila chanzo *kimoja (1).*

(iv) Kamati **inaishauri** Serikali kuweka mfumo *mmoja (1)* wa utoaji wa Hati za Ardhi ili kudhibiti maeneo yetu pamoja na kuepusha vitendo visivyo vyakizalendodhidi ya nchi yetu.

(v) Kamati **inaishauri**Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuzitaka Serikali za Mitaa kuhakikisha wageni wote wanaoingia katika Wilaya hii na nyenginezo kuwa ni lazima wafike na barua za uthibitisho wa wanakotoka.

(vi) Kamati **inaishauri** Wilaya kusimamia kikamilifu vyanzo vya mapato katika Halmashauriyake.

(vii) Kamati **inaiagiza**Wilaya hii kusimamia kikamilifu suala la usafi wa mazingira ili kujikinga na maradhi ya mripuko ambayo hutokea baadhi ya wakati katika nchi yetu.

3.5.5 WILAYA NDOGO TUMBATU

Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Wilaya Ndogo ya Tumbatu kwa kipindi cha *Aprili – June, 2017* na kuelezwa mambo mbalimbali yanayotekelezwa katika Wilaya hii.

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WILAYA NDOGO TUMBATU

Wilaya ndogo ya tumbatu inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Ukosefu wa wafanyakazi wa kisekta na hata pale wanapohitajika kwa dharura basi huchukua muda mrefu kufika na kushiriki katika jambo mahususi.

(ii) Kuwepo kwa shughuli za uvuvi haramu katika Wilaya hii na ukosefu wa vifaa vya kisasa vya kuvulia, jambo linalowafanya kushindwa kufika katika bahari kuu.

(iii) Katika Wilaya hii ipo Redio Jamii ambayo hutumika kuwaelimisha wana jamii ya Tumbatu na maeneo ya jirani ila changamoto inayoikabili ni uhaba wa mafundi mitambo, ukosefu wa jengo la ofisi na mwamko mdogo wa jamii.

(iv) Uwepo wa wanyama waharibifu wa mazao kama vile kima na wadudu wanaoharibu mahindi na mazao mengine ya nafaka. Hata hivyo, Wilaya kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imekuwa ikijitahidi katika kupambana na kadhia hii lakini mpaka sasa bado tatizo hili linaendelea kuathiri kwa kiasi kikubwa juhudi za wakulima wa mahindi na nafaka.

(v) Kuwepo kwa athari za kupasuka kwa mabomba ya maji mara kwa mara na kupelekea maji mengi kupotea kutokana na mabomba mabovu na yaliyo chini ya kiwango.

(vi) Kuwepo kwa mwamko mdogo wa wanajamii kujisajili katika vizazi na vifo hivyo kufanya wakaazi wengi wa eneo hili kushindwa kupata vyeti vya kuzaliwa na vifo.

(vii) kuwepo kwa mgogoro wa ardhi ambapo jitihada nyingi zimeshachukuliwa ikiwa ni pamoja na viongozi wa Serikali kuingilia kati lakini bado hamasa ya wananchi ni kubwa ya kutaka kulimiki eneo hilo kwa kila upande.

(viii) Kuwepo wa kesi za udhalilishaji ila ni kwa kiwango cha chini.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(i) Kamati **inaishauri** Redio Jamii iliyopo kisiwani Tumbatu itumike kwa kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na uhifadhi wa mazingira na usalama wa usafiri wa vyombo vya Baharini.

(ii) Kamati **inaushauri** uongozi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa kushirikiana Mamlaka ya Maji Zanzibar kulishuhulikia tatizo la uvujaji wa mabomba ya

maji kwa wakati ili kuzuia upotevu wa maji ambayo ni rasilimali muhimu katika jamii na nchi kwa ujumla.

(iii) Kamati **inaishauri** Serikali kufanya mazungumzo juu ya umuhimu wa kujenga kituo kidogo cha Polisi katika Wilaya hii kwani tayari Wilaya imeshatenga eneo la ujenzi huo.

(iv) Kamati **inaishauri** Serikali kulitaifisha eneo ambalo limekuwa likigombaniwa kwa muda mrefu kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiserikali tu ili kuepusha mgogoro uliodumu na unaoendelea kwa muda mrefu.

(v) Kamati **inaushauri**uongozi wa Mkoa na wataalamu wa fani mbalimbali kutembelea kisiwa hiki mara kwa mara ili kuweza kuibua changamoto zilizopo na kuweza kuwasaidia kwa wakati wananchi wa kisiwa hiki.

(vi) Kamati **inaishauri**Wilaya kuelekeza nguvu zaidi katika kupambana na kesi zinazohusiana na udhalilishaji kwani waathirika zaidi wa kesi hizo ni watoto.

3.5.6 ZIARA YA KAMATI KATIKA MANISPAA YA DODOMA KATIKA WIZARA YA OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi ilifanya ziara katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa *(TAMISEMI)* katika Manispaa ya Dodoma ambapo lengo kuu la ziara hii ni kupata uelewa juu ya dhana nzima ya Mfumo wa Ugatuzi kwa Wajumbe wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum.

Kamati ilipata maelezo juu ya majukumu ya msingi ya Mfumo wa Ugatuzi kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – TAMISEMI na kuelezwa hali halisi ya Ugatuzi ilivyo katika Halmashauri zote za Tanzania Bara pamoja na changamoto zake katika uendeshaji.

MAMBO YALIYOIBULIWA NA KAMATI KATIKA ZIARA HII

(i) Lengo kuu la Ugatuzi ni kurudisha Madaraka kwa wananchi, hivyo wananchi wanatakiwa watoe mawazo yao juu ya jambo/mradi wanaotaka katika jamii yao.

(ii) Ugatuzi unataka maamuzi yote yatoke kwa wananchi wenyewe na Serikali itekeleze tu maamuzi ya jamii katika mradi waliouchagua na kuongeza ufanisi na kusimamia matumizi bora ya rasilimali zilizopo katika Halmshauri au kijiji husika.

(iii) Mapato ya kuendeshea kazi hizo *(miradi iliyochaguliwa na jamii)*yatatoka katika makusanyo ya Halmashauri zao kwa mujibu wa vyanzo vyao vya mapato.

(iv) Changamoto kubwa ya mfumo huu wa madaraka ni bajeti katika utekelezaji na ukamilishaji wa malengo yaliyopangwa.

(v) Miradi ya wananchi ambayo wameichagua itekelezwe kwa kuangalia matakwa yao wenyewe kutokana na kipaumbele cha mradi huo kwa wananchi wenyewe.

(vi) Mfumo huu wa madaraka kwa wananchi una faida kubwa kwa wananchi na Serikali kwa ujumla kutokana na kutekelezwa kwa miradi waliyoichagua wenyewe, hivyo huwapa hamasa ya usimamizi na uendeshaji wakati ambao Serikali jukumu lake ni kusimamia utekelezaji wa mradi huo.

(vii) Uendeshaji wa mfumo huu ni lazima wizara za kisekta kujikita katika sera, kanuni na taratibu za wizara na kiutendaji iachie TAMISEMI kwani hawa ndio wahusika wakuu wa utendaji.

(viii) Ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri ni vyema kutumia mifumo ya kielektroniki, njia hii itasaidia kuongezeka kwa mapato, kupunguza kwa kiasi kikubwa upotevu wa fedha za Serikali, kupatikana uwazi na uwajibikaji pamoja na kulipa kodi kiurahisi na kwa wakati.

CHANGAMOTO ZINAZOUKABILI MFUMO WA UGATUZI WA MADARAKA

(i) Bajeti katika Halmashauri ndio kikwazo kikuu kinachorudisha nyuma maendeleo ya Ugatuzi.

(ii) Baadhi ya sekta kung'ang'ania madaraka na Rasilimali kunapelekea kushuka kwa kasi ya Serikali kujikita moja kwa moja katika Ugatuzi jambo ambao linaathiri maendeleo ya wananchi.

(iii) Ugatuzi hafifu wa kifedha na tatizo la fedha za ruzuku kutoka Serikali kuu kutotoka kwa wakati na kama ilivyopangwa kutolewa.

(iv) Tatizo la muundo wa madaraka kutegemea sekta tofauti kama vile miundombinu, ardhi, elimu na afya.

(v) Tatizo la rasilimali watu na uhaba wa vitendea kazi.

(vi) Malalamiko ya wananchi juu ya dhana ya utawala bora.

USHAURI WA KAMATI KWA WIZARA NA SERIKALI

(i) Kamati **inazishauri** wizara za kisekta zikubali kutoa madaraka kwa wananchi.

(ii) Kamati**inaishauri** Wizara kuwatumia vizuri Masheha ili waweze kutoa taarifa za matatizo na miradi ya wananchi wao.

(iii) Kamati **inaishauri** Serikali kwa lengo lakwenda sambamba na mabadiliko haya wawakilishi wa wananchi lazima washirikishwe katika vikao vyote vya jimbo kuhusu maendeleo ya jimbo husika.

(iv) Kamati **inazishauri**manispaa, mabaraza na halmashauri kuweka uhusiano mzuri wa kifedha katika kusimamia miradi ya maendeleo.

(v) Kamati **inashauri** katika kufanikisha azma ya Serikali ni lazima kuwepo kwa dhamira, uthubutu na malengo yaliyobora.

(vi) Kamati**inaishauri** Serikali katika kuimarisha ukusanyaji wa kodi ambao ndio kitu cha msingi katika kufikia malengo ni lazima tuhakikishe tumepata vifaa vya kutosha na vya kisasa katika kukusanyia kodi.

(vii) Kamati **inaishauri** Serikalikuweka mashirikiano mema na yenye kuleta ufanisi katika pande zote *mbili (2)* za Muungano katika sekta mbalimbali za kimaendeleo ikiwemo suala la Ugatuzi.

(viii) Kamati **inaishauri** Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuandaa mfumo maalum ambao utawadhibiti wanaokwepa kulipa kodi bila ya kuleta athari kwa Serikali kuu na jamii kwa ujumla.

(ix) Kamati inaishauri Serikali Kuu kutorudi nyuma katika utaratibu wa Ugatuzi.

3.6 IDARA MAALUM ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum katikakutekeleza majukumu yake, ilitembelea vikosi vyote *vitano (5)* vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambavyo ni: Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo, Jeshi la Kujenga Uchumi, Idara ya Chuo cha Mafunzo, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi na Kikosi cha Valantia Zanzibar kwa upande wa Unguja na Pemba na kujionea shughuli mbalimbali za kizalendo na kuleta maendeleo ndani ya Nchi yetu.

Hivyo, Kamati inapongeza sana juhudi zinazofanywa na wapiganaji wetu wa vikosi hivi kwa kazi nzito wanazozifanya za kulinda, kusimamia na kudumisha usalama wa raia na mali zao pamoja na kuhakikisha kuwepo kwa amani na utulivu katika Nchi yetu.

Sambamba na hayo, Kamati imeridhishwa kwa kiasi kikubwa kutokana na hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa Mahanga ya Askari kisiwani Pemba,juhudi hizo za Serikali zinaonekana kutia moyo kuona kuwa Serikali inawajali na kuwathamini vijana wetu na vilevile, Serikali kutekeleza kwa vitendo ahadi zake zilizotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka jana.

CHANGAMOTO ZINAZOZIKABILI IDARA ZA SMZ

Licha ya hayo, Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum katika ziara zake imeweza kubaini changamoto mbali mbali zinazorudisha nyuma maendeleo ya Idara hizi kama ifuatavyo:

(i) Ukosefu wa vitendea kazi ambavyo havikidhi haja ya askari wa vikosi hususanikatikaIdara amabazo zinajihusisha moja kwa moja na uzalishaji wa kilimo na shughuli nyengine za maendeleo.

(ii) Uhaba wa sare *(uniform)* za askari ambapo katika baadhi ya vikosi, hufikia hatua ya askari kuazimana sare.

(iii) Vile vile, licha ya juhudi kubwa kufanyika na kwa kisi fulani mafanikio kuonekana lakini bado ukosefu wa Hatimiliki na zaidi kwa upande wa Idara ya Mafunzo na JKU.

(iv) Ukosefu wa wataalamu katika vikosi hivi kwa ajili ya kuendesha shughuli mbalimbali za kitaalamu. Kwa mfano uhaba wa wataalamu katika fani za IT (*Information System)* na wakandarasi (*Engineering*).

(v) Kutotumika kwa Sheria inayohusiana na Utumishi wa Idara Maalum katika kuaandaa maslahi ya wastaafu wa Idara Maalum na kinyume chake kutumika sheria, kanuni na miongozo ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *(ZSSF)* katika kuandaa maslahi ya wastaafu hao jambo ambalo limekuwa ni changamoto kwa askari wa vikosi kwa vile wao wako nje ya huduma za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

(vi) Vituo vya afya vilivyo chini ya vikosi kutokupatiwa dawa na vifaa kutoka Wizara ya Afya licha ya vituo hivyo kuhudumia idadi kubwa ya wananchi, hali hii inapelekea vituo hivyo kukabiliwa na mzigo mzito wa kutoa huduma za afya na kutokufikia lengo la Serikali la kuipunguzia idadi kubwa ya wagonjwa katika Hospitali kuu ya Mnazi Mmoja.

3.6.1 KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO(KMKM)

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kina jukumu la kuhakikisha kuwa kinazuia usafirishaji wa mali yoyote ambayo imezuiwa kisheria kusafirishwa baharini na nchi kavu kwa namna yoyote kutoka nje ya mipaka ya Zanzibar.

Kamati inapongeza juhudi za Kikosi hiki kwa jinsi kinavyoisaidia Serikali na jamii katika kutoa huduma bora za afya kwa hospitali yake ya Kibweni pamoja vituo vyake mbalimbali katika kambi zake ziliopo Unguja na Pemba.

Katika kuhakikisha kuwa Kikosi kinatekeleza majukumu yake ipasavyo, Kamati ya Sheria na Utawala Bora na Idara Maalum ilifanya ziara maalum ya kutembelea kambi mbalimbali Unguja na Pemba kwa lengo la kujionea namna wanavyotekeleza majukumu yao pamoja na kubaini

changamoto mbalimbali zinazowakabili katika uendeshaji wa shughuli zao.

CHANGAMOTO ZINAZOKIKABILI KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO

Kikosi cha Kuzuia Magendo kinakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Uhaba wa mahanga ya kupumzikia wapiganaji pamoja na ukosefu wa vifaa vya kulalia na zaidi kwa wapiganaji wa kike.
(ii) Ukosefu wa Hatimiliki katika maeneo wanayotumia kwa shughuli zao za kiulinzi.
(iii) Ukosefu wa huduma za afya kwa baadhi kambi za mashamba.
(iv) Uhaba wa mahanga na nyumba za kulala maafisa wa KMKM kwa Unguja na Pemba.
(v) Ukosefu wa maji safi na salama katika baadhi ya kambi.
(vi) Kuendelea kwa mmung'unyuko wa ardhi katika ukanda wa Maruhubi na maeneo yote ya bahari katika makao makuu ya Kikosi hiki huko Kibweni.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(i) Kamati **inaiagiza** KMKM kuendelea kufuatilia upatikanaji wa Hatimiliki katika kambi zote ambazo bado hawajamiliki maeneo yake kisheria.
(ii) Kamati **inaishauri**Serikali kuchukuliwa jitahada zaidi ili kuziboresha kambi zenye Rada kwa ajili ya kupatikana kwa Rada za kisasa.
(iii) Kamati **inaishauri** Serikali kuandaa mpango maalum wa kujenga Chelezo kwa ajili ya matumizi ya vyombo vya baharini vya KMKM. Mpango huo utasaidia vyombo vya hivyokufanyiwa matengenezona KMKM yenyewe badala ya kupelekwa Mombasa.
(iv) Kamati **inaishauri** Serikali kuangalia uwezekano wa kuwa na *'jeti'* ndogo kwa ajili ya vyombo vya KMKM.

(v) KMKM **imeagizwa** kuzingatia umuhimu wa kuwa na mafuta ya kutosha kwa ajili ya vyombo vyake vya usafiri wa baharini wakati wa kuandaa bajeti yake ya mwaka wa fedha *2018/2019*.

(vi) Kamati **inaiagiza** KMKM kuandaa waraka maalum na kuuwasilisha Serikalini kwa ajili ya kuomba msaada wa ujenzi wa ukuta katika fukwe kwa ajili ya kudhibiti mmung'onyoko wa ardhi katika maeneo ya Maruhubi upande wa baharini.

KIKOSI CHA KMKM MASINGINI

Kamati ilitembelea na kukaguwa Kituo cha KMKM Masingini na kujionea shughuli mbalimbali ambazo zinatekelezwa katika majukumu yao ya kila siku.

Kambi hii inakadiriwa kuwa na ukubwa wa eneo lenye wastani wa ekari tatu (3) kwa upande wa Kaskazini na Kusini kuna kuta za makaazi ya raia, upande wa Mashariki kuna barabara na upande wa Magharibi kuna bonde ambalo wananchi wa kawaida wanalitumia kwa kazi za kilimo.

Kituo hiki kinahusika zaidi na ulinzi kwa kutumia Rada ambayo kwa muda mrefu sasa haifanyikazi sambamba ya Rada ya Kituo cha Sengenya Pemba.

Kituo cha Masingini kimekuwa kikishiriki katika ulinzi wa aina mbili ambao ni ulinzi wa ndani ya kambi na ulinzi wa nje katika sehemu ya mitambo ya mnara wa kurushia matangazo wa Shirika la Utangazaji la Zanzibar *(ZBC)*.

CHANGAMOTO ZINAZOKIKABILI KITUO CHA KMKM – MASINGINI

Kituo cha KMKM, Masingini kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinarudisha nyuma malengo ya kituo hiki kama vile:

(i) Kuwepo kwa uchakavu wa majengo.

(ii) Ukosefu wa uzio katika eneo la kambi ambapo inapelekea eneo lao kuvamiwa na wananchi wanaoishi jirani na kambi kwa shughuli mbalimbali zikiwemo za makazi na kilimo.

(iii) Kuwepo kwa changamoto kwa askari wanaolinda sehemu ya mnara wa ZBC kutokana na ukosefu wa kibanda cha walinzi pamoja na ukosefu wa vifaa vya kukabiliana na moto *(fire extinguisher)* wakati inapotokea dharura ya moto.

(iv) Kuwepo kwa mionzi mikali inayotokana na mitambo ya kurushia matangazo ambayo hupelekea kupata matatizo ya kiafya kutokana na athari za mionzi hiyo.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(a) Kamati **inaishauri**Wizara kuwapatia walinzi wanaolinda eneo la mnara wa kurushia Matangazohuduma stahiki kulingana na shughuli na mazingiza wanayokabiliana nao kama vile posho ya maziwa ili kuimarisha afya zao.

(b) Kamati inaishauri Wizara kuandaa utaratibu wa kukipatia kikosi cha Masingini eneo la bonde lilopo upande wa Magharibi kwa vile linamilikiwa na Serikali ili waweze kuimarisha shughuli zao za ulinzi na usalama.

KIKOSI CHA KMKM – MARUMBI

Kamati ilitembelea na kupokea taarifa ya Kituo cha KMKM Marumbi na kujionea shughuli zao mbalimbali ambazo wanazitekeleza katika majukumu yao ya kila siku. Aidha, Kamati imewataka wapiganaji kujituma kwa moyo wao wote katika kujenga misingi iliyobora katika kazi na kusimamia amani na utulivu uliopo katika nchi.

CHANGAMOTO YA KIKOSI CHA KMKM – MARUMBI

Kikosi cha KMKM Marumbi kinakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Uhaba wa maji safi na salama katika eneo la kambi.

(ii) Uhaba wa vyombo vya doria katika ukanda huu wa mashariki jambo linalopelekea kutumia boti za mradi wa Huba ya Menai.

(iii) Ukanda huu unakabiliwa na kiwango kikubwa cha uvuvi haramu pamoja na biashara za magendo ya bidhaa za chakula kutoka Tanzania Bara.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(i) Kamati **inazishauri** taasisi zinazohusika kuwachukulia hatua kali wafanyabiashara wanaokamatwa kuhusiana na kesi za magendo pamoja na kutaifishwa kwa vyombo vyao ili kukomesha vitendo hivyo na kulinda uchumi wa nchi yetu**.**

(ii) Kamati **inauagiza** uongozi wa KMKM kuhakikisha kuwa wanapeleka huduma za maji safi na salama katika kituo hiki kwani ikiwa tatizo lipo katika upatikanaji wa maji ya ZAWA basi ni vyema wakachimba kisima chao wenyewe ambacho kitasaidia kwa matumizi yao lakini pia na jamii inayowazunguka.

KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM) UNGUJA UKUU

Kamati ilitembelea na kujionea utendeji wa kazi mbalimbali katikakambi hii huku wakipambana na mazingira magumu katika utekelezaji wao wa majukumu ya kila siku.

CHANGAMOTO ZA KMKM UNGUJA UKUU

Kambi ya KMKM Unguja Ukuu inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Utowaji wa huduma za afya haukidhi mahitaji hasa ukizingatia kuwa mpaka wananchi wanaoishi karibu na eneo hili hutumia kituo hiki kwa ajili ya kupata huduma za kiafya.

(ii) Ukosefu wa madawa ambapo kamati imeelezwa kuwa kwa mara ya mwisho katika kituo hiki dawa zilipatikana katika bajeti ya *2016/2017*.

(iii) Kuwepo kwa ukosefu wa mahanga ya Askari.

(iv) Kuwepo kwa ukosefu mkubwa wa jengo la ofisi ambapo askari hulazimika kulala humo humo kwenye jengo la ofisi.

(v) Ukosefu wa vifaa vya kulalia kwa askari wanaohitaji kupumzika muda wa usiku.

(vi) Ukosefu wa usafiri na hivyo Kituo hulazimika kutumia vyombo vya kuazima kwa ajili ya kuzuru maeneo ya pwani.

(vii) Kuongezeka kwa biashara za magendo na uhujumu uchumi.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(i) Kamati **inashauri** kuboreshwa kwa huduma za afya katika kituo hiki cha Unguja Ukuu kwa kukamilisha ujenzi wa jengo la kituo cha afya ambao unakwenda kwa kusuasua.

(ii) Kamati **inashauri** kupatiwa madawa ya kutosha katika kituo hiki na kwa wakati kama ilivyo katika vituo vyengine.

(iii) Kamati **inashauri** wakati utakapofika kwa kujengwa mahanga ya askari hapa Unguja, basi kituo hiki kipewe kipaumbele kwani hali ilivyo sasa ni mbaya na inawakwaza askari wetu.

(iv) Kamati **inaoumba** uongozi wa KMKM kufikiria kwa kina suala la umuhimu wa vifaa vya kulalia na zaidi kwa askari wa kike kwani katika kituo hiki hakuna kabisa eneo lilitengwa kwa ajili ya askari wa kike.

(v) Kamati **inaishauri** Wizara kuchukua juhudi za makusudi kulipatiaufumbuzi suala la usafiri katika vituo vya Idara Maalum kwani limekuwa ni tatizo sugu kwa wapiganaji wetu kwa Idara zote Unguja na Pemba.

(vi) Kamati **inaishauri** Serikali kupitia Taasisi zinazopambana na uhujumu uchumi kusimamia kikamilifu sheria zinazopinga suala hili pamoja na kuendelea kuwachakulia hatua kali wale wanaojihusisha na biashara za magendo.

3.6.2 IDARA YA CHUO CHA MAFUNZO

Chuo cha Mafunzo ni miongoni mwa IdaraMaalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo ipo chini wa mwavuli wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Idara hii ina jukumu la kuwapokea wale wote wanaopelekwa

Chuo cha Mafunzo kwa mujibu wa sheria, kuwalinda pamoja na kuwarekebisha tabia ili wanaporejea katika jamii wawe raia wema. Urekebishaji wa tabia hizo unajumuisha fani mbalimbali zikiwemo kazi za mikono, ujenzi, ushoni, ufundi magari, ufundi kuchonga pamoja na huduma za ushauri nasaha.

CHANGAMOTO ZINAZOKIKABILI CHUO CHA MAFUNZO ZANZIBAR

Chuo cha Mafunzo kinakabiliwa na changamoto zifuatazo katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku:

(i) Ukosefu wa Hatimiliki za maeneo ya Kambi pamoja na mashamba wanayoyatumia kwa ajili ya kilimo ikiwemo kambi ya Tungamaa kisiwani Pemba.

(ii) Ukosefu wa usafiri wa uhakika katika kambi nyingi zikiwemo: Ubago, Kengeja na Kangagani.

(iii) Ukosefu wa huduma za afya za uhakika katika kambi za Kengeja, Kangagani na Tungamaa.

(iv) Uchakavu wa majengo ya ofisi, ubovu wa nyumba za kuishi askari pamoja na uchakavu wa jela za wanafunzi. Licha ya Serikali kuanzisha mradi mkubwa wa ujenzi wa Mahanga na nyumba za maafisa katika baadhi ya kambi kisiwani Pemba lakini bado ipo haja ya kuendelezwa kwa mradi huu katika kambi zote za Unguja na Pemba.

(v) Ufinyu wa Bajeti na fedha za matumizi mengineyo katika Idara ya Chuo cha Mafunzo ambako kunapelekea kushindwa kuendesha miradi yake iliyojipangia.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(i) Kamati **inashauri** suala la utafutaji wa Hatimiliki lisiwachiwe Idara ya Chuo cha Mafunzo peke yake bali liwe ni mkakati wa Serikali kuhakikisha kuwa kambi zote zinapatiwa Hatimiliki kwa upande wa Unguja na Pemba.

(ii) Kamati **inashauri**kuangaliwa kwa jicho la mbalisuala la usafiri ili kuboresha utendaji kwa askari wetu pamoja na kuwafanya watekeleze majukumu yao ipasavyo.

(iii) Kamati inapongeza sana ujenzi wa Mahanga na Nyumba za Maafisa katika kituo cha Tungamaa na Kamati ina imani kuwa ujenzi huu utaleta mazingira mazuri katika kambi nyengine.

(iv) Kamati **inashauri** kuboreshwa kwa fungu la Bajeti la Chuo cha Mafunzo ikiwa ni pamoja nakuingizwa kwa wakati.

CHUO CHA MAFUNZO KINUMOSHI

Kamati ilitembelea Chuo cha Mafunzo Kinumoshi na kujionea shughuli zao mbalimbali za kimaendeleo ambapo imeridhishwa na huduma wanazopatiwa wanafunzi waliopo katika kituo hiki na kuwataka askari kuendelea kuwasimamia na kuwafundisha wanafunzi maadili mema ili watakapotoka wawe wamejifunza maadili mema na kuacha kutenda maovu waliyokuwa wakitenda hapo awali.

Kamati inatoa pongezikwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kikosi hii kwa juhudi zao mbalimbali wanazozichukuwa katika kukabiliana na changamoto zinazowakabili.

CHANGAMOTO ZINAZOKIKABILI CHUO CHA MAFUNZO KINUMOSHI

Chuo cha mafunzo Kinumoshi kinakabiliwa na changamoto kuu zifuatazo:

(i) Uwepowa madeni ambayo Chuo kinadai katika taasisi mbalimbali za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

(ii) Kutokulipwa kwa posho la kujikimu kwa askari wanaopata uhamisho kutoka Unguja kwenda Pemba au kutoka Pemba kuja Unguja.

(iii) Kutomalizika kwa ujenzi wa barabara ya Kizimbani hadi Miwani, kunaleta usumbufu kwa Maafisa na Wanafunzi wa Chuo hicho.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(i) Kamati **inaishauri** Idara ya Chuo cha Mafunzo ilete mabadiliko katika sekta ya kilimo kwa kufuatilia mashamba yake ya uzalishaji ili kusaidia kukuza uchumi wa nchi yetu.

(ii) Kamati **inaishauri**Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na uongozi wa Idara ya Mafunzo Zanzibar kuzitembelea kambi zote za Idara ya Chuo cha Mafunzo Unguja na Pemba na kujionea changamoto zinazowakabili katika suala zima la Mahanga ya askari, Kamati ina imani kuwa ziara hii itasaidia sana wakati watakapokaa kuandaa Bajeti ya Idara hii kuwaangalia kwa umakini na kulipa umuhimu suala la makazi ya askari wetu.

(iii) Kamati **inaishauri** Idara ya Chuo cha Mafunzo kupitia wakandarasi wake kujipanga kutafuta usajili wa kampuni yao ya ujenzi, hii itaweza kuwasaidia kupata zabuni za ujenzi katika vikosi vya SMZ lakini pia, kupunguza gharama za ujenzi katika vituo hivyo.

(iv) Kamati **inaishauri**Wizara kuiomba Mamlaka ya Maji Zanzibar kwamba wanapochimba visima vyao katika maeneo ya mashamba ya Chuo cha Mafunzo wawapatie fursa ya kutumia visima hivyo katika kilimo cha umwagiliaji na vilevile, wanapojenga uzio katika maeneo ya visima hivyo wazingatie utaratibu maalum kwa kuangalia umuhimu na ukubwa eneo husika.

3.6.3 IDARA YA JESHI LA KUJENGA UCHUMI ZANZIBAR

Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) ni miongoni mwa Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Jeshi la Kujenga Uchumi limeanzishwa kupitia ibara ya *121(2)* ya Katiba ya Zanzibar chini ya *Sheria ya Jeshi la Kujenga Uchumi, nambari 6 ya mwaka 2003*. Kupitia Sheria hii, JKU imepewa jukumu la kutoa mafunzo kwa vijana katika nyanja za uzalishaji wa kilimo, mifugo na uvuvi. Vilevile, kuwafunza vijana katika fani ya ufundi, kazi za amali na

uzalendo ili kuwafanya vijana hao waweze kujitegemea na waweze kuitumikia na kujenga nchi yetu.

Dira ya JKU ni kuratibu, kusimamia na kuendesha mafunzo endelevu hivyo basi kupitia JKU vijana wa Zanzibar waweze kujengeka kiuzalendo, kujitegemea na kujiamini.

Dhamira ya JKU ni kuchangia kuimarisha uchumi kwa kutoa mafunzo ya uzalishaji, ufundi na kazi za amali, mila na utamaduni na uzalendo.

Kamati inapongeza sana juhudi za JKU Zanzibar kwa kuendeleza miradi mbalimbali ya kimaendeleo, miradi ambayo kwa kiasi kikubwa huwasaidia askari wetu lakini pia jamii hufaidika kutokana upatikanaji nzuri wa huduma zao.

CHANGAMOTO ZA IDARA YA JKU ZANZIBAR

Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar linakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(a) **Uchache na uchakavu wa miundombinu**

(i) Miundumbinu na hasa ya majengo katika jeshi hili haipo katika hali ya kuridhisha na kutosheleza mahitaji yake. Hii ni kutokana na kutokutumika kwa muda mrefu kwa miundombinu hiyo kwa sababu ya ukosefu wa vijana wa kulala makambini mfano nzuri ni kikosi chaUpenja**.**

(ii) Kambi nyingizimekosa majengo ya kuweka vijana na matumizi mengine kwa mfano Kikosi cha Chambani kisiwani Pemba.

(iii) Kwa upande wa miundombinu ya maji na umemeila hatua zilizofikiwa zinatia moyo kwani Vikosi na Kambi zote za JKU ziliopo kisiwani Unguja zimeshafikiwa na huduma ya maji na umeme na kwa Pemba ni Kambi *tatu (3)* tu (Pujini, Mwambe, Kwapeza) ndizo ambazo hazijafikiwa na huduma ya umeme ambapo mipango inakaribia kukamilika kufikisha huduma hiyo.

(b) **Upungufu wa Vitendea kazi**

Kati ya mafunzo wanayopatiwa vijana ni ya ufundi na uzalishaji kwa nadharia na vitendo. Pamoja na juhudi zinazofanywa, Skuli ya Ufundi Mtoni inaendelea kutumia vifaa chakavu na vya kizamani hivyo mafunzo ambayo hutolewa kwa vitendo yanayoendana na wakati yanashindikana kutolewa kwa ufanisi.

(c) **Kukatishwa tamaa vijana juu ya upatikanaji wa ajira**

Kutokana na umuhimu wa sekta ya ulinzi, agizo la Serikali ni kwamba ajira za Vikosi vya ulinzi na usalama ipitie Jeshi la Kujenga Taifa *(JKT)* kwa Tanzania Bara au Jeshi la Kujenga Uchumi kwa Zanzibar. Agizo hili huwa tofauti kidogo pale inapotokea fursa za ajira kwa Idara Maalum na Jeshi la Wananchi la Tanzania *(JWTZ)* kwa upande wa Zanzibar. Vijana ambao tayari wameshahitimu mafunzo yao katika Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar hukosa ajira hiyo pale zinapotokea.

(d) **Uhaba wa vifaa na wafanyakazi** katika Hospitali ya JKU Saateni ambako kunachangiwa na ufinyu na ukomo wa bajeti ya JKU.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

Kamati **inaishauri** Serikali, Uongozi na wapiganaji wa JKU Zanzibar wafanye juhudi za makusudi ili kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili ikiwa ni pamoja na:

(i) Kuimarisha miundombinu kwa kukarabati na kujenga majengo mapya likiwemo jengo la Makao Makuu ya JKU ambapo kwa sasa wanatumia majengo yasiyokidhi mahitaji na hasa kwa kuzingatia historia ya jeshi hili. Aidha, hatua hizo zichukuliwe katika Vikosi na Kambi za kila Zoni kwa kutumia bajeti ya Serikali na mapato ya ndani ili kuongeza uwezo wa kusajili na kuwahudumia vijana ipasavyo.

(ii) Kamati **inashauri** kushughulikiwa kwa haraka upelekaji wa huduma ya umeme katikakambi ambazo bado huduma hiimuhimu kwa matumizi ya binaadamu haijafika.

(iii) Kamati **inaishauri** Wizara kushajihisha Taasisi za Serikali na hasa za Ulinzi na Usalama kutoa kipaumbele kwa vijana waliopo au waliopitia JKU wakati wanapotangaza nafasi za ajira, hii itaamsha ari na hamasa kwa vijana kujiunga na JKU.

(iv) Kamati **inaishauri** JKU kuendelea kubuni vianzio vipya vya mapato na kuvitumia vyema vile viliopo kwani ni miongoni mwa njia zitakazosaidia kupunguza changamoto ya fedha za uendeshaji wa miradi na kazi mbalimbali.

(v) Wizara kwa kushirikiana na uongozi wa JKU **wafuatilie** upatikanaji wa Hatimiliki za kambi na vikosi vyote vya Zanzibar.

(vi) Kamati **imeishauri** JKU kuhakikisha kuwa kilimo bora na cha kisasa cha *'Green House'*kinaendelezwa ambacho kitasaidia JKU katika sekta hii kwa kuongezeka kwauzalishaji na hivyo kuweza kushindana kikamilifu katika soko la kilimo na kukidhi mahitaji ya chakula nchini.

(vii) JKU **imeshauriwa** kuwa wakati inapopata fursa ya kuajiri, kipaumbele kiwekwe kwa kuajiri walimu wenye sifa zinazolingana na mahitaji yao ili kuboresha zaidi sekta ya elimu katika skuli ya Sekondari ya JKU iliopo Mtoni.

(viii) Kamati **imeshauri**nguvu zaidi za Serikali zinahitajika kwa lengo la kuboresha sekta ya afya katika Makao Makuu ya JKU Saateni kwani Hospitali hiiinajitahidi vya kutosha kutoa huduma za afya kwa askari na raia wanaoishi katika maeneo ya karibu.

(ix) Kutokana na kukua na ukubwa wa Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar, Kamati **inaishauri** Serikali kupitia Uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi kuanzisha utaratibu maalum wa kupewa nambari kwa kambi zote kama ilivyo kwa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ).

JESHI LA KUJENGA UCHUMI BAMBI MATOLA NA BAMBI 'KIM'

Jeshi la Kujenga Uchumi(JKU)lilikabidhiwa shamba la Matola kutoka Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi mwaka 2003. Shamba hili lina ukubwa wa ekari *585* na linauwezo wa kustawisha mazao ya aina mbalimbali ikiwemo mboga mboga.

Kamati yetu inapongeza sana juhudi za Jeshi hii kwa kuanzisha kilimo cha **'Green House'** katika sehemu *tatu (3)* tofauti ambazo zinatumika kwa kuatikia miche na vilevile mazao ya viungo.

Kamati imetembelea ujenzi wa bwalo la Askari ambalo bado halijakamilika na linategemewa litakapokamilika litakuwa na uwezo mkubwa wakuchukuwa vijana wa ujitolea.

CHANGAMOTO ZINAZOLIKABILI JKU BAMBI MATOLA NA JKU BAMBI 'KIM'

(i) Mabadiliko ya hali ya hewa yanayotokana na madiliko ya Tabia Nchi ambayo huathiri mazao.
(ii) Kuharibika kwa mazao kutokana na wadudu pamoja na kuibuka kwa maradhi mbalimbali yanayoharibu mazao hayo.
(iii) Kutokuwepo kwa sokola uhakika kwa mazao ya mbogamboga ambalo pia linaathiri juhudi za wakulima hawa katika kambi ya JKU Matola.
(iv) Ukosefu wa mafunzo ya kitaalamu kutoka nje ya nchi katika sekta zote zilizomo ndani ya jeshi.
(v) Kamati imeridhishwa na mpango wa JKU kuchimba kisima katika eneo ambalo linatumiwa kwa kilimo cha umwagiliaji ili kuepusha kutegemea mvua za msimu kama ilivyoeleka kwa wakukima wengi wa Zanzibar.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(i) Kamati **inauagiza** uongozi wa JKU Bambi Matola na Bambi 'Kim' kufuatilia kwa kikamilifu suala la upatikanaji wa Hatimiliki za mashamba yote wanayotumia ili kuepusha kuvamiwa na wananchi.

(ii) Kamati **inaishauri** JKU Matola kuanzisha kilimo cha viungo *(spices)* ambacho kitawapatia soko la uhakika kutokana na umuhimu wake katika jamii.

(iii) Kamati inashauri kuboreshwa kwa sekta ya maji na miundombinu ya barabara katika eneo lote la kambi hii.

(iv) Aidha, Kamati **inashauri** kupitiwa upya malengo ya mradi huu na kama malengo hayajafikiwa kwa kiwango kikubwa basi Serikali iandae utaratibu mwengine wa kuliendeleza shamba hili la Bambi 'Kim'.

(v) Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kusaidia juhudi za JKU katika kukuza sekta ya kilimo kwa kuwapatia wataalamu na washauri mbalimbali wa kilimo na mifugo ambao ni changamoto kubwa kwao ili kuendeleza sekta ya kilimo nchini, pamoja na kuwasaidia katika miundombinu ya Kilimo.

KIKOSI CHA JKU MACHUI

Kamati ilitembelea na kupokea taarifa ya Jeshi la Kujenga Uchumi katika kambi ya Machui ambapo changamoto mbalimbali zinazowakabili katika utekelezaji wa majukumu yao zilielezwa.

Katika ziara hii, Kamati imegundua kuwa Kambi hii ndio pekee ambayo imebahatika kuwa na kilimo cha mikarafuu kwa Unguja na Pemba. Jumla ya *Shilingi za Kitanzania* 7,000,000.00 zimekusanywa kutoka uchumaji wa karafuu ambapo fedha hizo zimeingizwa katika mapato ya Jeshi.

Pamoja na kilimo cha mikarafuu, Kambi hii pia inajishughulisha na kilimo cha mbogamboga na viungo mbalimbali pamoja na kuatika miche kwa ajili ya kilimo.

CHANGAMOTO ZINAZOKIKABILI KIKOSI CHA JKU MACHUI

(a) Ukosefu wa usafiri.

(b) Ukosefu wa bweni la kupumzikia askari wanawake jambo ambalo huleta usumbufu kwa askari hao wakati wa usiku na wanapohitaji kupumzika.

(c) Uhaba wa upatikanaji wa vifuko kwa ajili ya kuoteshea miche ambapo hurudisha nyuma juhudi za kuendeleza kilimo, hali hii imetokana na marufuku ya manispaa katika uingizwaji wa mifuko ya plastiki.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(a) Kamati **inawashauri** wapiganaji na maafisa wa kituo hiki kufanya kazi kwa bidii na moyo wa kujitolea.

(b) Aidha, suala la usafiri linahitaji kushughulikiwa kwani imekuwa ni changamoto kuu juu ya Idara zote za JKU.

(c) Kamati **inaushauri** uongozi wa JKU kutafuta njia mbadala itakayosaidia au kurahisisha uatikaji wa miche bila ya kutumia vifuko vya plastiki.

KIKOSI CHA JKU – KAMA

Kikosi cha JKU Kama kina ukubwa wa eneo lenye hekta za mraba *127.5* eneo ambalo wamepewa kisheria na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na hatimiliki za eneo hilo.

Kambi ya JKU Kama inajishughulisha na kazi kuu *tatu (3)* ambazo ni: kilimo cha mazao mchanganyiko, kilimo cha mifugo ya kuku na ng'ombe pamoja na shughuli za ulinzi.

Aidha, kikosi hiki kinajishughulisha pia na uzalishaji mali kwa njia ya biashara ambayo inahusisha mradi wa Matofali na mradi wa duka.

Vile vile, mapato yote yanayotokana na miradi hii ya biashara pamoja na ile ya uzalishaji wa kuku na ng'ombe hutumika kwa ajili ya uendeshaji wa kambi na vilevile mapato mengine huingia Serikalini.

Pia, kikosi hiki kimepanga kununua gari *moja (1)* kwa njia ya mkopo ili kupunguza tatizo la usafiri katika kambi hii. Aidha, kikosi kinaendelea na ujenzi wa Rest House hatua ambayo inaleta matumaini makubwa kwa kikosi hicho.

Kamati imeridhishwa sana na utendaji wa kikosi hiki pamoja na kujitolea kwao kwa lengo la kuimarisha maendeleo na usalama wa nchi yetu.

CHANGAMOTO ZA JKU KAMA

Kikosi cha JKU Kama kinakabiliwa na changamoto tofauti ambazo zinachangia kutokamilika kwa malengo wanayojipangia, miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo:

(i) Ufinyu wa bajeti ya JKU ambao unaathiri miradi na malengo mbalimbali ambayo wamejipangia.
(ii) Kupanda mara kwa mara kwa bei za chakula cha mifugo hususan chakula cha kuku.
(iii) Ugumu wa upatikanaji wa kuku mama *(breeder)* ambapo hupelekea kutoongezeka kwa idadi ya kuku kwa muda mrefu.
(iv) Kuibuka kwa migogoro ya ardhi na wananchi wananchi wanaozinguka katika maeneo ya kambi hiyo.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(i) Kamati **inaishauri** Serikali kuboresha upatikanaji wa bajeti yenye kulingana na malengo yaliyopangwa kufikiwa.
(ii) Aidha, Kamati **inashauri** kuimarishwa kwa miundombinu ambayo itakuwa rafiki na mazingira ya uzalishaji ikiwa ni pamoja na kusimamiwa na kutafutiwa ufumbuzi changamoto ya kupanda mara kwa mara bidhaa za chakula cha mifugo ya kuku na ng'ombe.
(iii) Vile vile, Kamati **inaishauri** jamii kuepuka migogoro isiyo ya lazima kwa lengo la kujimilikisha maeneo ya ardhi ambayo yanamilikiwa ni jeshi hilo kihalali na kisheria.

(iv) Kamati **inaishauri** Serikali na Makao Makuu ya JKU kusaidia kukamilika kwa ujenzi wa *'Rest House'* iliyopo kambini hapo kwa lengo la kwenda sambamba na malengo yao ya kupunguza changamoto ya makazi kwa maafisa wa kikosi.

3.6.4 KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU)

Kikosi cha Zimamoto na Uokozi ni miongoni mwa Idara Maalum za SMZ chini ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ. Idara hii imeanzishwa chini ya Sheria nambari 7 ya mwaka 1999 na inajukumu la kuzima moto na uokoaji wa maisha na mali za watu, kusimamia na kuhakikisha kuwa huduma za zimamoto na uokozi katika viwanja vya ndege na bandari zinakwenda sambamba kwa mashariti ya kitaifa na kimataifa. Aidha, kikosi kinatoa elimu ya zimamoto na uokozi kwa wananchi na Taasisi za Serikali pamoja na Taasisi binafsi juu ya kinga na hadhari za moto.

Miongoni mwa mambo ya msingi ambayo yamekuwa ni changamoto kwa KZU Uwanja wa Ndege ni pamoja na ukosefu wa maji kwa ajili ya kuendeshea shughuli zao mbalimbali ikiwemo za kimafunzo.

Katika eneo lenye kituo kipya lipo hodhi ambalo limewahi kutolewa ahadi na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kutakiwa kuwekewa miundombinu bora ili kutoa huduma za maji kwa kikosi, kinyume chake ahadi hiyo haikutekelezwa na mpaka kufikia wakati huuhodhi hilo halina miundombinu ya umeme.

Kamati inatoapongezi zake za dhati juu ya juhudi zinazochukuliwa na kikosi hiki katika kuhakikisha kuwa elimu ya kujikinga na moto na uokozi inaifikia jamii. Hivyo, jumla ya vipindi *vitatu (3)* vimerushwa katika televisheni na *12* kwa njia redio pamoja na mafunzo kwa Taasisi *15* za Serikali na Taasisi *33* za watu binafsi yametolewa.

MAFANIKIO YA KIKOSI CHA KZU

Licha ya changamoto kadhaa ambazo zinawakabili, kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar kimefanikiwa sana katika:

(i) kuimarisha huduma za zima moto na uokozi Mijini na Vijini;
(ii) kuimarisha huduma za zima moto na uokozi katika viwanja vya Ndege;
(iii) kupatikana kwa Hatimiliki katika maeneo yanayomilikiwa na KZU;
(iv) kuendelea na ujenzi wa kituo cha Zima moto Marumbi ambachi kitaanza kutumika hivi karibuni;
(v) kupata msaada kwa baadhi ya vifaa vya uokozi kutoka Serikali ya Ujerumani;
(vi) kutowa mafunzo kwa maafisa na wapiganaji, katika utumiaji wa vifaa vya uokozi na uokozi majini ambapo jumla ya wapiganaji 50 waliopatiwa mafunzo hayo tayari wanatoa buduma katika bandari za Malindi na Mkoani kwa Pemba;
(vii) Mafunzo ya udereva ngazi ya C1 kwa wapiganaji 36 yametolewa;
(viii) Kupatikana kwa gari ya usafiri kwa wapiganaji; pamoja na
(ix) Kupatikana kwa boti ya kisasa ya uokozi ambayo itawasili nchini hivi karibuni.

CHANGAMOTO ZA KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU)

(i) Kukosekana kwa eneo la kuegeshea *(parking)* ya magari katika kituo kidogo *(cha zamani)*cha uwanja wa ndege, jambo linalopelekea gari zao kuharibika kwa kupigwa ni vumbi, mvua najua kwa muda mrefu.
(ii) Kuwepo kwa ujenzi holela usiozingatia taratibu za ujenzi na uokozi. Hii inatokana na kutokushirikishwa kwa Kikosi cha Zimamoto na taasisi zetu zinazohusika na majenzi katika mpango wa ujenzi na hivyo kujenga bila kuzingatia taratibu zinazotakiwa.
(iii) Ukosefu wa visima vya kuchukulia maji pamoja uchavu wa miundombinu ya maji *(Fire Hydrant)* kwenye maeneo mbalimbali ya mijini Unguja na Pemba. Hili husababisha tatizo ambalo linahitaji kushughulikiwa kwa haraka katika kukabiliana na ajali za moto.

(iv) Kutokuwepo kwa huduma za maji katika kituo kipya cha Zimamoto Uwanja wa Ndege jambo linalopelekea kushindwa kufanya baadhi ya shughuli zao.

(v) Kutokupatiwa mgao wa makusanyo ya kifungu cha *safety fee* ambapo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wamepewa ruhusa ya kutumia fedha hizo.

(vi) Kukosekana kwa mafunzo ya zimamoto kutokana na uhaba wa fedha.

(vii) Vilevile, suala la uhaba na uchakavu wa majengo ni miongoni mwa changamoto zinazoikabili KZU kwa upande wa Unguja na Pemba.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(i) Kamati **inaishauri** kuangaliwa vyema suala la nyongeza katika ukomo wa bajeti kwani kwasasa ni ndogo na haikidhi mahitaji katika kutekeleza majukumu yake. Hii itasaidia Serikali kuacha kuingiza fungu maalum kila ifikapo katikati ya bajeti kutokana na kumalizika kwa fedha za matumizi kwa kikosi hiki.

(ii) Kamati **inaishauri** Serikali kuendeleza mpango wake wa kujenga vituo vya Zimamoto na Uokozi ambao ulipangwa kujengwa kituo *kimoja (1)*katika kila Wilaya.

(iii) Aidha, Kamati **inaishauri** Serikali kuchukua juhudi za makusudi ya kukipatia kikosi vifaa vya zimamoto kulingana na mazingira wanayofanyia kazi.

(iv) Kamati **inaigiza** Shirika la Bandari kusaidia upatikanaji wa vifaa vya zimamoto na uokozi kwa vikosi vya Bandarini angalau kuwapatia vifaa vya huduma ya mwanzo *(first aid kit)* na mafuta.

(v) Kamati *inaziagiza* Taasisi zinazosimamia huduma za fedha na zile za ujenzi kushirikiana kikamilifu na KZU kwa lengo la kuboresha kazi zao na kufikia malengo yanayokusudiwa.

(vi) Kamati **inashauri** Taasisi na wawekezaji wanaowekeza katika miradi mikubwa ya kimaendeleo kusaidia katika ujenzi wa vituo na kutoa vifaa vya zimamoto na uokozi katika maeneo ya karibu na miradi yao.

(vii) Kamati **inaishauri** KZU kutanua wigo wa urafiki na nchi zilizoendelea katika masuala ya uokozi wa majanga mbalimbali ya moto na ajali za baharini.

(viii) Kamati inasahuri wizara ya Nchi OR - Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ pamoja na wizara ya Ujenzi, Usafirishajina

Mawasiliano, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, pamoja na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege **wakae kwa pamoja** ili kutafuta muafaka wa mambo yafuatayo; ujenzi wa sehemu ya parking kwa gari za zimamoto Airport, ukamilishaji wa miundombinu ya maji katika kituo kipya cha Airport pamoja na kuweka kizuizi maalum cha kukinga vumbi katika jengo la kituo ili kuzinusuru gari mpya za Zimamoto kuharibika kwa vumbi. Pia kutafuta muafaka mzuri wa kuwapatia Zimamoto sehemu ya fedha za *safety fee* ili kikosi hicho kiweze kuboresha huduma zake.

3.6.5 KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR (KVZ)

Kikosi cha Valantia ni miongoni mwa Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Jukumu la KVZ ni kuweka amani na utulivu katika nchi; kupambana na janga lolote litakaloikumba jamii; kulinda viongozi na mali za Serikali na kufanya kazi za kijeshi kwa lengo la kulinda hali inayohatarisha usalama wa Taifa.

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI KVZ

(i) Kamati imeelezwa kuwa, Kikosi kinakabiliwa na ufinyu wa ukomo wa bajeti usiokidhi mahitaji na kushindwa kutekeleza mipango yake kama inavyojipangia.

(ii) Ukosefu wa mahanga ya askari na maafisa wao katika vituo mbalimbali kama vile Kambi ya Ndugukitu na Pujini Kisiwani Pemba.

(iii) Ukosefu wa barabara zenye kukidhi mahitaji kwa vikosi vya Valantia kwa kambi zote za Mashamba.

(iv) Uchakavu na uhaba wa vyombo vya usafiri Unguja na Pemba.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(a) Kamati **inaishauri** Serikali kuboresha miundombinu ya barabara zinazokwenda Kambini katika vituo vyote ambavyo vinakabiliwa na hali mbaya katika sekta ya barabara.

(b) Kamati **inaishauri** Serikali kusaidia upatikanaji wa usafiri kwa jeshi hili angalau gari *moja (1)*kwa kila kambi hususan zile kambi Kuu.

(c) Aidha, katika mradi wa ujenzi wa nyumba za maafisa na mahanga ya askari awamu ya *pili (2)* ambao unatarajiwa kuanza baada ya kukamilika kwa awamu hii; Kamati **inashauri** kuangaliwa kwa kina hali halisi ya makazi ya jeshi hili kwani nao wapo katika hali mbaya na yenye kuzorotesha maendeleo yao.

KIWANDA CHA KUTENGENEZEA VIATU CHA KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR (KVZ) MTONI

Kamati ilifanikiwa kutembelea na kukaguwa Kiwanda cha kutengenezea viatu cha KVZ Mtoni pamoja na kujionea ujenzi unaoendelea wa jengo jipya la Kiwanda hicho lililopo ndani ya makao makuu Mtoni.

Kamati imeelezwa kuwa KVZ kinaendelea kuimarisha mradi wake wa kiwanda cha kutengenezea viatu na wamekusudia mradi huu kukamilika ndani ya miaka *mitano (5)* kuanzia mwaka wa fedha *2016/17* hadi *2020/2021*. Mradi umetengewa jumla ya *Shilingi za Kitanzania 5,395,000,000.00*. Katika mwaka wa fedha *2017/2018* mradi umeidhinishiwa *Shilingi za Kitanzania 400,000,000.00* kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake mbalimbali. Shughuli hizo ni kama vile: kuendelea na ujenzi wa jengo la kiwanda, kukipatia kiwanda vifaa vya alama za usalama, kushiriki katika maonesho ya Biashara ya Kimataifa na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya maendeleo ya mradi.

Kamati imeona kuwa, kwa sasa mradi wa jengo la kiwanda cha viatu upo katika hatua ya uwekaji wa taizi na upakaji wa rangi ambapo bado juhudi zaidi zinahitajika za kumsimamia mkandarasi kukamilisha mradi huu.

CHANGAMOTO ZINAZOUKABILI UJENZI

(a) Kuongezeka kwa gharama za ujenzi iliyosababishwa ni umbile baya la ardhi iliyojitokeza katika hatua za mwisho za ujenzi huo. Hivyo, jumla ya *Shilingi za Kitanzania 48,000,000.00* zimeombwa kwa ajili ya kukabiliana na changamoto hii katika kuboresha kuta za jengo hili kwa upande wa nyuma.

(b) Aidha, Kamati haikurishwa na ongezeko hili la gharama kwa kuwa mkataba wao haukuonyesha gharama za ziada endapo itajitokeza na kwa vile fedha zote zimeshalipwa tokea mapema.

(c) Kamati imelezwa kuwa gharama zote za kampuni inayosimamia ujenzi wa mradi huu zimeshalipwa tokea mwanzoni mwa ujenzi jambo ambalo halipendezi kwa mkadarasi kulipwa gharama zote mapema bila ya kukamilika kwa mradi.

(d) Uhaba wa wataalamu wa kuendesha kiwanda hiki wakati kitakapokamilika kwa vile kitakuwa cha kisasa na chenye mashine za kisasa zinazohitaji utaalamu zaidi.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(a) Kamati **inashauri** katika kuandaa mradi mkubwa kama huu ambao unatarajiwa kutumia fedha nyingi za umma basi ni lazima ufanywe utafiti mapema tena kwa mashirikiano na mkandarasi wa Serikali ili kuepusha gharama ambazo zitajitokeza baadae na kubebeshwa mzigo Serikali.

(b) Aidha, Kamati **inashauri** wakati kufungwa mikataba mikubwa kama hii ya ujenzi ambayo itatumia fedha nyingi za umma, basi ni vyema mikataba hiyo kuanzia hatua za awali ikashirikishwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali badala ya kufungwa mikataba hiyo kimazoea na kusababisha hasara kwa Serikali.

KIWANDA CHA USHONI CHA IDARA MAALUM ZA SMZ

Kamati imetembelea Kiwanda cha Ushoni cha Idara Maalum kiliopo katika maeneo ya Amani na kujionea mambo mbalimbali ambayo yanatekelewa kiwandani hapo.

CHANGAMOTO ZINAZOKIKABILI KIWANDA CHA USHONI

Pamoja na mambo mengine, Kamati imeelezwa kuwepo kwa changamoto zifuatazo ambazo zinahitaji kutatuliwa kwa haraka ili kiwanda kiweze kufikia malengo kilichojiwekea:

(i) Uhaba wa vifaa vya kisasa vyenye uwezo wa kufanyakazi kwa ufanisi zaidi. Hii inasababisha kukinyima uwezo wa kuzalisha kwa wingi na kwa muda mfupi kiwanda hiki.

(ii) Kutokana na kuwepo kwa mtaji mdogo wa kuendeshea kiwanda hiki,kumekisababishia kiwanda kukabiliwa na uhaba wa fedha jambo ambalo linarudisha nyuma jitihada zao za uzalishaji.

(iii) Vile vile, Kiwanda kinadaiwa na"*ZIPA*" deni la *Shilingi za Kitanzania 150,000,000* hivyo, kuufanya uongozi wa kiwanda hiki kuwa na imani ndogo ya kuendelea kuwepo katika jengo wanalotumia kwa sasa.

(iv) Baadhi ya Taasisi zinapopeleka kazi za kushonewa sare zao huchelewa kufanya malipo au kuchelewa kuchukua nguo hizo kwa muda mrefu jambo linapelekea usumbufu mkubwa kutokana na uhaba wa ofisi.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

(a) Kamati **inaishauri** Idara Maalum na Taasisi za Serikali kukitumia kiwanda hiki kwa lengo la kusaidia kuimarika kwa maendeleo ya kiwanda.

(b) Serikali ni vyema iwapatie mtaji wa kutosha ili kuweza kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazowakabili.

(c) Vile vile, kuhusiana na deni la kodi ya jengo ambalo kiwanda kinadaiwa na"*ZIPA*", Kamati**inaishauri**Serikali isaidie kuhakikisha kuwa deni hilo linasamehewa kwa vile taasisi hizi zote *mbili (2)* ni za Serikali na zinafanya kazi kwa kuisaidia Serikali.

UJENZI WA NYUMBA ZA MAAFISA NA MAHANGA YA WAPIGANAJI KWA IDARA MAALUM ZA SMZ PEMBA

Idara ya Chuo cha Mafunzo imebahatika kuwa miongoni mwa Idara Maalum zilizotengewa fedha kwa ajili ya mradi mkubwa wa ujenzi wa nyumba za kuishi maafisa na wapiganaji katika kambi ya Chuo cha Mafunzo Tungamaa na Kengeja.

Aidha, Idara nyengine ambayo imebahatika katika mradi huu ni Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo katika Kambi ya Likoni – Kojani.

Kamati imeridhishwa na inapongeza sana juhudi za Serikali kwa kuwajali wapiganaji wetu hawa ambapo kwa sasa ujenzi huu umeanza katika kituo cha Tungamaa na tayari nyumba *tatu (3)*za Maafisa na Bweni *moja (1)* la wapiganaji pamoja na kibanda cha walinzi cha kisasa zipo katika hatua ya kuezekwa.
Mradi huu unaratibiwa na Makao Makuu Zanzibar na Kamati yetu inaamini kuwa mradi huu utafanikiwa kwa kiwangokikubwa kama vile ulivyokusudiwa.

Baada ya kukamilika kwa mradi huu, Kamati inaamini kuwa tatizo la makaazi kwa maafisa na wapiganaji wanaofanya kazi Chuo cha Mafunzo Wete/Tungamaa litaondoka kwani maafisa na wapiganaji wengi hulazimika kukodi nyumba uraiani ambako chumba kwa sasa ni *Shilingi za Kitanzania 25,000* wakati wao wanalipwa posho la nyumba *Shilingi za Kitanzania 10,000* kwa sasa tatizo hili linaelekea ukingoni.

Vilevile, kukamilika kwa mradi huu utaondoa pia tatizo la kuleta manunguniko makubwa kwa askari wetu ambao baadhi yao huja na familia zao na hivyo kulazimika kukodi chumba zaidi ya kimoja.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI KWA IDARA HIZI

(i) Kamati **inawashauri** viongozi wanaosimamia ujenzi huu kuhakikisha kuwa wanatekeleza majukumu yao kwa uadilifu mkubwa majengo yanayojengwa

yaweze kuwa na ubora unaotakiwa na kupelekea kudumu kwa kipindi kirefu na kuhakikisha kuwa fedha za wananchi zinatumika ipasavyo na kupatikana thamani ya fedha hizo.

(ii) Kamati **inashauri**kukamilika kwa wakati kwa mradi huu ili kuepusha kutokewa ni mvua za masika yanayokuja ili kuepuka uharibifu utakaoweza kusababishwa na mvua hizo.

(iii) Kamati **inaushauri** uongozi wa Kambi ya Kojani kuhakikisha kuwa eneo la wazi liliopo katika Kambi hiyo lipandwe miti ya bustani na matunda ili kupunguza kasi ya jua pamoja na upepo ambao unaweza kuathiri matumizi endelevu ya majengo haya.

(iv) Kamati inawashauri askari wote katika vituo hivi kuwa rafiki na mazingira yao katika kuyadumisha kiusafi na kimaendeleo.

(v) Sambamba na hayo, juhudi za ziada zitahitajika katika kusimamia na kuhifadhi matumizi ya nyumba hizi ili ziweze kutumika siku hadi siku katika ubora wake.

(vi) Kamati inaona kuwa litakuwa ni jambo la busara baada ya kukamilika ujenzi huu, Serikali kuwapatia samani (furniture) mpya katika nyumba zote za maafisa na kwa yale mahanga ili kwenda sambamba na majengo na vifaa vyake.

(vii) Kamati inazidi kutoa **msisitizo** kwaWizara kwa kushirikiana na Idara Maalum za SMZ kutafuta Hatimiliki za maeneo yote ya kambi ambazo hazijapata Hati kisheria.

SEHEMU YA NNE

4. HITIMISHO

Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum katika kipindi chote cha mwaka *mmoja (1),* imeweza kufanya mizunguko katika kila *robo mwaka*kwa wizara zilizochini ya Kamati hii na kutoa maoni, maagizo na maelekezo ambayo inatarajia yatawasaidia katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku, hatua ambayo italeta manufaa kwa wananchi na Serikali kwa ujumla.

Vilevile, Kamati inampongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. ali Mohammed Shein kwa kusimamia vizuri katika uendeshaji wa Vikosi vyetu. Aidha, Kamati inashauri Serikali Kuu kulifanyia kazi tatizo kubwa la makaazi (Mahanga) ya askari wetu, kwani hivi sasa tayari vikosi vya KMKM na Mafunzo wameshaanza Mradi wa ujenzi wa Mahanga baada ya kuwezeshwa na Serikali, Kamati imeridhika sana na utekelezaji huu wa Serikali.
Ni matarajio yetu kwamba matatizo ya usafiri, nguo pamoja na viatu vya askari wetu nayo, pia yatapatiwa ufumbuzi wake hivi karibuni.

Aidha, Kamati inashauri Serikali kusimamia kikamilifu utekelezwaji wa Sera ya Ugatuzi katika Taasisi zote ambazo zimeridhiwa kuanza kutekeleza Ugatuzi, ni imani ya Kamati hii kuwa maendeleo makubwa yatafikiwa endapo malengo ya Ugatuzi yatasimamiwa na kuthaminiwa na kila mmoja miongozi mwetu.

Pia, Kamati inatoa ushauri kwa Wizara kuwasilisha kwa wakati taarifa zao au ripoti zinazohitajika mbele ya Kamati ili kuepusha usumbufu usio wa lazima, pamoja na ushauri huo Kamati inawapongeza sana Mawaziri na Manaibu waziri, Maafisa Wadhamini wa wizara zote mbili pamoja na Wakuu wa Vikosi vya Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutoa mashirikiano yao mazuri kwa Kamati, na ni matuamini yetu kuwa ushirikiano huo utaendelea.

Kamati inatoa shukurani zake za dhati kwa Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Katibu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar pamoja na watendaji wengine wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Kamati katika kipindi chote ambacho Kamati ilitekeleza majukumu yake na inawaomba waendelee kutoa ushirikiano kila itakapohitajika.